

Lialona



**Ni Yeye Pekee
Angeweza Kuwa
Mwokozi Wetu, uk. 8**

**Ni Kweli Zipi Tunazo Jifunza kuhusu
Mwili kutokana na Ufufuko? uk. 14**

**Kutafuta Uhuru kutokana na Mizigo
ya Unyanyasaji wa Kijinsia, uk. 22**

**Mjue Adui Yako: Jinsi ya Kuhimili
Mikakati Minne ya Shetani, uk. 30**



Wafanyakazi wanaweka alama katika eneo la ujenzi wa Hekalu la Bern Switzerland. Hekalu hilo liliveweka wakfu Septemba 1955 na Rais David O. McKay. Lilikuwa hekalu la kwanza kujengwa nje ya Amerika ya Kaskazini na ni la kwanza kufanya ibada katika lugha nyingine zaidi ya Kiingereza.

Picha kwa Hisani ya Maktaba ya Historia ya Kanisa



UJUMBE

- 4 Ujumbe wa Urais wa Kwanza: Wenye Haki Wataishi kwa Imani**
Na Rais Dieter F. Uchtdorf
- 7 Ujumbe wa Mwalimu Mtembeleaji: Kiapo na Agano la Ukuhani**



JUU YA JALADA
Wakina Maria Watatu wakiwa Kaburini,
na William-Adolphie Bouguereau

MAKALA YA HABARI MAALUMU

- 8 Upatanisho wa Mwokozi: Msingi wa Ukristo wa Kweli**
Na Mzee Robert D. Hales
Kwa sababu Yeye anaishi, sisi wote tutaishi tena.
- 14 Kufufuka kwa Yesu Kristo na kweli kuhusu Mwili Wake**
Na David A. Edwards
Ufufuko wa Yesu Kristo hutufundisha kweli muhimu kuhusu asili takatifu na ya milele ya mwili.
- 22 Daraja la kwenda kwenye Tumaini na Uponyaji**
Na Nanon Talley
Jinsi gani wewe au mpendwa wako mnaweza kupata amani, matumaini, na uponyaji baada ya kitu kiovu na cha kutia kiwewe kama unyanyasaji wa kijinsia?

- 28 Albamu ya Zamani ya Familia: Nguvu ya Hadithi za Familia**
Na Amrieris Puscasu
Hadithi n maisha ya mababu zangu vinaendelea kuniimarisha.
- 30 Vita inaendelea**
Na Mzee Larry R. Lawrence
Mzee Lawrence anaelezea mikakati minne kati ya mikakati ya Shetani na jinsi ya kujikinga nayo.

IDARA

- 20 Muziki: Njooi, Njooi Kwake**
na Steven K. Jones na Michael F. Moody
- 38 Taswira za Imani: Skaidrite Bokuma**
- 40 Sauti za Watakatifu wa Siku za Mwisho**
- 80 Mpaka Tutakapo Kutana Tena: Nguvu za Mungu.**
Na Mzee Bruce R. McConkie



44 Kuelewa Baraka Yako ya Kipatriaki

Na Allie Arnell na Margaret Willden
Baraka za Kipatriaki ni kama ramani za barabara zetu binafsi. Hapa ni baadhi vidokezo kwa ajili ya kuongoza njia zako.

48 Kujitayarisha kwa ajili ya Safari Mpya

Na Karina Martins Pereira Correia de Lima
Mashaka na woga kuhusu kuanza familia yangu mwenyewe kunanitia wasiwasi. Ningeweza kupata amani?



Tazama kama unaweza kuiona Liahona iliyofichwa katika toleo hili. Dokezo: Je inang'ara?

50

50 Naweza kujifunza Akilini mwangu na Moyoni mwangu?

Njia ya Bwana ni ipi ili kupata majibu ya maswali yangu na uelewa mzuri wa maandiko?

52 Fanya Ujumbe kuwa Wako katika Kujifunza Kwako Injili

Jifunze jinsi unavyoweza kuutumia vyema zaidi muda wako wa mafunzo ya injil.

56 Majibu kutoka kwa Viongozi wa Kanisa: Jinsi ya Kupata Amani ya Kweli

Na Mzee Quentin L. Cook

57 Vitabu vilivyo Sahaulika, Ushuhuda Unaokumbukwa

Na Abigail D. Ferrer
Siku niliyombwa kuelezea taarifa kuhusu Kanisa ndiyo siku hiyo hiyo nilisahau vitabu vyangu vya Kanisani. Je maneno yangu ya kawaida yangetosha?

58 Wao walimwona

Soma shuhuda hizi za Mwokozi mfufuka na ona jinsi wewe unavyoweza kuwa shahidi wa Kufufuka Kwake pia.

62 Nafasi Yetu

63 Bango: Songa Mbele, Askari wa Kikristo

64 Maswali na Majibu

Je ni kwa Namna Gani naweza kujua Mungu anasikiliza maombi yangu?



66 Andrea na Neno Baya

Na Julie C. Donaldson
Neno moja dogo baya lisingekuharibu sana, sawa?

68 Majibu kutoka kwa Mtume: Ninaweza kuisaidia familia yangu kuwa imara?

Na Mzee David A. Bednar

69 Jitayarisha kwenda Hekeluni Kila Siku

Na Joy D. Jones
Jifunze kuhusu jinsi Dada Jones alivyoweza lengo muhimu.

70 Star anang'ara

Na Jane McBride
Star alikuwa na woga kuhusu kwenda darasa la watoto wa Msingi. Je angeweza kumpata rafiki?

72 Kuwa Nuru!

Na Elizabeth Pinborough
Njia nane za kuwa rafiki mwema.

73 Vigogo wa Historia ya Kanisa: Kueneza Injili

74 Kumfikiria Yesu

Na Lindsay Tanner
Mia anajifunza kuhusu sakramenti.

76 Hadithi za Yesu: Yesu alitupa Sakramenti

Na Kim 'Webb Reid

79 Maua meupe ya Pasaka



Gazeti la Kimataifa la Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

Urais wa Kwanza: Thomas S. Monson, Henry B. Eyring, Dieter F. Uchtdorf

Akidi ya Mitume Kumi na Wawili: Russell M. Nelson, Dallin H. Oaks, M. Russell Ballard, Robert D. Hales, Jeffrey R. Holland, David A. Bednar, Quentin L. Cook, D. Todd Christofferson, Neil L. Andersen, Ronald A. Rasband, Gary E. Stevenson, Dale G. Renlund

Mhariri: Joseph W. Sitati

Wahariri Wasaidizi: Randall K. Bennett, Carol F. McConkie
Washauri: Brian K. Ashton, Jean B. Bingham, LeGrand R. Curtis Jr., Christoffel Golden, Douglas D. Holmes, Erich W. Kopischke, Larry R. Lawrence, Carole M. Stephens

Mkurugenzi Mtendaji: Peter F. Evans

Mkurugenzi wa Magazeti ya Kanisa: Allan R. Loyborg
Meneja wa Biashara: Garff Cannon

Mhariri Mtendaji: Adam C. Olson

Mhariri Mtendaji Msaidizi: Ryan Carr

Mchapishaji Msaidizi: Cremilda Amaral

Kuandika na kuhariri: Bethany Bartholomew, Brittany Beattie, David Dickson, David A. Edwards, Matthew D. Flitton, Lori Fuller, Garrett H. Garff, LaRene Porter Gaunt, Charlotte Larcabal, Michael R. Morris, Eric B. Murdock, Sally Johnson Odekerk, Joshua J. Perkey, Jan Pinborough, Richard M. Romney, Mindy Anne Selu, Marissa Widdison

Mkurugenzi Mtendaji Sanaa: J. Scott Knudsen

Mkurugenzi wa Sanaa: Tadd R. Peterson

Usanifu: Jeanette Andrews, Fay P. Andrus, C. Kimball Bott, Thomas Child, David Green, Colleen Hinckley, Eric P. Johnson, Susan Lofgren, Scott M. Mooy, Mark W. Robison, Rachel Smith, Brad Teare, K. Nicole Walkenhorst

Mratibu wa Haki Miliki: Collette Nebeker Aune

Meneja wa Uzalishaji: Jane Ann Peters

Uzalishaji: Glen Adair, Connie Bowthorpe Bridge, Julie Burdett, Bryan W. Gygi, Ginny J. Nilson, Gwyle Tate Rafferty, Derek Richardson

Kabla ya Chapa: Joshua Dennis, Ammon Harris

Mkurugenzi wa Uchapishaji: Steven T. Lewis

Mkurugenzi wa Usambazaji: Troy K. Vellinga

Kwa usajili na bei nje ya Marekani na Kanada, nenda store.lds.org au wasiliana na kituo cha usambazaji cha Kanisa katika eneo lako ama kiongozi wa kata au tawi.

Kuwasilisha miswada na maswali mitamboni katika liahona.lds.org; na barua pepe liahona@ldschurch.org; ama kwa barua Liahona, Rm. 2420, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150-0024, USA.

Liahona (meno katika Kitabu cha Mormon linalomaanisha "dira" ama "kielekezi") imechapishwa katika Kialbeni, Kiarmeni, Bislama, Kibulgaria, Kikambodia, Kisebuano, Kichina, Kichina (kilichorahisishwa), Kikroeshia, Kicheki, Kidenishi, Kiholanzi, Kiingereza, Kiestoni, Kifiji, Kifinishi, Kifaransa, Kijerumani, Kigiriki, Kianguya, Kiaislandi, Kiindonesia, Kiitaliano, Kijapani, Kikiribati, Kikorea, Kilatvia, Kilithuania, Kimalagasi, Kimarshali, Kimongolia, Kinorwei, Kipolishi, Kireno, Kiromania, Kirusi, Kisamoa, Kislovenia, Kihispania, Kiswahili, Kiswidi, Kitagalogi, Kitahiti, Kithai, Kitonga, Kiukreni, Kiurdu, na Kivietnamu. (Masafa hutofautiana kwa lugha.)

© 2017 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa Limepigwa chapaMarekani.

Tarifa ya Hakimiliki: Isipokuwa imeelezwa vinginevyo, watu binafsi wanaweza kunakili yaliyomo katika Liahona hii kwa matumizi yao binafsi, yasiyo ya kibishara (ikijumuisha kwa mito ya Kanisa). Haki hiyo yaweza kuondolewa wakati wa wote. Kazi za picha zisinakiliwe kama kuna zuio linaloeleza hivyo kwenye mstari pembeni ya mchoro. Maswali juu ya hakimiliki yaelekezwe kwa Intellectual Property Office, 50 E. North Temple St., FL 13, Salt Lake City, UT 84150, USA; email: cor-intellectualproperty@ldschurch.org.

For Readers in the United States and Canada:

April 2017 Vol. 4 No. 1. LIAHONA (USPS 311-480) Swahili (ISSN 2326-3695) is published once a year (April) by The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150. USA subscription price is \$1.00 per year; Canada, \$1.20 plus applicable taxes. Periodicals Postage Paid at Salt Lake City, Utah. Sixty days' notice required for change of address. Include address label from a recent issue; old and new address must be included. Send USA and Canadian subscriptions to Salt Lake Distribution Center at address below. Subscription help line: 1-800-537-5971. Credit card orders (American Express, Discover, MasterCard, Visa) may be taken by phone or at store.lds.org. (Canada Post Information: Publication Agreement #40017431)

POSTMASTER: Send all UAA to CFS (see DMM 507.1.5.2). NONPOSTAL AND MILITARY FACILITIES: Send address changes to Distribution Services, Church Magazines, P.O. Box 26368, Salt Lake City, UT 84126-0368, USA.

Mawazo kwa ajili ya Jioni ya Familia Nyumbani

Toleo hili lina makala na shughuli ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya jioni ya familia nyumbani lfuatayo ni mifano miwili.



“Wao Walimuona Yeye,” ukurasa wa 58:

Ina maana gani kuwa shahidi wa Kristo? Baada ya kusoma kifungu kama familia, unaweza kujadili njia unayoweza kuwa shahidi wa Kristo hata bila ya kumwona Yeye kwa macho. Unaweza kufikiria wazo la kuwa karibu na Mwokozi kama vile kutafuta nafasi ya kuwahudumia wakimbizi katika jumuiya yako, kujifunza kuhusu maisha ya Mwokozi wakati wa kusoma maandiko, kukaa na mtoto ili wana ndoa waweze kwenda hekaluni, au kumfikia rafiki mwenye shida. Pia unaweza kutazama Video inayopakana kwenye mormon.org/ easter na kutafakari umuhimu wa Kristo na Ufufuko Wake katika maisha yetu.

“Kujiandaa kwa ajili ya Hekalu Kila Siku,”

ukurasa wa 69: Dada Joy D. Jones anatukumbusha sisi umuhimu wa kulifanya hekalu kuwa kipaumbele katika maisha yetu na kufanya kazi ya historia ya familia ili kutusaidia sisi kujiandaa kuingia. Unaweza kufikiria kuwa na “usiku wa historia ya familia na hekalu” kwa ajili ya jioni ya familia nyumbani Unaweza kujifunza jinsi ya kuorodhesha majina na kutafuta kumbu kumbu za familia au kujadili umuhimu wa ibada za hekaluni na kuangalia picha za mahekalu yaliyoko ulimwenguni kote. Kama unaishi karibu na hekalu, unaweza kutembelea maeneo ya hekalu na kujadili jinsi ambavyo mahekalu yanavyoweza kutuleta karibu na Baba wa Mbinguni na kutusaidia kuhisi upendo Wake.

ZAIDI KWENYE MTANDAO

Liahona na nyenzo zingine za Kanisa zinapatikana katika lugha nyingi kwa languages.lds.org. Tembelea [facebook.com/liahona.magazine](https://www.facebook.com/liahona.magazine) (Inapatikana katika Kingereza, Kireno, na Kihispania) kupata ujumbe wenye maongozi, dhana kwa ajili ya jioni ya familia nyumbani, na mambo mengine ambayo unaweza kushirikiana na rafiki zako na familia yako.

MADA KATIKA TOLEO HILI

Nambari zinawakilisha ukurasa wa kwanza wa makala.

Amani, 48, 56, 62, 66

Baraka za Kipatriaki, 44

Familia, 28, 42, 48, 68

Historia ya familia, 28

Historia ya Kanisa, 73

Huduma, 4, 42, 68

Imani, 4, 38, 41, 48, 80

Kuabudu Hekaluni, 69

Kujifunza maandiko, 43, 52, 57

Lugha, 40, 66

Maagano, 7

Maarifa, 50, 52

Majaribu, 30, 63

Maombi, 41, 62, 64

Mfano, 72

Mwili, 14

Nguvu za Kiroho, 4, 30,

63, 80

Pasaka, 14, 58, 76, 79

Roho Mtakatifu, 50

Sakramenti, 74, 76

Tumaini, 22, 48

Ufufuko, 8, 14, 58, 76, 79

Ujasiri, 40, 57, 63

Ukuhani, 7, 80

Unyanasaji wa

Kijinsia, 22

Upatanisho, 8, 22, 74, 76

Uponyaji, 22

Urafiki, 70, 72

Ushuhuda, 38, 50, 57, 58

Uzima wa milele, 8, 14

Yesu Kristo, 8, 14, 30, 56,

58, 74, 76, 79



**Na Rais
Dieter F. Uchtdorf**

Mshauri wa Pili katika
Urais wa Kwanza

WENYE HAKI WATAISHI KWA IMANI

Rabi na Mtengeneza Sabuni

Kuna hekaya ya kale ya Kiyahudi kuhusu mtengeneza sabuni ambaye hakumwamini Mungu. Siku moja akiwa anatembea na rabi, alisema, “Kuna kitu nisichoweza kukielewa. Tumekuwa na dini kwa maelfu ya miaka. Lakini kila unakoangalia kuna maovu, ufisadi, udanganyifu, udhalimu, maumivu, njaa, na vurugu. Inaonekana kwamba dini haijausaidia ulimwengu kabisa. Hivyo nakuuliza wewe, ina uzuri gani?”

Rabi hakujibu kwa muda bali aliendelea kutembea na mtengeneza sabuni. Hatimaye walikaribia uwanja wa michezo ambapo watoto, wakifunikwa na vumbi, walikuwa wanachezea udongo.

“Kuna kitu sikielewi,” rabi alisema. “Waangalie wale watoto. Tumekuwa na sabuni kwa maelfu ya miaka, na bado wale watoto ni wachafu. Nini uzuri wa sabuni?”

Mtengeneza sabuni akajibu, “Lakini rabi, si sahihi kulaumu sabuni kwa ajili ya watoto hawa wachafu. Sabuni inabidi itumike kabla haijatimiza malengo yake.”

Rabi yule akatabasamu na akasema, “Kabisa.”

Jinsi Gani Tunapaswa Kuishi?

Mtume Paulo, akimnukuu nabii wa Agano la Kale, alifanya muhtasari ina maana gani mwenye kuamini pale alipandika, “Mwenye haki ataishi kwa imani” (Warumi 1:17).

Huenda katika maelezo haya rahisi tunaolewa tofauti kati ya dini ambayo ni dhaifu na isiyo jiamini na ile ambayo ina nguvu na inabadilisha maisha.

Lakini ili kuelewa ina maana gani kuishi kwa imani, ni lazima tuelewe imani ni nini.

Imani ni zaidi ya kuamini. Ni kumwamini kabisa Mungu kukiambatana na matendo.

Ni zaidi ya kutamani.

Ni zaidi ya kukaa nyuma, tukiinamisha vichwa vyetu, na kusema tunakubali. Tunaposema “mwenye haki kwa *imani ataishi*,” tuna maana tunaongozwa na kuelekezwa na imani yetu. Sisi *hutenda* kwa njia ambayo inaendana na imani yetu—siyo nje ya mawazo yasiyo ya utiifu bali katika kujiamini na upendo wa kweli kwa Mungu wetu na kwa hekima isiyo na thamani Yeye amefunua kwa watoto Wake.

Imani lazima iambatane na matendo; vinginevyo haina maisha (ona Yakobo 2:17). Sio imani kabisa. Haina nguvu ya kumbadilisha hata mtu mmoja, achilia mbali ulimwengu.

Wanaume na wanawake wenye imani wanaamini katika huruma ya Baba yao wa Mbinguni—hata wakati wa mashaka, hata wakati wa wasiwasi na shida wakati wasipona vizuri au kuelewa vizuri.

Wanaume na wanawake wenye imani wanatembea njia ya ufuasi na kujitahidi kufuata mfano wa Mwokozi wao mpendwa, Yesu Kristo. Imani inatia hamasa na, hakika, inatusukuma kuelekeza mioyo yetu mbinguni na kuwafikia, kuwainua, na kuwabariki wanadamu wenzetu.

Dini bila matendo ni kama sabuni ambayo imebaki kwenye boksi. Inaweza kuwa na umuhimu wa ajabu, lakini kwa uhakika ina nguvu kidogo ya kuleta tofauti hadi itakapotimiza majukumu yake. Injili iliyorejeshwa ya Yesu Kristo ni injili ya matendo. Kanisa la Yesu Kristo linafundisha dini ya kweli kama ujumbe wa matumaini, imani, na hisani, ikijumuisha kuwasaidia wanadamu wenzetu katika njia za kiroho na kimwili.

Miezi michache iliyopita, mke wangu, Harriet, na mimi tulikuwa kwenye safari ya kifamilia pamoja na baadhi ya watoto wetu katika eneo la Mediterania. Tulitembelea



Rais Uchtdorf na binti yake Antje, waliwatembelea wakimbizi katika kambi jirani na Athens, Ugiriki.

baadhi ya makambi ya wakimbizi na kukutana na familia zilizotoka kwenye nchi zenye vita. Watu hawa hawakuwa wa imani yetu, lakini walikuwa kaka na dada zetu na walihitaji msaada wa haraka. Mioyo yetu iliguswa sana wakati tulipoona kwa macho yetu jinsi imani hai ya waumini wetu wa Kanisa ilivyoleta msaada, faraja, na tumaini kwa wenzetu wenye shida, bila kujali dini, taifa, au elimu yao.

Imani ikiunganishwa pamoja na matendo inajaza moyo kwa wema, akili pamoja na hekima na kuelewa, na nafsi pamoja na amani na upendo.

Imani yetu inaweza kubariki na kwa haki ikashawishi wale wanaotuzunguka na sisi wenyewe.

Imani yetu inaweza kuujaza ulimwengu kwa mema na amani.

Imani yetu inaweza kubadilisha chuki kuwa upendo na maadui kuwa marafiki.

Wenye haki, kisha, huishi kwa imani; wanaishi kwa kumwamini Mungu

na kutembea katika njia Yake.

Na hiyo ndiyo aina ya imani ambayo inaweza kumbadilisha mtu mmoja mmoja, familia, mataifa, na ulimwengu. ■

KUFUNDISHA KUTOKANA NA UJUMBE HUU

Raisi Uchtdorf anaelezea kwamba imani ni zaidi ya onyesho la kusa-diki. Imani ya kweli kwa Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo inahitaji matendo, na kuishi kwa imani kuna nguvu ya kubadilisha maisha na nyumba zetu. Unaweza kuwaalika wale unaowafundisha kuelezea matukio wakati walipoona baraka na nguvu za kuishi kwa imani—kupitia mfano wake binafsi au kwa kuwaona wengine. Watie moyo ili waombe kwa ajili ya kuongozwa ili kujua njia nzuri ya kuishi injili.

Kuwahudumia Wengine katika Imani

Rais Uchtdorf anatuambia sisi kwamba imani yetu kwa Mungu *lazima* "iambatane na matendo." Wakati imani yetu "imefungwa nira pamoja na tendo endelevu," anaelezea, "huijaza . . . nafsi kwa amani na upendo." Pamoja na ahadi ya baraka hii, sisi *tunaweza* kuleta tofauti, na tunaweza kuona hili katika maisha yetu kama tunachukua muda wetu kufanya huduma iliyojaa-imani. Unaweza kuomba kila asubuhi ili kumwomba Bwana msaada katika kuwatumikia wengine. Kwa mfano, muombe Yeye akuonyeshe wakati ndugu zako wanahitaji msaada wa kazi ndogo ndogo au wakati rafiki anahitaji kupongezwa. Kisha, wakati unapokea msukumo utendee kazi! Kama ukiyafanya maombi na huduma hii kuwa tabia, ndipo, matendo yako ya uaminifu na endelevu yatabariki maisha yako na maisha ya wengine. Rais Uchtdorf ameahidi kwamba wewe "unaweza kuwabadilisha watu, familia, mataifa, na ulimwengu."




WATOTO

Amini

Jaribu shughuli hii pamoja na rafiki. Unatakiwa kuamini na kufuata mwongozo wao kwa uangalifu.

Kwa kalamu au penseli katika mkono wako, fumba macho yako. Acha rafiki yako akuambie wapi kwa kuchora macho, pua, mdomo, na nywele katika sura hii. Kisha angalia. Inaonekana namna gani? Unaweza kupaka rangi usoni na kuchora nyingine ili kucheza tena!

Wakati mwingine ni vigumu kufuata maelekezo. Lakini wakati tunapojaribu kumfuata Baba wa Mbinguni kwa kumsikiliza Roho Mtakatifu, Yeye atatusaidia. Tunaweza daima kumwamini Yeye.



Kiapo na Agano la Ukuhani

Kwa maombi jifunze maneno haya na utafute maongozi ili kujua kitu cha kufundisha. Ni kwa namna gani kuelewa lengo la Muungano wa Usaidizi wa Wakina Mama kutawatayarisha mabinti wa Mungu kwa ajili ya baraka za uzima wa milele?

Jinsi sisi kama kina dada tuna-
vyozidi kuelewa ya kwamba
kiapo na agano la ukuhani
inatuhusu sisi, ndivyo tutakavyo-
zidi kupokea baraka na ahadi za
ukuhani.

Mzee M. Russell Ballard
wa Akidi ya Mitume Kumi na
Wawili amesema, “Wote ambao
wamefanya maagano matakati-
fu na Bwana na wanaheshimu
maagano hayo wanastahili
kupokea ufunuo binafsi, kuba-
rikiwa kwa huduma ya malaika,
na kuzungumza na Mungu,
kupokea utimilifu wa injili, na,
hatimaye, kuwa warithi ubavuni
mwa Yesu Kristo kwa yote Baba
aliyo nayo.”¹

Baraka hizo na ahadi hizo
za kiapo na agano la uku-
hani ni kwa wote wanaume
na wanawake Dada Sheri L.
Dew, aliyekuwa mshauri kati-
ka Urais Mkuu wa Muungano
wa Usaidizi wa Wakina Mama,
alisema, “Utimilifu wa ukuhani



Imani
Familia
Usaidizi

uliomo katika ibada za nyumba
ya Bwana unaweza kupokelewa
tu na mwanaume na mwanam-
ke kwa pamoja.”²

Dada Linda K. Burton,
Rais Mkuu wa Muungano wa
Usaidizi wa Wakina Mama, ame-
toa wito huu, “Ninawaaliken
mkariri kiapo na agano la uku-
hani, ambalo linaweza kupa-
tikana katika Mafundisho na
Maagano 84:33–44. Kwa kufa-
nya hivyo, ninawaahidi ya kwa-
mba Roho Mtakatifu atapanua
uelewa wenu juu ya ukuhani na
kuwapa maongozi na kuwainua
kwa njia za ajabu.”³

Mafundisho ya Joseph Smith
kwa Muungano wa Usaidizi wa
Wakina Mama yalikuwa na lengo
la kuwatayarisha “kuja katika
kumiliki, kupokea fadhila &
baraka & vipawa vya ukuhani.”

Haya yangeweza kutimizwa kwa
njia ya ibada za hekaluni.

“ibada za hekaluni [ni] ibada
za ukuhani, lakini [hazi] tunukii
ofisi ya kichungaji juu ya wana-
ume au wanawake. [ibada hizi
zinatimiza] ahadi ya Bwana kwa-
mba watu wake—wanawake na
wanaume—watajaliwa na uwezo
kutoka juu. [M&M 38:32].⁴

Nyongeza ya Maandiko na Taarifa
Mafundisho na Maagano 84:19–40;
121:45–46; reliefsociety.lds.org

MUHTASARI

1. M. Russell Ballard, “Men and Women and Priesthood Power,” *Liahona*, Sept. 2014, 36.
2. Sheri L. Dew, katika *Daughters in My Kingdom: The History and Work of Relief Society* (2011), 128.
3. Linda K. Burton, “Priesthood Power—Available to All,” *Ensign*, Juni 2014, 39–40.
4. Mada za Injili, “Joseph Smith’s Teachings about Priesthood, Temple, and Women,” topics.lds.org.



Fikiria Hili

Unaweza
kufanya nini
ili uweze
kuelewa
kikamilifu na
kupata bara-
ka zilizoahidi-
wa za kiapo
na agano la
ukuhani?



GETHESEMANE, BY J. KIRK RICHARDS

Upatanisho wa Mwokozi:

MSINGI WA UKRISTO WA KWELI

*Sisi sote tutafufuliwa na kuishi milele kwa sababu
ya dhabihu ya Yesu Kristo ya kulipia dhambi.*

Nabii Joseph Smith (1805–44) aliulizwa, “Ni zipi kanuni za kimsingi za dini yako?” Yeye alijibu “Kanuni za msingi za dini yetu ni ushuhuda wa Mitume na Manabii, kuhusu Yesu Kristo, kwamba alikufa, akazikwa, na akafufuka tena siku ya tatu, na amepaa mbinguni; na mambo yote mengine ambayo yanahusiana na dini yetu ni viambatisho tu.”¹

Ninataka kutoa sauti yangu juu ya kauli ya Nabii Joseph. Kitovu cha yote tunayoamini ni Mwokozi na dhabihu Yake ya kulipia dhambi zetu—“ufadhili wa Mungu” (1 Nefi 11:16) ambapo Baba alimtuma Mwana Wake duniani kutimiza Upatanisho. Kitovu cha kusudio la maisha ya Yesu Kristo lilikuwa ni kukamilisha dhabihu ya kulipia dhambi. Upatanisho ni msingi wa Ukristo wa kweli.

Ni kwa nini Upatanisho wa Mwokozi ni kanuni kuu katika Kanisa na maishani mwetu?

Makala ya Imani 1:3

Makala ya tatu ya imani inasema, “Tunaamini kwamba kwa njia ya Upatanisho wa Kristo, wanadamu wote wanaweza kuokolewa, kwa kutii sheria na ibada za Injili.”

“Kuokolewa” katika muktadha huu ina maana kufikia kiwango cha juu zaidi cha utukufu katika ufalme wa selestia. Ufufuko umetolewa kwa kila anayekuja duniani, lakini ili kupokea uzima wa milele, zile baraka kamili za makuzi ya milele, kila mtu ni lazima atii sheria, apokee ibada, na afanye maagano ya injili.

Kwa nini ni Yesu Kristo, na ni Yeye pekee, ambaye aliweza kulipia dhambi za ulimwengu? Yeye ndiye aliyekuwa na sifa zote.



**Na Mzee
Robert D. Hales**
Wa Akidi ya
Mitume Kumi
na Wawili

Mungu Alimpenda na Kumwamini

Yesu alizaliwa kwa Wazazi wa Mbinguni katika ulimwengu wa kabla ya duniani. Yeye alikuwa Mzaliwa wa Kwanza wa Baba yetu wa Mbinguni. Yeye aliteuliwa kutokea mwanzo. Alikuwa mtiifu kwa mapenzi ya Baba Yake. Maandiko mara nyingi huzungumzia furaha ya Baba wa Mbinguni aliyo nayo kwa Mwana Wake.

Katika Mathayo tunasoma, “Na lo, akasikia sauti kutoka mbinguni, ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye” (Mathayo 3:17).

Luka anaandika, “Sauti ikatoka katika wingu, ikisema, Huyu ni Mwanangu, mteule wangu, msikieni yeye” (Luka 9:35).

Na hekaluni katika nchi ya Neema kufuatia Ufufuko wa Mwokozi, watu waliisikia sauti ya Baba: “Tazama Mwana wangu Mpendwa ninayependezwa na yeye” (3 Nefi 11:7).

Hilo hasa linagusa moyo wangu wakati ninaposoma kwamba wakati Yesu alipokuwa akiteseka katika Bustani ya Gethsemani, Baba, kutokana na upendo Wake mkubwa na huruma kwa Mwana Wake wa Pekee, alimtuma malaika amfariji na amuimarisha (ona Luka 22:43).

Yesu Alitumia Haki yake ya Kujiamulia Kutii

Yesu Alihitajika kutoa uhai Wake kwa hiari Yake kwa ajili yetu.

Katika Baraza kuu la Mbinguni, Lusiferi, “mwana wa asubuhi” (Isaya 14:12; M&M 76:26–27), alisema:

Tazama, niko hapa, nitume mimi, nitakuwa mwanao, nami nitawakomboa wanadamu wote, ili hata nafsi moja isipotee, na hakika nitatenda hivyo; kwa sababu hiyo nipe mimi heshima yako.

“Walakini, tazama, Mwanangu Mpendwa, ambaye alikuwa Mpendwa na Mteule tangu mwanzo, aliniambia—Baba, mapenzi yako na yatimizwe, na utukufu uwe wako milele na milele” (Musa 4:1–2; ona pia Ibrahimu 3:27).

Kwa sababu ya upendo mkubwa Mwana alio nao kwa Baba Yake na kwa kila mmoja wetu, Alisema, “Nitume mimi. Wakati Aliposema “nitume mimi, Alitumia haki Yake ya kujiamulia.

Kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba. Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo.

“Ndiposa Baba anipenda, kwa sababu nautoa uhai wangu ili niutwae tena.

“Hakuna mtu aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe. Nami ninao uweza wa kuutoa, ninao na uweza wa kuutwaa tena. Agizo hilo nalilipokea kwa Baba yangu.” (Yohana 10:15, 17–18).

Kama Mwokozi angelitaka, majeshi ya malaika wange-weza kumtoa msalabani na kumpeleka moja kwa moja hadi kwa Baba Yake. Lakini alitumia haki Yake ya kujiamulia ili kujitoa dhabihu kwa ajili yetu, kukamilisha misheni Yake katika mwili wenye kufa, na kustahmili hadi mwisho, akikamilisha dhabihu ya kulipia dhambi.

Yesu alitaka kuja duniani, na Alikuwa mwenye sifa zilizostahili. Na wakati Alipokuja, Alisema, “Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka.” (Yohana 6:38).

Yesu Aliteuliwa Kabla

Petro alifundisha kwamba Yesu “naye amejulikana kweli tangu zamani, kabla haijawekwa misingi ya dunia” (ona 1 Petro 1:19–21).

Manabii katika vipindi vyote vya maongozi ya Mungu walitabiri kuhusu kuja kwa Yesu Kristo na lengo la Misheni Yake. Kwa njia ya imani kubwa, Henoko alionyeshwa maono ya ajabu kuhusu kuzaliwa, kufa, Kupaa, na Ujio wa Pili wa Mwokozi:



ECCE HOMO. BY J. KIRK RICHARDS

Na tazama, Henoko aliiona siku ile ya kuja kwa Mwana wa Mtu, hata katika mwili; na roho yake ilifurahia, akisema: Mwenye haki ameinuliwa juu, na Mwanakondoo amechinjwa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu.

“Na Bwana akamwambia Henoko: Angalia, naye akaangalia na akamwona Mwana wa Mtu ameinuliwa juu ya msalaba, kwa jinsi ya wanadamu;

Naye akasikia sauti kubwa; na mbingu zikafunikwa kwa pazia; na viumbe wote wa Mungu waliomboleza; nayo dunia ikiugulia; na miamba kupasuka; na watakatifu waki-amka, na kuvikwa taji mkono wa kuume wa Mwana wa Mtu, kwa mataji ya utukufu.

Na Henoko akamwona Mwana wa Mtu akapaa juu kwa Baba.

Na ikawa kwamba Henoko aliiona siku ya kuja kwa Mwana wa Mtu, katika siku za mwisho, kukaa juu ya dunia katika haki kwa kitambo cha miaka elfu (Musa 7:47, 55–56, 59, 65).

Takriban miaka 75 kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, Amuleki alishuhudia: “Tazama, nawaambia, kwamba najua kwamba Kristo atakuja miongoni mwa watoto wa watu, kujitwalia makosa ya watu, na kwamba atalipia dhambi za ulimwengu; kwani Bwana Mungu amesema” (Alma 34:8).

Yesu Alikuwa na Sifa za Kipekee

Ni Yesu Kristo pekee ambaye angeweza kutekeleza dhabihu ya kulipia dhambi—akiwa amezaliwa na mama mwanadamu, Maria, na akiwa amepokea nguvu za uzima kutoka kwa Baba Yake (ona Yohana 5:26). Kwa sababu ya nguvu hizi za uzima, Alishinda mauti, nguvu za kaburi zilibatilishwa, na akawa Mwokozi na Mpatanishi na Bwana wa Ufufuko—njia ambayo kwayo tunapata wokovu na uwezo wetu sisi sote wa kuishi milele. Tutafufuliwa na kuishi milele kwa sababu ya dhabihu ya Yesu Kristo ya kulipia dhambi.

Yesu kwa Hiari Yake Alilipia Dhambi ya Asili

Makala ya pili ya imani inasema, “Tunaamini kwamba wanadamu wataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao wenye-we, na siyo kwa ajili ya uvunjaji sheria wa Adamu.”

Kupitia matumizi ya haki yetu ya kujiamulia, sisi tunachagua kutumia imani yetu. Kwa bidii, tunaweza kutubu; bila Upatanisho, hatuwezi.



GRAY DAY GOLGOTHA BY J. KIRK RICHARDS

Katika Musa tunafundishwa, “Kuanzia hapa ukaenea msemu miongoni mwa watu, kwamba Mwana wa Mungu amelipia hatia ya asili, ambayo ni kuwa dhambi za wazazi haziwezi kujibiwa juu ya vichwa vya watoto” (Musa 6:54).

Katika 2 Nefi tunapewa mafunzo muhimu sana:

“Kwani kifo kimekuja juu ya wanadamu wote, ili kutimiza mpango wa huruma wa Muumba mkuu, inahitajika lazima pawe na nguvu ya ufufuko, na inahitajika lazima ufufuko umfikie mwanadamu kwa sababu ya anguko; na anguko lilitokana na uvunjaji sheria; na kwa sababu hiyo mwanadamu akawa ameangukaa wakawa wametengwa mbali na uwepo wa Bwana.

“Kwa sababu hivyo, unahitajika kuwe na upatanisho usio na kipimo—bila huu upatanisho usio na kipimo huu uharibifu hauwezi kuvaa kutoharibika. Kwa sababu hivyo, hukumu ya kwanza iliyompata mwanadamu lazima ingekuwa kwa muda usio na mwisho. Na kama ni hivyo, miili hii lazima ingelala chini kuoza na kurudi mavumbini ilikotoka, bila kufufuka tena” (2 Nefi 9:6–7).

Yesu Alikuwa Kiumbe Pekee Mkamilifu

Katika Mafundisho na Maagano, Mwokozi Anasema, “Baba, tazama mateso na kifo chake yeye ambaye hakute-nda dhambi, ambaye ulipendezwa naye; tazama damu ya mwanao iliyomwagika; damu yake yeye ambaye ulimtoa ili upate kutukuzwa” (M&M 45:4).

Yesu ni binadamu wa pekee ambaye alikuwa mkamilifu, bila dhambi. Dhabihu katika Agano la Kale ilikuwa na maana dhabihu ya damu—ikionyesha mbele hadi dhabihu ya Bwana na Mwokozi wetu akiwa msalabani akitimiza dhabihu ya kulipia dhambi. Wakati dhabihu za damu zilizokuwa zikifanywa katika mahekalu ya kale, makuhani walitoa kafara kondoo asiye na ila, mkamilifu katika kila njia. Mwokozi mara nyingi anasomwa katika maandiko kama mwana kondoo wa Mungu kwa sababu ya usafi Wake (ona, kwa mfano, Yohana 1:29, 36; 1 Nefi 12:6; 14:10; M&M 88:106).

Petro alifundisha kwamba tunakombolewa kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo (1 Petro 1:19).

Yesu Kristo Aliziondoa Dhambi za Dunia

Aya zifuatazo zinaonyesha wazi kwamba kwa njia ya Upatanisho Wake, Mwokozi alilipia dhambi zetu:

Sisi sote, kama kondoo, tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake; na Bwana amemwekea maovu yetu sisi sote (Mosia 14:6).

Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwenye sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.

Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake.

Wala si hivyo tu, ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye sasa tumeupokea huo upatanisho.

Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki. (Warumi 5:8, 10–11, 19).

Ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magojwa yetu (Mathayo 8:17).

Lakini Mungu hakomi kuwa Mungu, na rehema hudai wanaotubu, na rehema huja kwa sababu ya upatanisho; na upatanisho huleta ufufuo wa wafu; na ufufuo wa wafu huwarudisha watu kwenye uwepo wa Mungu; na hivyo wanarudishwa kwenye uwepo wake,

kuhukumiwa kulingana na matendo yao, kulingana na sheria na haki.

Na hivyo Mungu hutimiza kusudi lake kubwa na la milele, ambalo lilitayarishwa kutokea msingi wa dunia. Na hivyo huja wokovu na ukombozi wa binadamu, na pia maangamizo yao na taabu. (Alma 42:23, 26).

Yesu Alivumilia hadi Mwisho

Yesu Alivumilia majaribu, mateso, dhabihu, na dhiki za Gethsemani, pamoja na kuteseka kwake kule Golgotha msalabani. Kisha, hatimaye, Aliweza Kusema, Imekwisha (Yohana 19:30). Alikuwa amekamilisha kazi Yake akiwa katika hali ya mauti na kuvumilia hadi mwisho, hivyo basi kukamilisha dhabihu ya kulipia dhambi.

Katika bustani Alisema, Baba yangu, ikiwezekana, kiko-mbe hiki kiniepuka; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe. (Mathayo 26:39).

Katika Mafundisho na Maagano tunafundishwa:

Mateso ambayo yalisababisha Mimi mwenyewe, hata Mungu, mkuu kuliko wote, kutetemeka kwa sababu ya maumivu, na kutoka damu kwenye kila kinyweleo, na kuteseka mwili na roho—na kutamani nisinywe kikombe kichungu, na kusita—

Hata hivyo, utukufu na uwe kwa Baba, na Mimi nika-chukua na kukamilisha maandalizi yangu kwa wanadamu” (M&M 19:18–19).



WAMEMWEKA WAPP? NA J. KIRK RICHARDS

Yesu Alimwambia Baba Yake, “Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye” (Yohana 17:4).

Kisha, msalabani, “basi Yesu alipokwisha kuipokea ile siki, alisema, Imekwisha. Akainama kichwa, akaisalimu roho yake” (Yohana 19:30).

Yesu alikuja duniani, akasalia na Uungu Wake ili Yeye aweze kutekeleza ile dhabihu ya kulipia dhambi, na kuvumilia hadi mwisho.

Mkumbukeni Yeye kwa njia ya Sakramenti

Leo tunakumbuka dhabihu ya Mwokozi ya kulipia dhambi kwa kutumia ishara za maji na mkate—ishara ya mwili na damu Yake—kama ilivyoanzishwa wakati wa Karamu ya Mwisho ya Bwana akiwa na Mitume Wake.

“Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.

“Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula; akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu” (Luka 22:19–20).

Katika Yohana 11:25–26 tunasoma:

“Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi:

“Naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele.”

Tunasoma pia: “Mimi ndimi chakula chenye uzima kilicho shuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakacho toa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu” (Yohana 6:51).

“Uzima wa ulimwengu” ina maana uzima wa milele

Tunahitaji kujitayarisha pamoja na familia zetu kila wiki ili kuwa wenye kustahili kushiriki sakramenti na kujazwa na Roho Mtakatifu.

Baba na Mwana Wanatupenda Sisi

Baba alimtuma Mwanawe duniani—ufadhili—kumruhusu Yeye kusulubiwa na kupitia yale yote ambaye Yeye aliyohitaji kuyapitia. Katika Yohana tunasoma:

Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.

Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba; tangu sasa mnamjua, tena mmemwona (Yohana 14:6–7).



DOUBT NOT, THOMAS, BY J. KIRK RICHARDS

Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu (1 Yohana 4:10).

Kipatanisho inamaanisha maridhiano au kuridhisha.

Hitimisho

Kila anayekuja duniani na kupokea mwili wenye kufa atafufuliwa, lakini ni lazima tufanye bidii ili tupate baraka ya kuinuliwa kupitia uaminifu wetu, haki yetu ya kujiamulia, utiifu wetu, na toba yetu. Huruma itatolewa pamoja na haki, kuruhusu toba.


Kwa sababu tumechagua kumfuata na kumkubali Yesu Kristo kama Mkombozi, tunajichukulia jina Lake juu yetu tunapobatizwa. Tunajichukulia sheria ya utiifu. Tunaahidi ya kwamba tutamkumbuka daima na kushika amri Zake. Tunaweza upya maagano yetu wakati tunapopokea sakramenti.

Kwa kufanya upya maagano yetu, tunapewa ahadi ya Roho Wake kuwa pamoja nasi daima. Ikiwa tutamruhusu Roho Wake aje maishani mwetu na atuongoze, tunaweza kurudi katika uwepo wa Baba wa Mbinguni na Mwanawe, Yesu Kristo, ambao huu ni mpango Wao kwa ajili ya furaha yetu sisi—ule mpango wa wokovu. ■

Kutoka katika hotuba, “The Atonement,” iliyotolewa wakati wa semina ya marais wapya wa misheni katika Kituo cha Mafunzo ya Wamisionari cha Provo mnamo Juni 24, 2008.

MUHTASARI

1. *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* (2007), 49.



Kufufuka KWA Yesu Kristo NA KWELI KUHUSU MWILI

Na Mzee David A. Edwards

Magazeti ya Kanisa

“**A**lisema, Imekwisha: Akainama kichwa, akaisalimu roho yake” (Yohana 19:30). Wakati ule, roho ya Yesu Kristo iliuaacha mwili wake—mwili ambao umevumilia mateso ili kwamba aweze kulipia dhambi za watu wote na kuwasaidia katika udhaifu wao (ona Alma 7:12–13). Mwili ule, sasa ambao ni chombo kitupu, ulitolewa kutoka msalabani, ukaviringishwa katika nguo za kitani, na hatimaye kuwekwa katika kaburi. Siku ya tatu, wanawake wakilikaribia kaburi walikuwa pale ili kukamilisha matayarisho ya maziko kwa ajili ya mwili ule.

Lakini mwili ulikuwa umetoweka.

Ugunduzi wa kaburi tupu ulikuwa ndio mwanzo tu. Mariamu Magdalena, Mitume, na wengine wengi baadaye walishuhudia kitu cha kimiujiza: Yesu Kristo mfufuka, mkamilifu, katika umbo la kibinadamu lenye kugusika.

Mwokozi alihakikisha kwamba wale walio mshuhudia baada ya kufufuka kwake wali-elewa kikamilifu aina gani ya mwili alikuwa nao. Aliwaalika Mitume, kwa mfano, kuushika mwili Wake ili kwamba waweze

kujihakikishia wenyewe kwamba Yeye alikuwa na mwili halisi na sio roho (ona Luka 24:36–40).¹ Hata alikula pamoja nao (ona Luka 24:42–43).

Wakati Mitume wakiwa wanatimiza amri waliyopewa ya kuhubiri injili ya Yesu Kristo, walikabiliwa na upinzani na mateso, baadhi ya hayo yalikuja kwa sababu wao walifundisha kwamba Yesu Kristo alifufuka na kwamba binadamu wote wangepufuka kama matokeo ya hilo (ona Matendo 4:1–3).

Leo, Ufufuko wa Yesu Kristo ni kitovu cha ujumbe unaotangazwa kwa ulimwengu na Kanisa Lake kama ilivyokuwa wakati ule. Kama Nabii Joseph Smith Alivyosema: “Kanuni za msingi za dini yetu ni ushuhuda wa Mitume na Manabii, kuhusu Yesu Kristo, kwamba alikufa, akazikwa, na akafufuka tena siku ya tatu, na kupaa mbinguni; na mambo yote mengine ambayo yanahusiana na dini yetu ni viambatisho tu”²

Ufufuko unasaidia kujibu maswali ya msingi kuhusu asili ya Mungu, asili yetu na uhusiano wetu na Mungu, makusudi ya maisha

*Kupitia Ufufuko
Wake, Yesu Kristo
alitufundisha
kweli muhimu
kuhusu Mwili.*



“Yoyote ambaye anapuuza dhana ya Mungu mwenye mwili anapuuza vyote Kristo aliyekuwa na mwili wenye kufa na Kristo mfufuka.”
—Mzee Jeffrey R. Holland

haya, na matumaini tuliyo nayo katika Yesu Kristo. Hapa pana kweli chache zilizo sisitizwa na ufufuko wa Yesu Kristo.

Baba wa Mbinguni Ana Mwili Uliotukuka

Wazo la kwamba Mungu ana umbile la bina-damu kwa hakika limeota mizizi katika Biblia,³ vilevile katika fikra zinazopendwa, lakini desturi nyingi za kiteolojia na falsafa za kidini zime-ikataa na kupendelea Mungu “asiye na mwili, sehemu, au hisia kali,”⁴ tangu wakati ule, kwa mtazamo huu, mwili (na maada kwa kawaida) ni uovu au sio ya kweli, kwa maana hiyo roho, akili, au mawazo ni kitu chenye kweli ya msingi na hatima ya kuwa au ni kitu halisi.

Jinsi gani kupendeza kwa kawaida na kimapinduzi, ulikuwa, ufunuo huu wa asili ya Mungu kupitia Mwanawe, Yesu Kristo.

Wakati wa huduma yake, Mwokozi alisema, “Aliyeniona mimi amemwona Baba” (Yohana 14:9). Hii ilikuwa kweli zaidi baada ya Ufufuko Wake na mwili mkamilifu, mwili usiokufa, ambao ulionesha kwamba “Baba ana mwili wa nyama na mifupa unao shikika kama wa bina-damu; na Mwana pia” (M&M 130:22).

Asili ya mwili wa Baba wa Mbinguni ndivyo ilivyo funuliwa. Kama Joseph Smith alivyoeleza baadaye, “Kile ambacho hakina mwili au sehemu sio kitu. Hakuna Mungu mwingine ndani ya mbingu lakini Mungu yule aliye na nyama na mifupa.”⁵

Mzee Jeffrey R. Holland wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili ameiweka katika njia hii: “Kama kuwa na mwili sio tu hakuhitajiki lakini haipendezi kwa Mungu, kwa nini Mkombozi wa wanadamu aliukomboa mwili *Wake*, aki-ukomboa kutokana na kushikwa na mauti na kaburi, kuuhakikishia kamwe hautatengana tena na roho Yake kwa sasa au milele? *Yo yote ambaye ana puuza dhana ya Mungu mwenye mwili anapuuza vyote Kristo aliyekuwa na mwili wenye kufa na Kristo mfufuka.*”⁶

Baba wa Mbinguni ni mwenye Nguvu- Zote, Mjua -Yote, Upendo- Wote

Sifa bora kabisa za tabia ya Baba wa Mbinguni zimefunuliwa pia katika tendo halisi la ufufuko wa Yesu Kristo. Kama Mzee D. Todd Christofferson wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alivyosema, “Kutokana na ukweli wa Ufufuko wa Kristo, mashaka kuhusu kudura, kujua yote, na ukarimu wa Mungu Baba—aliyemtoa Mwanawe wa Pekee kwa ajili ya ukombozi wa ulimwengu—mashaka haya hayana msingi.”⁷

Uwezo, maarifa, na uzuri wa Mungu vime- thibitishwa kwa Ufufuko wa Yesu Kristo. ambao unatoa ushahidi wa hekima na upendo katika mpango wa Baba wa Mbinguni na uwezo wa (Mwanawe) wa kufanya hilo.

Sisi ni watoto wa Mungu

Kama Biblia inavyo tufundisha, tumeumbwa kwa mfano wa Mungu wanaume na wanawake: (Mwanzo 1:27) Ufufuko wa Yesu Kristo uliiongeza nguvu ukweli huu. Ukweli ni kwamba, katika saa ile ile ya Kufufuka kwa- ke, Yesu Kristo alisisitiza uhusiano wetu kwa Baba wa Mbinguni, akisema, “Napaa kwenda kwa Baba yangu, *naye ni Baba yenu*; na

kwa Mungu wangu, naye ni Mungu wenu”
(Yohana 20:17; mkazo umeongezwa)

Mwokozi alifunua kwamba Mungu na mwanadamu sio kabisa hawafanani kati yao katika kuwepo kwao kiasili. Umbile la msingi la miili yetu ni sawa na lile la roho zetu,⁸ na roho zetu ziliumbwa kwa mfano wa Mungu kwa sababu hiyo ndiyo asili ya uhusiano kati ya mzazi na mtoto.

Mwili ni kipawa cha Kuwezesha na cha Kuadilisha

Kupitia Ufufuko Wake, Mwokozi alituonesha sisi kwamba mwili, uliopo kwa kuunganishwa ni sehemu muhimu ya kuwepo kwa Mungu milele na watoto Wake. Kama Bwana alivyo mwonyesha Joseph Smith, Vitu vya asili ni vya milele, na roho na vitu vya asili, ambavyo vimeungana na haviwezi kutenganishwa, hupokea shangwe kamilifu (M&M 93:33). Huku kuunganishwa kusikoweza tenganihwa kunaunganishwa roho na maada za kimwili pamoja na hivyo vinakuwa kimoja kisicho kufa, kisicho haribika, kitukufu, na mwili kamili—aina pekee ya mwili wenye uwezo wa kupokea ukamilifu wa furaha ambao Mungu anao.

Kinyume na hayo, baada ya kuwa na maumbile ya kimwili na kisha kutenganishwa nayo na kuingia ulimwengu wa kiroho, wafu [wanaona] juu ya kutokuwepo kwa roho zao kutoka kwenye miili yao kama kifungo (M&M 138:50; ona pia M&M 45:17).

Hata miili yetu yenye kufa ni sehemu muhimu ya mpango wa Baba wa Mbinguni na sisi ni zawadi takatifu. Wakati roho zetu huko mbinguni zinapokuja katika dunia hii, “Zinaongezwa juu” (Abraham 3:26) ya mwili. Kama Nabii Joseph Smith alivyofundisha: “Tulikuja kwenye dunia hii ili tuweze kuwa na mwili na kuuwakilisha ukiwa msafi mbele ya Mungu katika Ufalme wa selestia. Kanuni kuu ya furaha inajumuisha kuwa na mwili. Ibilisi hana mwili, na hiyo ndiyo adhabu yake.”⁹

Kama Mzee David A. Bednar wa Akidi

ya Mitume Kumi na Wawili alivyo fundisha: “Miili yetu ya asili inawezesha kwa mapana, marefu, na wingi wa uzoefu ambao kiurahisi usingeweza kupatikana katika uwepo wetu kabla ya kuja hapa duniani. Hivyo, uhusiano wetu na watu wengine, uwezo wetu wa kugundua na kufanya kufuatana na ukweli, na uwezo wetu wa kutii kanuni na ibada za injili ya Yesu Kristo zinakuzwa kupitia maumbile ya kimwili. Katika shule ya mwili wenye kufa, tunapata uzoefu wa wema, upendo, upole, furaha, huzuni, masikitiko, maumivu, na hata changamoto za mapungufu ya kimwili katika njia ambazo zinatutayarisha kwa ajili ya maisha ya milele. Kiurahisi imesemwa, kuna masomo ambayo lazima tujifunze na uzoefu lazima tuwe nao, kama maandiko yanavyoeleza, ‘kulingana na mwili’ (1 Nefi 19:6; Alma 7:12–13).”¹⁰

Kwa nyongeza, kama Joseph Smith alivyofundisha, “Viumbe wote walio na mwili wana nguvu juu ya wale ambao hawana mwili.”¹¹ Shetani anaweza kutujaribu, lakini hawezi kutulazimisha. “Ibilisi hana nguvu juu yetu mpaka pale tunapomruhusu.”¹²

Hatimaye, zawadi ya mwili uliokamilihwa, uliofufuliwa inasaidia kutuweka

Mili yetu yenye kufa ni sehemu muhimu ya mpango wa Baba wa Mbinguni na ni zawadi takatifu. Wakati roho zetu zinapokuja katika dunia hii, “Zinaongezwa” (Abraham 3:26) na mwili.



mbali na nguvu za shetani milele. Kama pasingekuwa na Ufufuko, roho zetu lazima zingekuwa chini ya utawala wa ibilisi, zisingeinuka kamwe. Na roho zetu lazima zingekuwa kama yeye, na tuwe maibilisi, malaika kwa ibilisi, kutengwa na uwepo wa Mungu wetu, na kuishi na baba wa uwongo, katika huzuni, kama yeye mwenyewe” (2 Nefi 9:8–9).

Roho na Mwili Sio Maadui

Ingawa zipo tofauti, roho na mwili hazistahili kuwa vitu viwili kimsingi tofauti na zenye uhalisia usioweza kupatanishwa. Kama Joseph Smith alivyo jifunza, “Hakuna kitu kama kitu kisicho na umuhimu. Roho yote ni maada, lakini ni safi mno au halisi na inaweza tuu kutambulika kwa macho safi zaidi, hatuwezi kuiona; lakini wakati miili yetu itakapo kuwa imetakaswa tutaona kwamba yote ni maada” (M&M 131:7–8).

Katika hali Yake tukufu, na hali ya kufufuka, Yesu Kristo anawakilisha muungano mkamilifu wa roho na mwili akituonesha kwamba “Roho na mwili ni nafsi ya binadamu” (M&M 88:15). Katika maisha haya tunajitahidi kuwa “na mawazo ya kiroho” kuliko “mawazo ya kimwili” (2 Nefi 9:39), “[kuondoa] ubinadamu wa asili (Mosia 3:19), na “kuzuia tamaa [zetu] zote” (Alma 38:12). Lakini hiyo haimaanishi kwamba roho na mwili ni maadui. Kama Yesu Kristo alivyotunesha, mwili sio wa kudharauliwa na kufanywa uvuke mpaka lakini utawaliwe na kubadilishwa.

Maisha katika Mwili wenye Kufa una Makusudi ya Maana

Fikra kwamba maisha haya ni majaribio zinaleta maana zaidi tunapo fikiria nini tunajua kuhusu maisha yetu kabla



na baada ya hapa. Tuliishi kama roho kabla ya kuja duniani, na Baba wa Mbinguni ana kusudia tuwe kama Yeye na kuishi milele na maumbile ya kimwili yasiyo kufa. Kweli hizi zina maana kwamba muda wetu wa majaribio katika miili hii yenye kufa sio ya kiholela bali yana makusudi yenye maana ya kweli.

Kama Mzee Christofferson alivyoelezea: “Kwa chaguzi zetu tutaonesha kwa Mungu (na kwetu wenyewe) msimamo na uwezo wetu wa kuishi sheria yake ya kiselestia wakati tupo nje ya uwepo Wake na katika maumbile ya kimwili na nguvu zake zote, tamaa, na hamaki. Tungeweza kuuzuia mwili ili kwamba uwe kifaa kuliko kuwa mtawala wa roho? Tungeweza kuaminiwa kwa vyote katika muda huu na milele na nguvu za kimungu, ikijumuisha pamoja na uwezo wa kuumba uhai? Tungeweza sisi wenyewe mmoja mmoja kushinda uovu? Wale walioweza wangepata kuongezewa utukufu juu ya vichwa vyao kwa milele na milele’ [Ibrahimi 3:26]—kipengele chenye maana sana cha utukufu ule kuwa maumbile ya mwili uliofufuka, usio kufa, na mwili unaoshikika uliotukuka.”¹³

Uzoefu wetu katika miili yetu ya sasa, ukijumuisha mahusiano yetu sisi kwa sisi, yana maana kwa sababu yana fanana na yale ambayo yatakuja. Kama Joseph Smith alivyo jifunza, Kwamba uhusiano huu huu uliopo miongoni mwetu hapa utakuwepo miongoni mwetu kule, isipokuwa utazidishiwa utukufu wa milele, utukufu ambao sasa hatuufaidi (M&M 130:2).

Tunalo Tumaini katika Yesu Kristo

Tangu pale kaburi tupu lilipoonekana, Ufufuko wa Yesu Kristo umeleta matumaini kwa sababu tunatambua katika Ufufuko Wake ni mategemeo yetu wenyewe ambapo yote

Katika hali yake ya kufufuliwa, na kutukuka, Yesu Kristo anawakilisha muungano mkamilifu wa roho na mwili akituonesha kwamba “Roho na mwili ni nafsi ya binadamu” (M&M 88:15).



Tangu pale kaburi tupu lilipoonekana, Kufufuka kwa Yesu Kristo kumeleta matumaini kwa sababu tunatambua katika Kufufuka kwake ni mategemeo ya ufufuko wetu sisi wenyewe.”

[sisi] tuliyopoteza tutarejeshewa [sisi], ilimradi [sisi] tunae-ndelea kuwa waaminifu.¹⁴

Mitume wa awali wa Mwokozi waliweza kutoa ushahidi wa kijasiri wa Kufufuka Kwake kwa sababu waliuona na kuugusa mwili Wake. Lakini kulikuwa na mengi zaidi juu ya hilo kuliko hayo. Kama vile Yesu Kristo alivyokuwa ameponya udhaifu wa kimwili ili kuonesha kwamba alikuwa na uwezo wa kusamehe dhambi (ona Luka 5:23–25). Kufufuka Kwake—ushahidi wa kushikika wa uwezo Wake wa kushinda mauti ya kimwili—ukawa uhakikisho kwa wafuasi Wake juu ya nguvu Zake za kushinda mauti ya kiroho. Ahadi ambazo Yeye alizitoa katika mafundisho Yake—msamaha wa dhambi, amani katika maisha haya, uzima wa milele katika ufalme wa Baba—zikawa thabiti na imani yao haikuyumba.

“Kama Kristo hakufufuka, imani [yetu] ni bure” (1 Wakorintho 15:17). Lakini kwa sababu Yeye *ali* inuka

kutoka kwa wafu, tunaweza “kuwa na tumaini kupitia upatanisho wa Kristo na uwezo wa kufufuka kwake, kuinuliwa kwenye uzima wa milele, na hii kwa sababu ya imani [yetu] kwake kulingana na ile ahadi (Moroni 7:41).

Wakati wa maisha Yake katika mwili wenye kufa, Yesu Kristo aliwaalika watu wamfuate Yeye. Baada ya Kifo Chake na Kufufuka, makusudio yakawa wazi zaidi. Kama sisi, kwa utiifu wa sheria na ibada za injili, tukakuza roho ya kiselestia ndani yetu, tunaweza kupokea mwili huo huo ambao ulikuwa mwili wa asili na {ukahuishwa kwa sehemu ya utukufu wa selestia [na] kisha kupokea huo huo hata utimilifu (M&M 88:28–29). Yeye ameonesha njia. Yeye ni njia. Ni kwa uwezo Wake—kupitia Upatanisho na Kufufuka- Kwake—kwamba ukamilifu huu wa selestia unawezekana, ambao unajumuisha ukamilifu wa furaha katika mwili uliofufuka. ■

MUHTASARI

1. Wakati Yesu Kristo alipowatokea watu katika Ulimwengu Mpya, Aliwaomba—maelefu yao—kumwendea, “mmoja mmoja,” na kugusa mikono Yake, miguu na ubavu wake ili kwamba waweze kushuhudia kwamba waliweza kugusa na kumwona Bwana mfufuka (ona 3 Nefi 11:14–15; 18:25).
2. *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* (2007), 49.
3. Ona Mwanzo 1:27; Kutoka 33:11; Matendo 7:56.

4. Ingawa mawazo kama haya yalikuwepo katika imani za mwanzo za Kikristo, maelezo haya pekee yanakuja kutoka Makala thelathini na tisa za Kanisa la Angalikana (1563).
5. *Teachings: Joseph Smith*, 42.
6. Jeffrey R. Holland, “The Only True God and Jesus Christ Whom He Hath Sent,” *Liahona*, Nov. 2007, 42.
7. D. Todd Christofferson, “The Resurrection of Jesus Christ,” *Liahona*, Mei 2014, 113.
8. Hata ufunuo wa Yesu Kristo kabla ya kuja

- duniani ulikuwa ni ushuhuda wa ukweli huu, kwa vile ulionesha kwamba mwili wa roho Yake ulikuwa wa kibinadamu kimaumbile (ona Etheri 3:16).
9. *Teachings: Joseph Smith*, 211.
 10. David A. Bednar, “We Believe in Being Chaste,” *Liahona*, Mei 2013, 41.
 11. *Teachings: Joseph Smith*, 211.
 12. *Teachings: Joseph Smith* 214.
 13. D. Todd Christofferson, “Why Marriage, Why Family,” *Liahona*, Mei 2015, 51.
 14. *Teachings: Joseph Smith*, 51.

Njoo, Njoo Kwake

Ya Dhati ♩ = 44-48

Maneno na Steven K. Jones
Muziki na Michael F. Moody

mp

KULIA

1. Ali -
(2. Kaj) -
(3. Ali) -

5

kuja kw - etu, ali - tupe - nd - a sana Hakun - a na - f - si asiyo - we
a duni - ani ka - ma mwan - a - d - amu. Ha - ku - na hi - ta - ji asi -
pi - tia huz - uni ka - ma si - si; Kw - a wa - ami - ni - o Hu -

8

za gu - s - a; Ma - isha ya giza, as - iyo a - ngaza. Hu -
lo - li - ele - wa, Wa - la m - au - mivu as - iyo - ya - jua; Si
to - a m - sa - ada Hu - fun - gua ma - cho, Hu - was - a - mehe Wa - nyen -

rall.

11

a tempo

zun - i maj - on - zi as - iyo - o - ndo - a. Njoo, njoo Kw - a -
nja - a, m - aumivu, ha - we - zi - po - nya Njoo, njoo Kw - a -
yeke - vu wa - amini - fu, wamfu - a - ta - o Njoo, njoo Kw - a -

2



14

ke. _____
ke _____ Njoo Kw - ake jifu - nze kwa - ke. _____ Mpole
ke _____

17

mnye - nyek - evu mw - eny - e hu - ruma Njoo, njoo Kw - a -

20

ke _____

1, 2. _____ 3. _____

2. Kaj - _____ Ee,
3. Ali - _____

23

rall.

njoo, njoo Kw - a - ke _____

© 2016 na Steven K. Jones na Michael F. Moody. Haki zote zimehifadhiwa
Wimbo huu unaweza kunakiliwa kwa ajili ya mahitaji, yasiyo ya kibiashara ya matumizi kanisani ama nyumbani.



DARAJA LA KWENDA
KWENYE

Matumaini NA Uponyaji

*Kwa usaidizi unaofaa,
waathiriwa wa
unyanyasaji wa
kijinsia wanaweza
kupata uponyaji
wanaotamani
kwa dhati.*

Na Nanon Talley

LDS Family Services, Texas, Marekani

Hebu fikiria unasimama kwenye ukingo wa korongo na unataka kuvuka kwenda upande ule mwingine wa korongo kuu, ulikoelezwa kwamba kuna furaha kubwa inayokusubiri. Wakati unatafuta njia ya kuvuka, unaona rundo la vifaa ambavyo, ikiwa vitawekwa pamoja kwa njia inayofaa, vitajenga daraja la kuvuka korongo hilo.

Ikiwa haujui jinsi ya kujenga daraja, vifaa vile vitakuwa havina maana kwako kabisa nawe utajiona unachanganyikiwa na kukata tamaa. Lakini ikiwa utapata usaidizi kutoka kwa mtu aliye na uzoefu katika kujenga madaraja, ufahamu wako na kuelewa kwako kwaweza ongezeka na kwa pamoja kazi hiyo inaweza kukamilika.

Kwa muda wa miaka 18 iliyopita, kazi yangu imekuwa kutoa vifaa na mwongozo ili kuwasaidia watu kuvuka ghuba la mateso ya kihisia na kiakili. Kati ya wale watu wote ambao nimekwisha kuwashauri, hakuna wateja wengine ambao huja wakiwa wamejeruhiwa sana kama wale ambao wamekuwa waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia. Nimeona athari ambayo changamoto hii inayo juu ya uwezo wa mtu huyo katika kuvumilia hadi mwisho.

Hata hivyo, nimekuja pia kujua ya kwamba msaada wa kudumu kutokana na mapambano na mateso yetu inawezekana kupitia kwa Mwokozi wetu. Upendo wake unawainua watu kutoka gizani na kuwaingiza katika nuru.

Ni Kwa nini Unyanyasaji wa Kijinsia Unasababisha Madhara Kama Haya?

Waathirika wa unyanyasaji hunielezea kuhusu maisha yaliyojawa na msongo wa mawazo, kutojamini, na uchungu mwingine mkubwa wa kihisia. Rais Gordon B. Hinckley (1910–2008) alitusaidia kuelewa ni kwa nini unyanyasaji wa kijinsia husababisha maumivu makubwa hivi:

“Kuna tabia ya kutisha, na kutatanisha ya unyanyasaji wa kijinsia. Ni zaidi ya uwezo wa kuelewa. Ni fedheha kwa heshima ambayo inastahili kuwepo ndani ya kila mwanauume na mwanamke. Ni *ukiukaji wa sheria ya kile kilicho kita-katifu na cha kiungu*. Ni uharibifu katika maisha ya watoto. Ni ya kukemewa na *yenye kustahili kulaaniwa vikali kabisa*.

“Aibu kwa mwanaume au mwanamke yeyote anayemnyanyasa mtoto kijinsia. Kwa kufanya hivyo, mnyanyasaji *hajeruhi tu katika njia mbaya zaidi*. Yeye pia huwa na hatia mbele ya Bwana.”¹

Uwezo wa kuumba maisha ni uwezo uliotukuka na ambao Mungu amewapa watoto Wake. Mzee David A. Bednar wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alifundisha: Uwezo wa kuumba maisha ni muhimu kiroho. Baba yetu wa Mbinguni na Mwanawe Mpendwa ni waumbaji na

wamemkabidhi kila mmoja wetu sehemu ya uwezo Wao wa kuumba.² Si ajabu, hasa, kwamba kukiukwa kwa uwezo huu mtukufu kunastahili kushutumiwa vikali sana” na kunasababisha “majeraha makali zaidi ya aina hiyo i.”

Kuelewa Majeraha

Unyanyasaji wa kijinsia ni uhusiano bila idhini unaoshirikisha tabia za kugusa au tabia zisizo za kugusa ambapo mtu anatumika kwa kumridhisha mwingine kijinsia. Mara nyingi sana, waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia huachwa na fikra za kuchanganyikiwa vile vile na hisia za kutokuwa wenye kustahili na aibu ambayo inaweza kufikia kuwa nzito zaidi kuvumilika. Uchungu na mateso ambayo waathiriwa hupitia mara nyingi huzidishwa na maoni ya watu wengine yanayotokana na kutoelewa unyanyasaji wa kijinsia na athari zake. Waathiriwa wengine hutuhumiwa kuwa wanadanganya au wanaambiwa kuwa unyanyasaji huo ulikuwa ni makosa yao wenyewe. Wengine kimakosa wanaongozwa kuamini ya kwamba ni lazima watubu, kama kwamba kwa njia fulani walikuwa wametenda dhambi kwa kuwa waathirika.

Wateja wengi ambao nimefanya kazi nao ambao walinyanyaswa kijinsia utotoni au ujanani mwao huambiwa “waachane na hayo,” au “samehe tu na usahau.” Matamshi ya aina hii—hasa wakati yanapotoka kwa marafiki wa karibu, wana familia, au viongozi wa Kanisa—yanaweza kumfanya mwathirika kuwa msiri zaidi na kuaibika badala ya kupona na kuwa na amani. Sawa tu na jeraha kubwa la kimwili au maambukizi, majeraha haya ya kihisia hayapotei tu kwa kuyapuza. Bali, kuchanganyikiwa kunakoanza wakati wa unyanyasaji kunazidi kuongezeka, na pamoja na hisia za uchungu zinazo fuaatia, fikra za mtu zaweza kubadilika, hatimaye kusababisha kuwepo kwa tabia zisizo bora. Sio ajabu kwa waathirika wa unyanyasaji kutojua kwamba kilicho watokea ilikuwa ni unyanyasaji, na wana-weza kuwa na tabia zisizo nzuri na hisia chungu.

Hannah (jina limebadilishwa) alinyanyaswa kijinsia mapema utotoni mwake. Kama waathiriwa wengine, alikua akijihisi kwamba alikuwa mtu mbaya asiye na thamani. Alitumia sehemu kubwa ya maisha yake akijaribu kuwahudumia wengine kiasi cha kufidia hisia zake za kutokuwa “mzuri vya kutosha” kwa Baba wa Mbinguni au mtu mwingine ye yote kumpenda. Katika uhusiano wake,



aliogopa kwamba ikiwa mtu yeyote angejua kabisa ukweli juu yake, wangepikiria kuwa yeye ni mbaya kama vile yeye mwenyewe alivyoamini. Alihisi hofu kubwa sana ya kukataliwa ambayo ilimsababisha kuwa na uoga kujaribu mambo mapya maishani au kufanya majukumu madogo kama kumpigia mtu simu.

Alikuwa amebarikiwa kwa kipaji cha sanaa lakini akakata tamaa kwa kuogopa kwamba hangeweza kustahimili kukosolewa.

Kwa zaidi ya miaka 50 hisia zake za unyonge, udhaifu, hofu, hasira, kuchanganyikiwa, aibu, upweke, na kujitenga ziliongoza maamuzi yake ya kila siku.

Kubadilisha Uchungu kuwa Amani

Mwokozi aliteseka maumivu na mateso na majaribu ya kila aina. Alifanya hivi ili kwamba Yeye “ajue kulingana na mwili jinsi ya kuwasaidia watu wake” (Alma 7:11–12). Mateso yake hayakuwa tu kwa ajili ya dhambi zetu lakini pia kwa ajili ya uponyaji wakati dhambi za mwingine zinapo sababisha kuteseka kwetu.

Ikiwa Yeye angekuwa hapa leo hii, ninafikiri Mwokozi angelia na kuwabariki wale walionyanyaswa kijinsia, kama vile alivyolia na kuwabariki Wanefi (ona 3 Nefi 17). Wakati Yeye hayuko hapa kimwili, Roho Wake anaweza kuwa nasi, na ametuandalia njia ya kupona, kujisikia amani, na kusamehe.

Kwa wengi ambao wameumizwa, dhana ya kuwa uchungu walio nao unaweza kubadilishwa na kuwa na



amani ni kana kwamba haiwezekani kuaminika. Mara nyingi vidonda vya walionyanyaswa huwa havionekani na havitambuliwi na wengine kwa miaka mingi. Majeraha yanafunikwa na nyuso zenye tabasamu, utayari wao wa kuwasaidia wengine, na kuishi maisha kana kwamba hakuna chochote kibaya kilichofanyika, lakini bado uchungu ungalipo.

Wacha tulinganishe mchakato wa uponyaji wa kihisia na kuhudumia na kutibu jeraha la kimwili. Tuseme kwa mfano wakati ulipokuwa mchanga, ulivunjika mguu wako. Badala ya kwenda kwa daktari kupata matibabu, ulichechemea hadi uchungu huo mkubwa ulipo potea, lakini siku zote kuna uchungu kidogo kwa kila hatua unayochukua. Miaka kadhaa baadaye unahitaji uchungu huo uondoke kabisa, kwa hivyo unaenda kumwona daktari. Ni lazima daktari aupange upya mfupa, asafishe sehemu yoyote iliyokuwa imekua vibaya, aikate, na akupeleke kwa tabibu wa viungo vya mwili ili kuimarisha mguu wako.

Mchakato wa kupona kutokana na unyanyasaji ni sawa sawa na huu kwa vile muathirika ni lazima kwanza atambue kwamba uchungu ni wa kweli

TABIA ZA KAWAIDA ZA WAATHIRIWA

Waathirika mara nyingi hupata taabu katika kuwa na uhusiano na yawezekana mara kwa mara kutafuta kukubalika mbele ya wengine, hukosa kuonyesha hisia, hujiwekea viziwi ili kuwazuia watu kuwa karibu nao ili wasije wakaumizwa, kuwa wazinzi kwa ajili ya kujipatia utunzaji kupitia vitendo vya kimapenzi (ikiwa ni pamoja na ponografia na kujisisimua wenyewe), au kufanya kinyume kabisa na kuepuka cho chote kinachohusiana na ngono. Aibu inayohusiana na tabia hizi mara nyingi huzuia watu wasitafute usaidizi kutoka kwa wazazi, viongozi wa ukhuni, au wataalamu kwa sababu hawaelewi uhusiano baina ya kile kilichowatokea na tabia zao.

Katika kuishi injili, waathirika huonekana kuegemea upande mmoja uliokithiri au huo mwingine: Wengine huwa watu wa dini kupindukia. Katika jaribio la kufunika kile wanachokiona kama kutostahiki kwao, wao hujaribu kufanya kila kitu inavyopaswa. Wengine hujihisi kwamba kamwe hawatakuja kuwa wenye kustahili uzima wa milele na mara nyingine hao hukata tamaa.

MASOMO KUTOKA MAFUNDISHO NA MAAGANO 123

Wakati Nabii Joseph Smith alipokuwa amefungwa gerezeni kule Liberty, Missouri, alilia-ndikia Kanisa waraka, ndani yake ni sehemu za 121–124 za Mafundisho na Maagano, ambayo inajumuisha “wajibu wa Watakatifu juu ya watesaji wao” (M&M 123, utangulizi). Hakuwaambia Watakatifu waliokuwa wamepitia mateso na majeraha ya kimwili kusalia na maumivu yao wenyewe na kujifanya kama hakuna kilichokuwa kimetendeka. Zingatia jinsi ushauri uliotolewa katika sehemu ya 123 unavyoweza kutumika katika matatizo ya unyanyasaji.



na kwamba kuna jambo linaloweza kufanyi-ka juu ya uchungu huo. Mchakato unajumu-isha kukiri kile kilichofanyika na kuruhusu hisia za kujeruhiwa, hofu, na huzuni lazima uzisikie, zitambuliwe, na kuthibitishwa. Mara nyingi inasaidia kufanya kazi na mtaalamu mwenye uzoefu katika mchakato huu wa uponyaji. (Mwulize kiongozi wako wa ukuhani ikiwa LDS Family Services inapatikana katika eneo lako.)

Muathirika awe au asiwe na uwezo wa kupata usaidizi wa mtalaamu, ni vyema kuomba, soma kuhusu maisha ya Mwokozi na Upatanisho Wake, na kuonana mara kwa mara na kiongozi wako wa ukuhani. Anaweza kusaidia kupunguza mizigo na kupokea maongozi ya kumsaidia mwa-thirika kuelewa thamani yake tukufu na uhusiano wake na Baba wa Mbinguni na Mwokozi. Dada Carole M. Stephens, Mshauri wa Kwanza katika Urais Mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Wakina Mama hivi karibunu alifundisha “Uponyaji waweza kuwa mchakato mrefu. Itakuhitaji kwa maombi utafute mwongozo na usaidizi unaofaa, ikiwa ni pamoja na kushauriwa na wenye ukuhani waliotawazwa ipasavyo. Unapojifunza kuwasiliana wazi wazi, weka mipaka inayofaa na pengine tafuta ushauri

nasaha. Kudumisha afya ya kiroho katika mchakato huo wote ni muhimu!”³

Kwa Hannah, maisha yake yalikuwa yamekosa faraja kiasi cha kwamba alitafuta usaidizi. Alijua kutokana na ushuhuda wake ya kwamba angeweza kujisikia amani na kuridhika maishani mwake lakini hakuji-sikia hivyo katika hali endelevu. Kupitia maombi na kuzungumza na askofu wake, alielekezwa kupata ushauri nasaha, ambapo aliweza kupata vifaa alivyohitaji ili kutoa ukweli kutoka gizani na kushirikiana na mnasihi mzigo mbaya aliokuwa akibeba pekee yake. Katika kufanya hivyo, aliweza kuachilia uchungu na kupata amani iliyo ahidiwa na Mwokozi (ona Yohana 14:27). Pamoja na amani hii na faraja kulikuja hamu na uwezo wa kusamehe.

Haja ya Kusamehe

Dhana ya kusamehe mara nyingi huwa ngumu kwa waathirika wa unyanyasaji kusikia na mara nyingi huwa inaeleweka vibaya. Ikiwa watafikiria kwamba kusamehe ni kama kumwachilia mkosaji aende zake au kusema ya kwamba kile walichokifanya kwa sasa si tatizo tena, muathirika atajiona hatambuliki. Huku tukiwa tumeamriwa kusa-mehe (ona M&M 64:10), katika hali ambazo

majeraha ni makubwa, uponyaji kawaida lazima uanze kabla ya muathirika hajaweza kumsamehe mnyanyasaji kikamilifu.

Wale ambao wanateseka kwa uchungu ulio sababishwa na unyanyasaji wanaweza kupata faraja katika ushauri huu kutoka Kitabu cha Mormoni: “Mimi, Yakobo, nitawazungumzia wale walio safi moyoni. Mtegemeeni Mungu kwa mawazo yaliyo imara, na mwombeni kwa imani kubwa, na Yeye atawafariji katika mateso yenu, na atatetea teto zenu, na kuwateremshia hukumu wale wanaotaka kuwaangamiza” (Yakobo 3:1). Haja ya haki na haki ya kurejeshewa vyaweza kuachwa kwa Bwana ili Yeye aweze kubadilisha majeraha yetu kuwa amani.

Hannah hatimaye aligundua ya kwamba angeweza kumwachia Mwokozi kutaka kwake haki na kama malipo angepata hisia ya amani maishani mwake kwa jinsi ambavyo hajawahi kujisikia hivyo hapo awali. Mwanzoni alikuwa anaogopa kuhudhuria mikutano ya familia ambapo alijua mnyanyasaji wake angekuwepo. Sasa, kwa sababu ya kuwa kwake tayari kukabiliana na majeraha magumu ya kihisia akiwa njiani kuelekea uponyaji, sasa hana hofu tena ya kuwa katika uwepo wake na anaweza hata kumhurumia yeye katika umri wake wa zee.

Huru kutokana na Mizigo Isiyohitajika

Mzee Richard G. Scott (1928–2015) wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alisema ya kwamba “uponyaji kamili utakuja kupitia imani yako katika Yesu

Kristo na nguvu Zake na uwezo Wake, kupitia Upatanisho Wake, kuponya makovu ya kile kisicho cha haki na kisichostahili. . . .

“Anakupenda. Alitoa uhai Wake ili uwe huru na mizigo isiyohitajika. Yeye atakusaidia kufanya hivyo. Ninajua kwamba anao uwezo wa kukuponya.”⁴

Adui anataka kuwashikilia watu wakiwa wamefungwa kwa uchungu na mateso kwa sababu yeye ni mwenye huzunii (ona 2 Nefi 2:27). Kwa usaidizi wa Mwokozi, Yesu Kristo, uchungu waweza hakika kubadilishwa na kuwa amani, kama vile tu Mwokozi anavyoweza kutoa, nasi tunaweza kuishi kwa shangwe. “Adamu alianguka ili wanadamu wawe; na wanadamu wapo, ili wapate shangwe” (2 Nefi 2:25). Kuishi kwa shangwe kutatuwezesha nyakati za majaribu kuvumilia zaidi na kutuwezesha kujifunza na kukua na kuzidi kuwa kama Baba wa Mbinguni.

Nimenyenyekezwa na baraka niliyokuwa nayo maishani mwangu kuketi na wale wote waliojeruhiwa na unyanyasaji na kuona muujiza wa uponyaji unaokuja tu kupitia kwa Mwokozi. Ikiwa unateseka, tafadhali kwa maombi geuka upate usaidizi. Hauhitaji kubeba mzigo huo mzito pekee yako. Ninajua Yeye huponya, kwani nimeshuhudia haya mara nyingi sana. ■

MUHTASARI

1. Gordon B. Hinckley, “Save the Children,” *Ensign*, Nov. 1994, 54; emphasis added.
2. David A. Bednar, “We Believe in Being Chaste,” *Liahona*, Mei 2013, 42.
3. Carole M. Stephens, “The Master Healer,” *Liahona*, Nov. 2016, 11.
4. Richard G. Scott, “To Be Free of Heavy Burdens,” *Liahona*, Nov. 2002, 88.

USHAURI KWA VIONGOZI, FAMILIA, NA MARAFIKI

Wakati ambapo muathirika anakuamini kiasi cha kushirikiana nawe mateso yao na kunyanyaswa kwao, mazungumzo nao yanapaswa kuanza kwa upendo na huruma. Mara nyingi sana waathirika wameshirikiana nami ya kwamba wakati walipomwendea askofu wao wapate usaidizi, lengo la kwanza lilikuwa ni kuhitajika kwao wao kumsamehe aliye wakosea. Hili laweza kumua cha muathirika ahisi ya kwamba cha muhimu zaidi ni mkosaji. Kama hili likitokea, mara chache watu hao hurudi kwa maaskofu wao wapate usaidizi na wanakosa uponyaji wa kiroho ambao unawezekana kwa upendo na msaada wa kikanisa.

Kusamehe ni sehemu muhimu katika mchakato wa uponyaji na ni amri—lakini tafadhali amini ya kwamba kumruhusu mtu kukiri mateso yao, kuhisi hisia zao, na kuzungumza kuhusu hayo pamoja na mtu anayemwamini kwa wakati wake kutasababisha uponyaji unaokuja kutokana na kuwa na uwezo wa kumsamehe mnyanyasaji.

Viongozi wa kanisa wanaweza kurejea ministering.lds.org ili kupata “Abuse: Help for the Victim” kwa taarifa zaidi.

Albamu ya Zamani ya Familia:

Nguvu ya Hadithi za Kifamilia

Urithi wa mababu zangu unaendelea kuishi kupitia mimi, daima ukishawishi maisha yangu kuwa bora.

Na Amneris Puscasu

Asubuhi moja wakati wa kiangazi kabla ya Vita vya Pili vya Dunia, baba wa babu yangu aliamka kama afanyavyo siku zote—kabla ya jua kuchomoza. Alitoka nje ya nyumba yake kwenye kilima kilichokuwa juu ya bonde la kijani kibichi la kijiji chake kule Romania, na akaketi kwenye nyasi zilizo funikwa na umande wa asubuhi mapema, akiwa amezama katika mawazo yake—mawazo yale yale ambayo yalikuwa akilini mwake kwa muda sasa. Mwanaume aliyeelimika mwenye moyo mkarimu na akili dadisi, alipendwa na kuheshimiwa na kila mtu katika kijiji.

Baada ya jua kuchomoza, alienda nyumbani na kukiri kwa mkewe kwamba amekuwa na hamu ya kutaka kujua mazishi yake yangekuwa ya aina gani, na alitaka kufanya mazoezi ya mavazi yake ya mazishi. Alipanga tarehe, akannua jenzea, akakodisha kuhani na waombolezaji wenye taaluma, na akapata vifaa vingine vyote vinavyohitajika katika tamaduni Halisi ya Kiothodoksi ya Kigiriki. Kisha siku ya mazishi ya kuigiza ikafika. Meza ziliandaliwa kati kati ya kijiji kwa ajili ya karamu ya makumbusho, familia yote ilikuwa imevalia nguo nyeusi, kuhani akaja, baba wa babu yangu akajilaza ndani ya jenzea, akigeuza mto ili aweze kuonekana vizuri, na kisha maandamano ya mazishi yakaanza. Wakati sherehe ilipokamilika, kijiji kizima kilialikwa kwenye karamu, na baba wa babu yangu alitimiza ndoto yake ya kucheza ngoma katika mazishi yake. Aliishi miaka mingine 20, mara kwa mara akichunguza kuona ikiwa jenzea lake bado lilimtosha.

Siyo tu Majina na Tarehe

Sijawahi kukutana na baba wa babu yangu, lakini simulizi yake siku zote imekuwa yenye kunipendeza zaidi ambayo niliambiwa na babu na bibi yangu. Kila siku babu na bibi zangu wangetuelea ndugu zangu na mimi simulizi kuhusu mababu zetu wa kale: kule walikotoka, jinsi walivyokuwa, maadili yao, ndoto na matumaini. Baada ya mlo wa kila Jumapili, babu na bibi yangu wangechukuwa



albamu ya familia, na kwa kufungua kila ukurasa, simulizi zilitolewa na mioyo iliunganishwa pamoja katika pambo la upendo kwa muda wa vizazi sita. Hazikuwa tu ni picha kuu kuu zilizokuwa zimeandikwa majina na tarehe upande wa nyuma. Nyuma ya kila sura kulikuwa na baba au mama, mwana au binti, ndugu au dada, na hivyo basi ukawa urithi wao, ikiwa ni pamoja na tamaduni nyingine za familia, nilizorithishwa.

Nguvu Katika Nyakati za Majaribu

Wakati nilipokuwa nafika umri wa miaka 19, wazazi wangu na wengi kati ya wana familia wangu wa karibu walikuwa wameaga dunia na mali nyingi niliyokuwa nimerithi ilipotea au kuibiwa. Na bado kuna kitu kimoja ambacho muda, majanga ya asili, au hata kifo hakiwezi kuharibu: daraja linalounganisha siku zilizopita, wakati wa sasa, na siku zijazo ambazo kila mmoja wa wana familia wangu walijenga. Kwa sababu ya bidii yao, nyuzi zinazounganisha mioyo ya familia yangu pamoja imenipa nguvu ya kushinda hali ngumu.

Wakati wazazi wangu na babu na bibi zangu walpoikufa, nilihisi huzuni kubwa sana kiasi cha kwamba niliwaza kama nitakuwa na nguvu za kutosha kuendelea kuishi. Nilibarikiwa kuhisi ushawishi wao kutoka upande huo mwingine wa pazia, na hiyo ilinisaidia kupata ushuhuda wa nguvu kuhusu mpango wa wokovu, kuhusu maisha baada

ya kifo, na kisha baadaye, kuhusu ibada za hekaluni ambazo ni muhimu sana kwa ajili ya wokovu wetu. Kamwe sikuwahi kukutana na mababu zangu wakuu au wengi wa mashangazi na wajomba zangu, lakini kila wakati ninapoichukuwa albamu kongwe ya familia iliyo na picha zao, ninajiona mimi mwenyewe machoni mwao. Niko jinsi nilivyo kwa ajili ya wale walionitangulia. Uzoefu wao na hekima yao vimesaidia kujenga tabia yangu na kuniongoza maishani.

Mojawapo ya zawadi kubwa ambayo familia yangu ilinipa tangu mapema utotoni ni ufahamu wa historia ya familia yangu na imani ya kwamba mimi ni kiungo baina ya siku zilizopita na siku zijazo. Pia ninajua ya kwamba nilikuja duniani kuishi maisha yangu—kuchunguza na kujifunza na kuyathamini. Ni ufahamu huu wa historia ya familia yangu ambao unanisaidia kupitia majaribu yote ya maisha.

Mimi hufikiria mara kwa mara kuhusu familia yangu iliyo upande mwingine wa pazia na dhabihu ambazo walifanya kwa niaba yangu ili niweze kuwa na maisha bora. Ninafikiria kuhusu ibada za hekaluni ambazo zinatuwezesha kuwa pamoja tena kama familia siku moja. Na ninafikiria kuhusu Upatanisho wa Mwokozi wangu, aliyefanya kuwezekana kwa haya yote. Alilipa fidia ili tuweze kuishi. Kwa sababu hii tunampenda na kumwabudu Yeye kwa shukrani leo na milele. ■

Mwandishi anaishi New York, Marekani.





**Na Mzee Larry R.
Lawrence**
Wa Sabini



Vita Vinaendelea

Vita ambavyo vilianza mbinguni bado vinaendelea hadi siku hii ya leo. Kwa kweli, vita vinakuwa vikali kadiri Watakatifu wanapojitayarisha kwa ajili ya kurudi kwa Mwokozi.

Mtu yeyote anayefuata habari za kimataifa atakubali ya kwamba tunaishi katika nyakati za “vita na minong’ono ya vita” (M&M 45:26). Kwa bahati nzuri, kila mtu duniani ni mkongwe wa vita. Tumekuwa tukipigana na majeshi ya uovu katika vita vinavyoendelea ambavyo vilianza katika ulimwengu wa kabla ya kuzaliwa duniani.

Kwa sababu hatukuwa tumepokea miili, tulipigana Vita hivyo vya Mbinguni bila sime, au bunduki, au mabomu. Lakini mapigano hayo yalikuwa makali tu kama vita vya kisasa, na kulikuwa na mabilioni ya majeruhi.

Vita vya kabla ya kuzaliwa vilipiganwa kwa maneno, mawazo, mijadala, na ushawishi (ona Ufunuo 12:7–9, 11). Mbinu ya Shetani ilikuwa ni kuwatisha watu. Alijua kwamba hofu ni mbinu bora ya kuharibu imani. Anaweza kuwa alitumia hoja kama hizi: “Ni ngumu sana.” “Haiwezekani kurudi ukiwa msafi.” “Kuna hatari kubwa sana.” “Unajuaje kama unaweza kumwamini Yesu Kristo?” Alimwonea wivu sana Mwokozi.

Kwa shukrani, Mpango wa Mungu uliushinda uongo wa Shetani. Mpango wa Mungu ulishirikisha haki ya maadili ya kujiamulia kwa ajili ya binadamu na dhabihu kuu. Jehova, anajulikana kwetu kama Yesu Kristo, alijitolea kuwa dhabihu hiyo—ili ateseke kwa ajili ya dhambi zetu. Alikuwa radhi kufa kwa niaba ya kaka zake na dada zake ili wale ambao wangetubu wangerudi wakiwa wasafi na hatimaye kuwa kama Baba yao wa Mbinguni. (Ona Musa 4:1–4; Ibrahimu 3:27.)

Faida nyingine ambayo ilimsaidia Jehova kushinda mioyo ya watoto wa Mungu ni ushuhuda wa nguvu uliotolewa na wafuasi Wake, wakiongozwa na Mikaeli, malaika mkuu (ona Ufunuo 12:7, 11; M&M 107:54). Katika maisha ya kabla ya kuja duniani, Adamu aliitwa Mikaeli, na Shetani aliitwa Lusiferi, linalomaanisha “mbeba nuru.”¹

Katika Vita vya Mbinguni, tulimpenda na kumuunga mkono Baba wa Mbinguni. Tulitaka kuwa kama Yeye.

Hilo laweza kuonekana kama jina la ajabu kwa mfalme wa giza (ona Musa 7:26), lakini maandiko yanafundisha ya kwamba Shetani alikuwa “malaika wa Mungu aliyekuwa mwenye mamlaka katika uwepo wa Mungu” kabla ya kuanguka (ona M&M 76:25–28).

Ni namna gani roho mwenye elimu na uzoefu mwingi angeanguka mbali hivyo? Ilikuwa kwa sababu ya kiburi chake. Lusiferi aliasi dhidi ya Baba yetu wa Mbinguni kwa sababu aliutaka ufalme wa Mungu uwe wake.

Katika hotuba yake maarufu “Jihadhari na Kiburi,” Rais Ezra Taft Benson (1899–1994) alifundisha ya kwamba Lusiferi “alitaka kuheshimiwa zaidi ya wengine wote” na hiyo “hamu ya kiburi chake ilikuwa ni kumpindua Mungu.”² Umesikia pia kwamba Shetani alitaka kuharibu haki ya mwanaadamu ya kujiamulia, lakini hiyo sio sababu pekee iliyomfanya aanguke kutoka kwenye neema ya Mungu. Alifukuzwa kutoka mbinguni kwa sababu ya uasi dhidi ya Baba na Mwana (ona M&M 76:25; Musa 4:3).

Ni kwa nini wewe na mimi tulipigana dhidi ya ibilisi? Tulipigana kutokana na utiifu. Tulimpenda na kumuunga mkono Baba yetu aliye Mbinguni.

Tulitaka kuwa kama Yeye. Lusiferi alikuwa na lengo tofauti. Alitaka kuchukua nafasi ya Baba (ona Isaya 14:12–14; 2 Nefi 24:12–14). Hebu fikiria jinsi usaliti wa Shetani ulivyowaumiza Wazazi wetu wa Mbinguni. Katika maandiko, tunasoma ya kwamba, “mbingu zililia juu yake” (M&M 76:26).

Baada ya kampeni kali, Mikaeli na majeshi yake walishinda. Theluthi mbili ya majeshi ya mbinguni walichagua kumfuata Baba (ona M&M 29:36). Shetani na wafuasi wake walifukuzwa kutoka mbinguni, lakini hawakupelekwa mara moja nje gizani. Kwanza, walitumwa



hapa duniani (ona ufunuo 12:7–9), ambapo Yesu Kristo angezaliwa na ambapo dhabihu yake ya upatanisho ingetendeka.

Ni kwa nini majeshi ya Shetani yaliruhusiwa kuja duniani? Walikuja kutoa upinzani kwa wale waliokuwa wakijaribiwa hapa (ona 2 Nefi 2:11). Je hatimaye watatupwa nje gizani? Ndiyo. Baada ya Milenia, Shetani na majeshi yake watatupwa nje milele.

Shetani anajua siku zake zimehesabiwa. Wakati wa Ujio wa Pili wa Yesu, Shetani na malaika wake watafungwa kwa kipindi cha miaka 1000 (ona Ufunuo 20:1–3; 1 Nefi 22:26;

M&M 101:28). Wakati tarehe hiyo ya mwisho inapokaribia, majeshi ya uovu yanapigana mno ili kuteka nafsi nyingi iwezekanavyo.

Yohana Mfunuzi alionyeshwa Vita vya Mbinguni kama sehemu ya maono makubwa. Alionyeshwa jinsi Shetani alivyotupwa duniani kuwajaribu wanadamu. Hii ndilo itikio la Yohana: “Ole kwa wakazi wa nchi na wa bahari! Kwa maana yule Ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu” (Ufunuo 12:12).

Kwa hiyo ni namna gani Shetani anatumia wakati wake, akijua hana wakati wa kupoteza? Mtume Petro aliandika “ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitaifuta mtu ammeze” (1 Petro 5:8).

Ni kipi kinamchochea Shetani? Kamwe hatawahi kuwa na mwili, hatawahi kuwa na mke au familia, na hatawahi kuwa na ukamilifu wa shangwe, kwa hivyo anataka kuwafanya wanaume na wanawake wote “wawe na huzuni kama yeye” (2 Nefi 2:27).

Shetani huwalenga wanadamu wote, lakini hasa wale walio na uwezo mkubwa wa kuwa na furaha ya milele. Ni wazi kuwa anamwonea wivu mtu yeyote aliye katika njia ya kuinuliwa. Mafundisho yanatufundisha ya kwamba Shetani “hufanya vita na watakatifu wa Mungu, na kuwazi-ngira” (M&M 76:29).

Vita ambavyo vilianza mbinguni vinaendelea hadi hii leo. Kwa kweli, vita vinakuwa vikali kadiri Watakatifu wanapojitayarisha kwa ajili ya kurudi kwa Mwokozi.

Rais Brigham Young (1801–77) alitabiri “kwamba Kanisa lingeneza, fanikiwa, kukua na kupanuka, na kuwa kwa uwiano na ueneaji wa Injili kwa mataifa ya ulimwengu, pia nguvu za Shetani zingengezeka.”³

Ninafikiri sisi sote tutakubali kwamba utabiri huu unatimizwa huku tukiona uovu ukipenya katika jamii za dunia. Rais Young alifundisha kwamba tunahitaji kujifunza mbinu za adui ili tuweze kumshinda. Ninashirikiana nanyi mbinu nne za Shetani ambazo zimethibitika na mawazo kadhaa kuhusu jinsi unavyoweza kumpinga.

Mbinu za Shetani

1. Majaribu. Shetani hana haya ikija katika kuweka mawazo maovu akilini mwetu. Kitabu cha Mormoni

kinafundisha kwamba Shetani hunong’ona mawazo machafu na ya uhasama na kupanda fikra za mashaka. Yeye hutusumbua ili tuitikie haja za kutawaliwa na tukubali uchoyo na ulafi. Hataki tutambue kule ambapo mawazo haya yanatoka, kwa hivyo ananong’ona, “Mimi sio ibilisi, kwani ibilisi hayupo” (2 Nefi 28:22).

Ni namna gani tunaweza kupinga majaribu haya ya moja kwa moja? Moja ya zana yenye mafanikio zaidi ni kumfu-kuza. Hivyo ndivyo Yesu angefanya.

Hadithi moja ya Mwokozi katika Agano Jipya akiwa juu ya mlima wa majaribu ni ya kuelimisha. Baada ya kila jaribu ibilisi alijitokeza Kwake, Yesu alitumia mbinu ya hatua mbili ili kujikinga: kwanza, alimwamuru Shetani aondoke; kisha akanukuu maandiko.

Wacha nikupe mfano: “Nenda zako, Shetani,” aliamuru Yesu, “kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake” (Mathayo 4:10). Aya inayofuata inaandika, “Kisha Ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia” (Mathayo 4:11). Kinga ya Mwokozi ilikuwa ya ufanisi mno!

Wasifu wa Rais Heber J. Grant (1856–1945) unatupa maarifa jinsi Rais Grant, kama mvulana mdogo alivyompinga ibilisi. Wakati Rais Grant alipotambua kwamba Shetani alikuwa akimnong’oneza, akijaribu kupanda shaka ndani ya moyo wake, alisema tu kwa sauti kubwa, “Bwana Ibilisi, nyamaza.”⁴

Una haki ya kumwambia Shetani aondoke wakati unapokabiliwa na jaribu. Maandiko yanafundisha, “Mpingeni Shetani, naye atawakimbia” (Yakobo 4:7).

Sehemu nyingine ya kinga ya Mwokozi ilikuwa kunukuu maandiko. Kuna nguvu kubwa katika kukariri maandiko, jinsi Yesu alivyofanya. Aya za kimaandiko zaweza kuwa ghala la silaha za kiroho.

Unapojaribiwa, unaweza kutamka amri kama hizi kama vile “Ikumbuke siku ya Sabato uitakase,” “Wapendeni adui zenu,” au “na wema uyapambe mawazo yako bila kukoma” (Kutoka 20:8; Luka 6:27; M&M 121:45). Nguvu za maandiko hazimtishi tu Shetani, lakini pia zinaleta Roho ndani ya moyo wako, ambaye anakuthibitishia, na kukuimarisha dhidi ya majaribu.

2. Uongo na Udanganyifu. Maandiko yanadhihirisha kuwa Shetani ni “baba wa uwongo” (2 Nefi 9:9). Usimwamini anaponong’ona uwongo ujumbe kama



“Hakuna unalofanya sawa,” “Wewe ni mwovu sana kiasi cha kutosamehewa,” “Hutaweza kubadilika,” “Hakuna ana-
yekujali,” na “Hauna vipaji vyovyote.”

Moja kati ya uongo wake anaotumia sana ni ufuatao: “Unahitaji kujaribu kila kitu angalau mara moja—ili tu upate uzoefu. Mara moja haitakuumiza.” Siri ndogo chafu asiyotaka ufahamu ni kuwa dhambi inalevya.

Uongo mwingine utumikao ambao Shetani ataujaribu juu yako ni: “Kila mtu anafanya hivyo. Ni SAWA.” Si SAWA! Kwa hivyo mwambie Shetani kwamba hutaki kwenda katika ufalme wa telestia—hata ikiwa watu wengine wote wanaenda huko.

Ingawa Shetani atakudanganya, unaweza kumtegemea Roho akueleze ukweli. Hiyo ndiyo sababu kipawa

cha Roho Mtakatifu ni muhimu.

Ibilisi ameitwa “mdanganyifu mkuu.”⁵ Yeye hujaribu kutengeneza vitu vya bandia vya kila kanuni ambayo Bwana huleta.

Kumbuka vitu vya bandia sio sawa na vitu vilivyo kinyume chake. Kinyume cha nyeupe ni nyeusi, lakini kitu cha bandia cheupe chaweza kuwa nyeupe kiasi au kijivu. Vitu vya bandia hufanana na vitu halisi ili kuwadanganya watu wasiotia shaka. Ni toleo la udanganyifu kinyume na kitu kizuri, kama vile pesa bandia, haina thamani. Wacha niwaonyeshe.

Mojawapo ya kitu bandia cha Shetani kwa imani ni ushirikina. Kitu bandia cha upendo ni tamaa. Yeye hutengeneza ukuhani bandia kwa kuanzisha ukuhani wa uongo, na huigiza miujiza ya Mungu kwa kutumia uchawi.

Unaweza kumtegemea Roho Mtakatifu akueleze ukweli. Hiyo ndiyo maana Roho Mtakatifu ni muhimu sana.



Ndoa kati ya mwanamume na mwanamke imetakaswa na Mungu, lakini ndoa ya jinsia moja ni ya bandia. Haileti watoto wala kuinuliwa. Ingawaje vitu vyake vya bandia huwadanganya watu wengi, sio vya kweli. Haiwezi kuleta furaha ya kudumu.

Bwana altuonya kuhusu vitu bandia katika Mafundisho na Maagano. Alisema, “Kile kisichojenga siyo cha Mungu, nacho ni giza” (M&M 50:23).

3. Ubishi. Shetani ndiye baba wa ubishi. Mwokozi anafundisha, “Huchochea mioyo ya watu kubishana na hasira mmoja kwa mwingine” (3 Nefi 11:29).

Ibilisi amejifunza kutokana na karne nyingi za uzoefu kwamba mahali ambapo pana ubishi, roho wa Bwana ataondoka. Kutoka alipomshawishi Kaini kumuua Habili,

Shetani amewashawishi ndugu kugombana. Yeye pia huchochea matatizo katika ndoa, miongoni mwa washiriki wa kata, na baina ya wamisionari. Anafurahia kuona watu wazuri wakigombana. Yeye hujaribu kuanzisha ugomvi katika familia Jumapili kabla ya kanisa, kabla ya jioni ya familia nyumbani Jumatatu usiku, na kila mara wana ndoa wanapanga kuhudhuria kikao cha hekaluni. Majira yake ni ya kutabirika.

Wakati kunapokuwa na ubishi nyumbani kwako au kazini, mara moja wacha unachofanya na utafute kuleta amani. Bila kujali nani alianzisha.

Ubishi mara nyingi huanza na kutafuta makosa. Joseph Smith alifundisha ya kwamba “ibilisi hutusifu sana kwamba sisi ni wenye haki sana, wakati tunapozungumzia makosa ya wengine.”⁶ Wakati unapofikiria juu ya hilo, kujiona mwenye haki ni bandia ya haki ya ukweli.

Shetani anapenda kueneza ubishi Kanisani Ana utaalamu katika kuonesha dosari za viongozi wa Kanisa? Joseph Smith aliwaonya Watakatifu ya kwamba mwanzo wa ukeengefu ni kupoteza imani katika viongozi wa Kanisa.⁷

Karibu fasihi zote za kupinga uMormoni msingi wake ni uongo kuhusu tabia ya Joseph Smith. Adui hufanya bidii kumfedhehesha Joseph kwa sababu ujumbe wa Urejesho unategemea historia ya Nabii kuhusu yale yaliyotendeka katika KisituKitakatifu. Shetani anafanya bidii zaidi siku hizi kuliko awali kuwafanya waumini watie shaka ushuhuda wao juu ya Urejesho.

Katika siku za mwanzoni mwa kipindi chetu hiki cha maongozi ya Mungu, ndugu wengi katika uongozi wa ukuhani, kwa majuto yao, hawakubaki waaminifu kwa Nabii. Mmoja wao alikuwa Lyman E. Johnson, ambaye alitengwa na Kanisa kwa mienendo yake ambayo haikuwa ya haki. Baadaye aliomboleza akiwa ameliasi Kanisa: “Ningekubali mkono wangu wa kulia ukatwe, ikiwa ningeamini tena. Kisha nilikuwa nimejawa na shangwe na furaha. Ndoto zangu zilikuwa nzuri. Wakati nilipoamka asubuhi roho yangu ilikuwa yenye furaha. Nilikuwa mwenye furaha mchana na usiku, nikiwa nimejawa na amani na shangwe na shukrani. Lakini sasa ni giza, uchungu, majonzi, mateso yaliyokithiri. Tangu wakati huo sijaona kipindi cha furaha.”⁸

Tafakari juu ya maneno hayo. Yanasimama kama onyo kwa waumini wote wa Kanisa.

Mimi ni mwongofu kwa Kanisa. Nili-batizwa wakati nikiwa na miaka 23 kijana mzima ambaye hajaoa nikisoma katika shule ya udaktari kule Arizona, Marekani. Ninajua moja kwa moja jinsi Shetani anavyofanya kazi juu ya wachunguzi katika kuwachanganya na kuwakatisha tamaa wakati wanapotafuta ukweli.

Katika ujana wangu wote, niliku-wa nikitazama mifano ya marafiki zangu Watakatifu wa Siku za Mwisho. Nilivutiwa na namna walivyo yaongoza maisha yao. Nilifanya uamuzi wa kujifunza zaidi juu ya Kanisa, lakini sikutaka kumwambia yeyote nilikuwa najifunza Umormoni. Ili kuepuka kusumbuliwa na marafiki zangu, niliamua kufanya uchunguzi wangu kuwa wa kibinafsi.

Hii ilikuwa miaka mingi kabla ya tovuti, kwa hiyo nilienda katika maktaba ya umma. Nilipata nakala ya Kitabu cha Mormoni na kitabu kinachoitwa *A Marvelous Work and a Wonder*, na Mzee LeGrand Richards (1886–1983) wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili. Nilianza kuvisoma vitabu hivi kwa hamu kubwa, na vilinitia msukumo.

Wakati roho yangu ilipokuwa ikitaka kujifunza zaidi, Shetani alianza kuno-ng'oneza sikioni mwangu. Aliniambia kwamba ili niweze kuwa mkweli kabisa, nilihitaji kusoma yale yaliyoandikwa na wakosoaji wa Kanisa pia. Nilirudi kwenye maktaba ya umma na kuanza kuangalia kote. Hakika, nilipata kitabu kilichomfedhehesha Nabii Joseph.

Kukisoma kitabu hiki dhidi ya Mormoni kulinichanganya. Nilipoteza yule roho mzuri na ushawishi uliokuwa umeongoza upelelezi wangu. Nilikata tamaa na nilikuwa karibu kuacha uchunguzi wangu wa ukweli. Nilikuwa naomba nipate jibu huku nikisoma fasihi dhidi ya Mormoni!

Kwa mshangao wangu, nilipokea simu kutoka kwa rafiki yangu mmoja aliyekuwa akisoma Chuo Kikuu cha Brigham Young. Alinalika niende nikamtembelee kule Utah, akiahidi



kwamba ningefurahia safari hiyo ya kuvutia macho. Hakuwa anajua nilikuwa nikichunguza Kanisa lake kwa siri.

Nilikubali mwaliko wake. Rafiki yangu alipendekeza twende Jijini Salt Lake tukatembee Temple Square. Alishangazwa na mwikio wangu wa shauku. Hakujuu ni namna gani nilikuwa na hamu ya kujifunza ukweli juu ya Joseph Smith na Urejesho.

Kina dada wamisionari katika Temple Square walikuwa wenye usaidizi mkubwa. Bila ya kujua, walijibu maswali yangu mengi. Ushuhuda wao ulinishawishi “kujibu [zangu] tuhuma,”⁹ na imani yangu ilianza kukua. Thamani ya ushuhuda wa kutoka moyoni haiwezi kupuuzwa.

***Shetani humlenga kila mtu, lakini
hasa wale walio na uwezo mkubwa
wa kuwa na furaha ya milele.***

Rafiki yangu pia alishirikiana nami ushuhuda wake na kunialika niombe na nimwulize Mungu ikiwa Kanisa lili-kuwa la kweli. Katika safari hiyo ndefu kurudi Arizona, nilianza kusali kwa imani—kwa mara ya kwanza “na kwa moyo wa kweli, na kusudi halisi” (Moroni 10:4). Wakati fulani katika safari hiyo, ilionekana kama kuwa gari langu lilikuwa limetiwa nuru na mwanga. Nilijifunza kuwa mwanga unaweza ukaondoa giza.

Baada ya kuamua kubatizwa, Shetani alianza mapambano ya mwisho. Alijaribu familia yangu, ambao walifanya kila kitu katika uwezo wao kunikatisha tamaa, na walikataa kuhudhuria ubatizo wangu.

Nilibatizwa hata hivyo, na pole pole mioyo yao ilifanywa kuwa laini. Walianza kunisaidia kuchunguza historia ya familia yangu. Miaka michache baadaye, nilimbatiza ndugu yangu mdogo. Rafiki ambaye alinalika nimtembelee kule Utah sasa ni mke wangu.

4. Kuvunjika Moyo. Shetani hutumia kifaa hiki kwa ufanisi kwa Waaminifu wakati mengine yote yanapokuwa yameshindwa. Kwangu mimi, wakati ninapoanza kuhisi kuvunjika moyo, ni ya manufaa kwangu kutambua ni nani anajaribu kuniangusha. Hili linanifanya nikasirike kiasi cha kuchangamka—ili tu nimchukize ibilisi.

Miaka kadhaa iliyopita, Rais Benson alitoa hotuba iliyoitwa “Msikate Tamaa.” Katika hiyo hotuba ya kugusa hisia, alionya, “Shetani anazidi kujitahidi kuwashinda watakatifu na kukata tamaa, kuvunjika moyo, kufa moyo, na huzuni.”¹⁰ Rais Benson aliwahimiza waumini wa Kanisa kuwa macho, na akawapa mapendekezo 12 ya kweli ya kukabiliana na kuvunjika moyo.

Mapendekezo yake yanajumuisha kuwahudumia wengine; kufanya kazi kwa bidii na kuepukana na kuwa wavivu; kuwa na tabia nzuri za kiafya, hii ikiwa ni pamoja na kufanya mazoezi na kula vyakula katika hali yake halisi; kutafuta baraka za ukuhani; kusikiliza muziki unaotia msukumo; kuhesabu baraka zako; kuweka malengo. Na juu ya yote, jinsi maandiko yanavyotufundisha, tunapaswa kusali siku zote ili tuweze kumshinda Shetani (ona M&M 10:5).¹¹

*Shetani hutetemeka wakati anapomwona
Mtakatifu mdhaifu kabisa akiwa amepiga magoti.¹²*

Ni muhimu kujua ya kwamba kuna mipaka ya nguvu za uovu. Uungu huweka mipaka hiyo, na Shetani hajaruhusiwa kuivuka. Kwa mfano, maandiko yanatuhakikishia ya kwamba “kwani uweza haujatolewa kwa Shetani wa kuwaribu watoto wadogo” (M&M 29:47).

Kizuizi kingine kikubwa ni kwamba Shetani hajui mawazo yetu hadi tumwambie. Bwana alieleza, “Hapana yeyote ila Mungu ambaye hujua mawazo yako na dhamira ya moyo wako” (M&M 6:16).

Pengine hii ndiyo maana Bwana ametupa amri kama vile “Usinung’unike” (M&M 9:6) na “Usimseme jirani yako uovu, wala usimdhuru” (M&M 42:27). Ikiwa unaweza jifunza kuuzuia ulimi wako kwa hatamu (ona Yakobo 1:26), mwishowe hutampa shetani maelezo mengi sana. Wakati anaposikia kunung’unika, kulalamika, na kukosoa, yeye kwa uangalifu huandika. Maneno yako hasi yanafichua udhaifu wako kwa adui.

Nina habari njema kwenu. Majeshi ya Mungu ni mengi zaidi kuliko ya Lusiferi. Unaweza ukaangalia kote na ufikirie wewe mwenyewe, “Dunia inageuka kuwa ovu na ovu zaidi. Shetani ni lazima anashinda vita.” Usidanganywe. Ukweli ni kwamba, tunamshida adui kwa idadi. Kumbuka, theluthi mbili ya watoto wa Mungu walichagua mpango wa Bwana.

Kaka zangu na dada zangu, hakikisheni ya kwamba mnapihana katika upande wa Bwana. Hakikisha ya kwamba umebeba upanga wa Roho.

Ni ombi langu kwamba mwishoni mwa maisha yenu, mweze kusema pamoja na Mtume Paulo, “Nimevipiga vita vilivyovizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda” (2 Timotheo 4:7). ■

MUHTASARI

1. Mwongozo wa Maandiko, “Lusiferi,” scriptures.lds.org.
2. Ezra Taft Benson, “Beware of Pride,” *Ensign*, Mei 1989, 5.
3. *Discourses of Brigham Young*, sel. John A. Widtsoe (1954), 72.
4. Ona Francis M. Gibbons, *Heber J. Grant: Man of Steel, Prophet of God* (1979), 35–36.
5. Ona, kwa mfano, Dieter F. Uchtdorf, “You Matter to Him,” *Liahona*, Nov. 2011, 20; Gordon B. Hinckley, “The Times in Which We Live,” *Liahona*, Jan. 2002, 86.
6. *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* (2007), 369
7. Ona *Teachings: Joseph Smith*, 318.
8. Lyman E. Johnson, in Brigham Young, *Deseret News*, Aug. 15, 1877, 484.
9. Dieter F. Uchtdorf, Njoo, Jiunge Nasi, *Liahona*, Nov. 2013, 23.
10. Ezra Taft Benson, “Do Not Despair,” *Ensign*, Nov. 1974, 65.
11. Ona Ezra Taft Benson, “Do Not Despair,” 65–67.
12. William Cowper, in Robert Andrews, comp., *The Concise Columbia Dictionary of Quotations* (1987), 78.

TASWIRA ZA IMANI

Skaidrite ni mmoja ya watu wenye furaha mmoja niliowahi kukutana nao. Maisha yake yanaonekana ni picha kamili. Lakini alipokuwa mtoto aliishi na mama yake mlevi, ambaye alikuwa hawezi kuwatunza yeye na dada yake. Skaidrite alishikilia mkono wa dada yake wakati dada akifa kutokana na njaa. Kuanzia umri wa miaka 8, Skaidrite aliishi katika nyumba mbali mbali za kulelea watoto. Alipigwa mateke, alipigwa bakora, na kuzuiwa kusali. Alitendewa kama mtumwa. Kwa miaka mingi, alifikiria sana kujiua.

Miaka mingi baadaye, akitafuta matumaini, Skaidrite aliingia katika nyumba ya mikutano ya LDS.

LESLIE NILSSON, MPIGA PICHA

Skaidrite Bokuma

Liepaja, Latvia

“Dada mmisionari aliniamkia na alitabasamu. Nilifikiri alikuwa ni malaika. Tangu siku ile maisha yangu yamebadilika. Hivi sasa imefikia miaka 17, na mawazo yote ya kumaliza maisha yangu yametoweka. Leo, mimi nina mawazo chanya. Ninapokuwa na masumbuko, ninayaweka kwa Mungu. Nimejifunza kumtegemea Yeye kwa kila kitu. Maisha ni mazuri kwangu.”

Jifunze namna ya kuwatambua na kuwasaidia wale ambao yawezekana wanafikiria kujinyonga katika lds.org/go/41739.





TAFADHALI USIUCHEZE WIMBO HUO

Muda fulani uliopita, familia yangu na mimi tuliishi Veracruz, Mexico, ambako watoto wangu walihudhuria shule ya msingi. Kila asubuhi nilipokuwa nawasaidia watoto wangu watatu kuwa tayari kwenda shule, tulisikiliza radio—kituo kilichopendwa sana jijini—na mfuatano wa vipindi uliofurahisha sana ulioongozwa na kijana wa kiume mtangazaji wa radio.

Tulianza kusikiliza wimbo wa kuvutia sana. Nilipoanza kusikiliza kwa makini maneno ya wimbo, nilitambua kwamba mambo yaliyokuwa yanasemwa, ingawa sio ya kishenzi, yalikuwa yenye kushawshi mabaya na yasiyo na maadili.

Nilisema kwa kudhamiria kwa watoto wangu, “Hatuwezi kusikiliza aina hii ya lugha.” Labda hawakusikiliza hata kidogo maneno ya wimbo wenyewe, lakini walisikiliza vya

kutosha kuweza kuimba tuni yake huku mdomo ukiwa umefungwa.

Waliniona nikizima sauti ya redio hiyo na wakaniuliza nilikuwa nafanya nini. “Ninakwenda kumwambia mtangazaji wa radio hii kuuondoa wimbo huo kutoka kwenye programu.” Mshangao wao ulinitia moyo kuchukua hatua zaidi.

Hawakuweza kuamini na hata mimi sikuweza kuamini, lakini niliua simu na kukipigia kituo cha radio. Sikutegemea kupata jibu, lakini kwa mshangao wangu, mtangazaji yule yule wa radio tuliyemsikia kwenye burudani alijibu simu yangu mara moja.

Nilimwambia kwamba sikukubaliana na kusikilizwa kwa wimbo ule, kwa


Wakati tuliposikia wimbo wa kuvutia sana kwenye radio, niliamza kusikiliza kwa makini maneno ya wimbo huo.

vile familia nyingi ilikuwa imetuni radio yao wakati ule asubuhi. Yeye aliniuliza ningepedekeza aubadilishe na nini, lakini mwenendo wake ulikuwa wenye adabu nzuri kiasi kwamba nilimwomba tu asiucheze wimbo huo wakati wa muda ambao watoto wapo nyumbani.

Sikugundua kama simu yangu ilikuwa hewani, lakini nilikuwa nimeshukuru tu kwamba mtangazaji yule wa radio amesikiliza. Na kwa siku chache zilizofuata, niliweza kusema kwamba ombi langu limekubaliwa.

Tukio lile limenihakikishia kwamba tunapaswa kuwa na ujasiri wakati inapokuwa mikononi mwetu kufanya maamuzi na kufanya kilicho cha muhimu ili kuwalinda watoto wetu kutokana na vishawishi hasi. Tunapofanya hivyo, Roho Mtakatifu anaweza kuendelea kuwa mwenzetu wakati wote. ■

Maria Hernandez, Texas, USA



POCHI ILIYOPOTEA

Hivi karibuni nilihamia kwenye nyumba mpya na nikawa-omba baadhi ya waumini wa Kanisa kunisaidia kazi maalumu katika nyumba yangu. Katikati ya mradi, niliondoka kwenda kununua vifaa tulivyo-hitaji kumaliza kazi. Baada ya kumaliza mradi, niligundua sikuwa na poch yangu. Nilitaharuki kwa sababu ndani ya poch yangu kulikuwa na nyaraka zangu binafsi pamoja na pesa ambazo nilikuwa nimepokea kutoka kwa mteja asubuhi ile. Nikarudi kufuatilia hatua zangu kwenda kule niliko nunua vitu lakini sikuwa na bahati. Nikaenda nyumbani na kutafuta kuona kama niliangusha sehemu, lakini bado sikuiona. Nikaanza kufikiria uwezekano kwamba nianze kupata nakala mpya za nyaraka zote. Ndipo kabla ya kuondoka nyumbani, rafiki yangu aliniuliza “Je umeshaomba tayari?”

Mara moja nikafikiria, “Ndio tayari nimekwisha omba!”

Lakini kwa kweli, sikuwa nimeomba kwa dhati. Badala yake, nilitaka kulazimisha mapenzi yangu kwa Baba wa Mbinguni na kwa namna fulani kuifanya kuwa ni kazi Yake kunisaidia mimi kutafuta poch yangu. Lakini kisha nikakumbuka maandiko katika Isaya 55:8: “Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana.”

Jumapili nilikwenda Kanisani, na muumini aliyekuwa na mimi jana



Nilimwomba Baba wa Mbinguni kujibu maombi yetu ili kuimarisha imani ya mke na watoto wangu.

aliniambia kwamba ameomba sana kwa Baba wa Mbinguni ili niweze kuipata poch yangu. Alisema amehisi kwamba nitaipata. Baadaye, nikiwa nimekaa kwa ajili ya mafunzo binafsi, nikaanza kusoma *Kupokea Majibu ya Maombi Yetu* na Mzee Gene R. Cook, mshiriki wa heshima wa Sabini. Ukurasa wa kwanza ulielezea habari sawa na ya kwangu: Mwana wa Mzee Cook alipoteza poch, hivyo familia ilikusanyika pamoja na kuomba kwa Bwana ili waweza kuipata.

Baada ya kusoma juu ya tukio lile, mimi niliyaweka katika vitendo yale niliyojifunza na kuwakusanya mke na watoto wangu pamoja. Tukatengeneza duara, na kila mtu alitoa maombi, tukimwomba sana Bwana kutusaidia

kuipata poch kama yalikuwa ni mapenzi yake.

Nimewahi kushuhudia nguvu za maombi, lakini baadaye, nikiwa ninaomba kwa siri, nilimwomba Baba wa Mbinguni kujibu maombi yetu ili kuimarisha imani ya mke na watoto wangu.

Siku iliyofuata mtu akanipigia simu. Alisema ameipata poch yangu, pamoja na pesa. Nikalia kama mtoto kwa sababu maombi yangu yalijibiwa na imani ya familia yangu iliimarishwa.

Ninajua kwamba Baba wa Mbinguni, hata pamoja na kuwa na watoto wengi wa kuwahudumia, anamjibu kila mmoja wetu kulingana na muda Wake na katika njia Yake. ■ Luiz Marcelino, Goiás, Brazil

KUOKOLEWA UKUMBINI

Mume wangu mara nyingi alitakiwa kufanya kazi Jumapili, akiniacha mimi kuwa msimamizi wa watoto wetu wakiume wanne kanisani peke yangu. Jumapili moja ya kukumbukwa wakati wa kipindi cha sakramenti, watoto wangu wawili walikuwa wakigombana. Kama niki-mfanya mmoja wa wavulana hawa kukipenda kitabu, kaka yake atakitaka. Nilijaribu vitafunwa, wanasesere, na kupaka rangi, lakini hakuna kilicho fanya kazi. Nilikuwa nimeshindwa kwa watoto wangu, ambao hawakuonekana kuwa wangekaa chini kimya kwa saa moja.

Nikatoa kitu kidogo cha kuchezea kwenye mkoba wangu na kumpa mtoto wangu wa mwaka mmoja. Mara moja kilio cha nguvu kilikuja kutoka kwa mwanangu wa- miaka- mitatu, Tyson wakati alipomvamia kaka yake mdogo, akijaribu kumpokonya mwanasesere. Niliaibika nikiwa nimewabeba watoto wawili waliokuwa wakipiga kelele na kugombana kwenda nje ukumbini.

Uso wangu ghafla ulilowa kwa machozi ya moto. Kwa nini hili linakuwa gumu? Nilikuwa nafanya kile ambacho Baba wa Mbinguni alitaka mimi nifanye kwa kuileta familia yangu kanisani, sawa? Lakini nisingeweza kufanya tena. Nilikuwa nimechoka na kuaibika kwa kugombana kwa watoto wangu katika kipindi cha sakramenti peke yangu kila wiki. Sikutaka kurudi tena.

Nilikaa na mawazo haya kwa

Nilikuwa nimeshindwa kwa watoto wangu, ambao hawakuonekana kuwa wangekaa chini kimya kwa saa moja.



sekunde 15 tu, kisha dada ambaye sikumfahamu vizuri akatoka nje ukumbini kunifuata. Jina lake lilikuwa Dada Beus. Mara nyingi alikaa peke yake, huku mume wake akihudumu katika uaskofu na watoto wake walikuwa wakubwa. Alisema, “Mara zote uko hapa peke yako! Ninaweza kuona kwamba unajitahidi sana. Je, Tyson anaweza kukaa na mimi?” Sikuweza kufikiria jibu! Nilikubali kwa kichwa akiwa anamchukua kwa mkono na kumwongoza, sasa akiwa mtulivu na mwenye furaha, akirudi kanisani.

Nikafuta machozi yangu, nika-mchukua mtoto wangu, na kwa unyenyekevu kurudi tena kanisani kufurahia mkutano kwa amani.

Jumapili iliyofuata tukiwa tunaingia katika mkutano wa sakramenti, Tyson alimtafuta rafiki yake mpya. Usiku angeomba, “Asante, Baba wa Mbinguni, kwa ajili ya Dada Beus. Ninampenda sana!”

Imekuwa miaka mitatu, na Tyson bado anamtafuta Dada Beus kanisani. Mwaka uliopita alitwa kuwa mwalimu wa Watoto wa Msingi darasa la Tyson. Alikuwa mvulana mdogo mwenye furaha aliyehai.

Ninafuraha tele kwa Dada Beus na kukubali kwake kuwapenda na kuwatumikia wengine. Ninajua kwamba tunaweza kubariki maisha ya wengine wakati tunapohudumu kama Mwokozi alivyofanya. ■

Kristi Lewis, Utah, Marekani

TAYARI!

Wakati wa ushahidi wangu kama askofu Jumapili moja jioni, nilipata nafasi ya kukaa chini pamoja na rafiki yangu mzuri kuingea kuhusu baadhi ya changamoto alizokuwa anakabiliiana nazo. Baada ya kusikiliza matatizo yake kwa dakika chache, nilihisi kwamba alichokuwa anahitaji ni kusoma maandiko mara kwa mara. Pia nilikumbushwa kwamba, kama askofu wake, na mimi pia nataka kusoma maandiko mara kwa mara, kitu ambacho nilikuwa nasumbuka nacho. Hivyo nilipendekeza kwamba tuwe “washirika wawajibikaji” katika kujitahidi kujifunza kwa mfululizo zaidi.

Kila siku baada ya kumaliza kusoma maandiko, tulitumiana ujumbe mfupi wa neno *Tayari!* Tukijua kwamba kuna mtu mwingine alikuwa anasubiri kusikia iwapo amemaliza au hajamaliza kusoma kwa siku ile ilikuwa ni kuhamasishana kwetu wote. Kama mmoja wetu amesahau, kupata ujumbe mfupi ilikuwa ni kukumbushwa. Kama mmoja wapo hajatuma ujumbe mfupi, hakuachwa nyuma Tuliacha kila mmoja wetu achukue changamoto hii bila ya kumfanya


mwingine ajisikie vibaya.

Tuliianzisha changamoto hii miezi sita iliyopita sasa, na sikumbuki siku ambayo tulikosa kusoma maandiko yetu. Kaka huyu alisimama wakati wa kipindi cha mfungo na ushuhuda miezi mwili iliyopita na kutoa ushuhuda wake wa matokeo mazuri aliyo yapata akiwa anasoma maandiko kila siku yeye na familia yake.

Ninamshukuru kaka huyu na urafiki wake, na pia ujumbe wake mfupi wa kila siku. Nimeona jinsi teknolojia, inapotumika vizuri, inavyoweza kuendeleza maisha yetu. Pia ninashukuru kwa ajili ya maandiko na jinsi yanavyo shuhudia juu ya Kristo. Ninajua kwamba dhabihu ya kulipia dhambi ya Mwokozi inamwezesha kila mmoja wetu kurudi kuishi pamoja Naye siku moja. ■

Alex Whibley, British Columbia, Canada

Tukawa “washirika wawajibikaji” katika kujitahidi kujifunza maandiko kwa mfululizo zaidi.





LIAHONA YAKO BINAFSI

. . . Baraka zako hazipaswi kuku-njwa kimaridadi na kuwekwa kando. Haifai kuwekwa kwenye fremu au kuchapishwa. Bali, ni za kusomwa. Zinapaswa kupendwa. Ni za kufuatwa. Baraka zako za kipatriaki zitakuwezesha kupitia katika usiku wa giza. Zitakuongoza wewe kupitia hatari za maisha. Baraka zako za kipatriaki kwako ni Liahona binafsi ya kupanga njia na kuongoza njia yako.

Rais Thomas S. Monson, Your Patriarchal Blessing: A Liahona of Light, *Ensign*, Nov. 1986, 66.



Kuelewa Baraka zako za Kipatriaki

Na Allie Arnell na Margaret Willden

Maisha yamejaa maji yasiyopimwa: *Wapi napaswa kwenda shule? Napaswa kujifunza nini? Je, napaswa kwenda misheni? Nimuoe nani?* Kama ungepewa ramani binafsi ili kuongoza maamuzi ya maisha yako, ungefuata?

Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo wametupa ramani kama hiyo—baraka za kipatriaki—ili kutupa mwelekeo katika maisha yetu. Ingawa tumepelewa kipawa cha haki ya kujiamulia ili kufanya maamuzi kwa hiari yetu wenyewe.

Lakini kuwa tuu na ramani hakutoshi. Lazima tujifunze, kuelewa, na kutumia maana iliyomo katika ramani. Hali kadhalika, unapokuja kuelewa lugha iliyotumika katika baraka yako ya kipatriaki—mwongozo wako binafsi maishani—utaweza kujua kuwa wewe ni nani katika macho ya Mungu na nini unachoweza kuwa.

Gundua Ukoo Wako

Kwanza kabisa, baraka yako ya kipatriaki inatangaza ukoo wako, au kabila mahsusi kati ya makabila

kumi na mawili ya Yakobo (ambaye baadaye alitwa Israeli) ambalo wewe unastahili kuwa. Ingawa sisi sio wote wazawa halisi wa Yakobo, maandiko yanatufundisha kwamba Waumini wa Kanisa wameasiliwa katika nyumba ya Israeli: “kwani kadiri wengi watakavyo ipokea Injili hii wataitwa kwa jina lako, nao watahesabiwa kuwa uzao wako, na watainuka na kukubariki, kama baba yao” (Ibrahimu 2:10).

Shelisa Schroepel wa Utah, Marekani, anasema, “Kujua kwamba mimi ni wa kutoka nyumba ya Yakobo kunanisaidia kujua makusudi yangu katika maisha haya na kwa nini ninaitwa kwenye wito fulani katika Kanisa.”

Baraka yako ya kipatriaki inaweza pia kueleza baraka zo zote zenye uhusiano ambazo zinafuatana mahsusi na kabila lako. Kwa mfano, waumini wengi wa Kanisa wanahusika na kabila la Efraimu, kabila ambalo lina majukumu ya kipekee kusambaza ujumbe wa injili ya urejesho ulimwengu (ona Kumbu kumbu ya Torati 33:13–17; M&M 133:26–34).



Kutambua sehemu za baraka yako kutakusaidia kupata mwelekeo wa maisha yako.

Tafuta Ushauri Binafsi

Ikitumika vizuri, ramani inamfanya msafiri asipotee. Vile vile, kwenye safari hii ya kidunia, baraka yako ya kipatriaki inaweza kutoa ushauri na mwelekeo kwa maisha yako. Baraka zako za kipatriaki hazikuelezi tu nini cha kufanya, lakini inaweza kutoa utambuzi binafsi kuhusu njia zipi—kama zikifuatwa katika imani—zinaweza kukusaidia wakati unapoyaoanisha maisha yako na mapenzi ya Baba wa Mbinguni. Unapojifunza baraka yako ya kipatriaki na kutaka kuishi kwa



VIDOKEZO KWA AJILI YA MAFUNZO

- Tambua ushauri, maonyo, vipaji, na ahadi katika baraka zako za kipatriaki. Omba kuhusu jinsi vinavyoweza kutumika kwako katika hatua yako ya sasa ya maisha.
- Jifunze baraka yako kikamilifu na mara kwa mara katika maisha yako yote. Sentensi hii hii inaweza kuwa na maana nyingi kwako kwa wakati tofauti.
- Kumbuka kwamba baraka ya kipatriaki haitaji kila kipeengele cha maisha yako. Hata kama lengo muhimu halikutajwa katika baraka yako, linaweza bado kuwa kitu cha muhimu kujitahidi nacho.
- Kuwa mtiifu kwa injili. Baraka katika baraka zako za kipatriaki zinaweza kupatikana kulingana na uaminifu wako.
- Weka malengo ya kutafuta karama na kukuza vipaji vilivyotajwa katika baraka yako.
- Tafakari wapi unaelekea katika maisha na wapi hatimaye unataka kuwa. Jinsi gani malengo yako yanaoana na baraka zako za kipatriaki?
- Fikiria kufanya nakala ya baraka zako za kipatriaki ili itumike kwa mafunzo. Unaweza kuandika mawazo yako, yawekee alama maneno ambayo yamejitokeza, na kuandika maandiko matakati fu ambayo yana uhusiano na baraka zako.

namna ambayo inamwalika Roho wa Mungu, unaweza kupata usalama, furaha, na mwongozo.

Gabriel Paredes wa Lima, Peru, anasema, “Baadhi ya ushauri ambao nilipewa katika baraka yangu nimeweza tu kuutuima kikamilifu na familia yangu baada ya kuunganishwa na mke wangu.

“Hivi karibuni tumekuwa tukishangaa nini tungeweza kufanya ili kuimarisha na kujenga familia yetu mpya. Swali letu lilijibiwa kupitia baraka yangu ya kipatriaki. Ndani yake nimeshauriwa kuweka kipaumbele heshima, uvumilivu, na upendo katika familia yangu, kwa sababu hizi ni baadhi ya misingi muhimu ya injili ya Yesu Kristo.

“Kama tulivyo fokasi juu ya hili, mke wangu na mimi tumeweza kuyashinda matatizo. Bado tuna changamoto mara moja kama familia, lakini tuna furaha. Nilihisi kama Bwana alikuwa ana nikumbusha jinsi ambavyo ningeweza kuwa na familia ambayo aliniahidi. Najua kwamba Bwana anasema kupitia baraka za kipatriaki na kwamba ushauri ulio ndani yake utumike katika maisha yetu.”

Sikiliza Maonyo

Ramani haitalazimika kuweka alama kila hatari zilizomo katika njia, bali kwa bahati mzuri, baraka za kipatriaki mara kwa mara zinatoa sauti za onyo ili kutulinda tukiwa njiani. Baadhi ya haya maonyo madogo husaidia kutulinda kutokana na ushawishi wa shetani; mengine yanaweza kutuelimisha juu ya jinsi tunavyoweza kushinda utu wa asili ndani yetu.

Kwa Caitlin Carr wa Utah, baadhi ya maonyo madogo katika baraka yake ya kipatriaki haikuwa wazi mara moja, lakini mafunzo yake ya baadaye ya baraka yake yalitoa utambuzi mpya.

“Wakati nilipopokea baraka yangu ya kipatriaki, nilionywa kuhusu watu watakao nijaribu na kuniyumbisha kutoka kwenye ukweli kwa mazungumzo ya kupendeza. Sikufikiria sana kuhusu hilo; nilikuwa na imani thabiti katika mafundisho niliyofundishwa.

“Hata hivyo, mwaka uliofuata nilikabiliwa na mawazo na falsafa ambazo, kwa juu juu zilionekana kujikita katika haki na upendo lakini haikuwa hivyo. Ujumbe huo ulionekana kuja kutokea kila mahali: vyombo vya habari, shuleni, hata marafiki wa karibu. Hata hivyo, nilijua falsafa hizi zilikuwa kinyume na mpango wa Mungu, nilijikuta mwenyewe nikitaka kuunga mkono vyote hivi ambavyo ni mawazo mapya ya kilimwengu *na* Kanisa. Mara moja nilitambua kwamba ‘hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili’ (Mathayo 6:24) na kwamba nisitegemee hekima ya binadamu. Baba wa Mbinguni alimaliza wasi wasi wangu kupitia maandiko na akazungumza amani akilini na moyoni mwangu. Na matokeo yake, ushuhuda wangu umeimarika na nimekuwa imara zaidi katika kulinda kile ambacho najua kuwa ni cha kweli.”

Kukuza Karama na vipaji

Baraka zako za kipatriaki zinaweza pia kutaja karama za kiroho na vipaji ambavyo Bwana amekupa ili kuujenga ufalme Wake. Kama baraka

zako zinataja kipaji ambacho sio cha kawaida kwako, hii inaweza kuwa kwa sababu hujawa bado na nafasi ya kugundua au kukuza kipaji hiki. Kupitia kutafuta kwa bidii na msaada wa Bwana, unaweza kukua ukijumuishisha kipaji hiki na vingine zaidi.

Kukuza vipaji vyako kunakusaidia kugundua vitu vya kipekee unavyo changia kwenye kazi ya Bwana.

Johanna Blackwell wa California, Marekani, anatafakari karama na vipaji katika baraka zake anapohisi kujaribiwa kujifananisha na wengine: “ninapo yaangalia maneno yote katika baraka yangu ya kipatriaki, nina kumbushwa kwamba nimebarikiwa na karama nilizozihitaji binafsi kushinda majaribu na kushiriki katika uharakishaji wa kazi ya Bwana.

“Baraka zangu zinanieleza juu ya uwezo wangu, wa kupenda, kusamehe, na kuwa na ujasiri wa kuchanganika na wale wanao nizunguka. Pale

nilipozitumia karama hizi, Bwana amenibariki kwa wingi wa hamu ya kukutana na kujumuika na watu wapya na tamaduni mpya. Kwa hiyo, ushuhuda wangu umekua kwamba sisi wote ni watoto wa Baba wa Mbinguni anaye tupenda, na nimeweza kuwaokoa wengine wakati kila mmoja wetu anapotafuta kuwa zaidi kama Kristo.”

Tafuta Baraka Zilizoahidiwa

Mwishowe, baraka zetu za kipatriaki zinaonesha ahadi zilizoahidiwa za Baba wa Mbinguni kwetu kama tutabaki kuwa waaminifu Kwake. Hakuna uhakikisho wa lini ahadi hizi zititimizwa, lakini tunaweza kujua kwamba ili mradi tunaishi injili kwa utiifu, zititimizwa, ama katika maisha haya au yajayo.

Sergio Gutierrez wa Nevada, Marekani, anategemea ahadi katika baraka yake ya kipatriaki wakati wo wote anapohisi wasiwasi kuhusu

mipango yake ya kazi ya baadaye: “Wakati mwingine nahisi mashaka kuhusu maisha yangu ya baadae, lakini kuna ahadi katika baraka yangu ya kipatriaki ambayo siku zote inatuzia akili zangu. Ahadi hii inanisaidia kujua kwamba ili mradi nafanya kazi kwa bidii na kubaki kuwa mwaminifu, nitakuwa na rasilimali muhimu za kuweza kutunza familia yangu na kulijenga Kanisa. Sijui bado kwa uhakika ni aina gani ya kazi ninataka kuifuata, lakini kuwa na ahadi hii inanipa imani na matumaini.”

Kama umewahi wakati wowote kustajabu nini mapenzi ya Baba wa Mbinguni yalivyo kwa ajili yako haupo peke yako. Bwana alielewa kwamba utakabiliwa na njia nyingi tofauti ambazo ungeweza kufuata katika maisha yako, kwa hiyo Yeye amekupa ramani binafsi ili uyaweke maisha yako yaoane na injili Yake. Baraka za kipatriaki haziwezi kufanya maamuzi kwa ajili yetu, lakini zinaweza kutuongoza kwenye ufunuo wetu binafsi. Kupitia baraka zetu za kipatriaki, tunaoneshwa jinsi tunavyoingia katika mpango wa Bwana wa kuwakusanya wana wa Israeli kwa kujifunza juu ya kabila letu; tunapewa ushauri binafsi, maonyo madogo madogo, na ahadi; na tumefundishwa kuhusu karama za kipekee na vipaji ambavyo Baba wa Mbinguni ametupa ili kumtumikia Yeye. Ili mradi unajaribu kuishi kufuatana na misingi hii ya baraka zako za kipatriaki, unaweza kujua kwamba maamuzi yako yamekuwa ndani ya mapenzi ya Bwana kwa ajili ya maisha yako. ■

Waandishi Wanaishi Illinois, Marekani na New York Marekani.



Bwana amekupa wewe ramani binafsi ili kuweka maisha yako yaoane na injili Yake.

Kujitayarisha kwa ajili ya Safari Mpya

Na Karina Martins Pereira Correia de Lima

Katika wiki zilizotangulia ndoa yangu na kuunganishwa hekaluni, nilianza kuwa na wasi wasi kidogo kuhusu mambo yote ambayo nilihitaji kufanya kabla ya kuanzisha familia yangu mpya. Licha ya furaha hiyo yote ya wakati huo, nilijihisi nimefadhaika kuhusu kuandaa utaratibu wetu mpya, kupanga hali yetu ya kifedha, kutafuta sehemu ya kuhifadhi mali yetu, na majukumu yangu mapya kama mke. Nilitaka kuhakisha ya kwamba tulianza ndoa yetu kwa njia sahihi kwa kutengeneza nafasi katika maisha kwa ajili ya shughuli muhimu kama vile kushika amri na kupata muda wa kuwa pamoja kama mume na mke licha ya maisha yetu yenye shughuli nyingi mno.

Kadiri siku ya harusi ilivyokuwa ikikaribia, nilishangazwa na mfululizo wa majinamizi yaliyohusu aina

zote za matatizo ambayo yangeweza kuiathiri familia. Kwa sababu nina-toka katika familia yenye upendo lakini iliyoteseka sana, iliyotishiwa na mabishano makali na ya kila mara na mioyo iliyovunjika, ndoto hizo mbaya ziliniathiri zaidi ya vile ilivyonipasa. Kwa hivyo usiku mmoja, baada ya nyingine kadhaa kama hiyo, niliamka nikitokwa na jasho na nikaamua kufuata ushauri ambao Dada Neill F. Marriot, Mshauri wa Pili katika Urais Mkuu wa Wasichana, alitoa katika hotuba yake “Yielding Our Hearts to God” (*Liahona*, Nov. 2015, 30–32).

Nilifunga macho yangu na kuomba, “Baba Mpendwa wa Mbinguni, ni nini naweza kufanya ili kuzuia mambo haya mabaya mbali na familia yangu?

Jibu lilinijia upesi na kwa nguvu kana kwamba mtu fulani alikuwa amefungua mlango kichwani mwangu na kuweka wazo lile hapo. Ile sauti ndogo,

Kama vile Nefi alivyosafiri kwa meli kuelekea asiko kujua, vivyo hivyo mimi nilihitaji kuwa na imani kwa Bwana kuhusu kuanzisha familia.

tulivu ilinshawishi, “Fanya kile tu unachopaswa kufanya. Kuwa mwaminifu katika kila hatua.” Roho alinong’ona ushauri fulani maalum, na nilihisi kwamba ikiwa ningefanya mambo hayo, kila kitu kingekuwa sawa.”

Nilitabasamu na kuhisi kifua changu kikiwa kimejaa upendo. Wasiwsi wote ulisahaulika ghafla,



kwa sababu nilijua ilikuwa ni kweli. Nilikuwa nimewahi kumsikia Roho Mtakatifu hapo awali, lakini kamwe sio jinsi nilivyomsikia kwa nguvu usiku ule. Nilihisi upendo wa Baba yetu wa Mbinguni na Mwokozi ukinizingira, na nilijua ya kwamba faraja na wokovu wa familia yangu ilikuwa muhimu kwao kama vile ilivyokuwa kwangu.

Kama nyongeza ya uhakikisho, hadithi kutoka kwenye maandiko ilinjia katika fahamu zangu—wakati Bwana alipomuamuru Nefi kujenga Meli: “Na ikawa kwamba Bwana akanizungumzia, na kusema: Wewe utajenga merikebu, *kulingana na vile nitakavyo kuonyesha*, ili niwavyushe watu wako haya maji” (1 Nefi 17:8; imetiliwa mkazo).

Nefi na familia yake walikuwa nyikani kwa muda wa miaka mingi, wakivumilia aina zote za dhiki. Angeweza kuhisi hofu ya kuanza safari ya kuvuka bahari na kuruhusu hofu zake kuwa na nguvu zaidi kuliko imani yake. Lakini hakufanya hivyo. Alikubali na kutii maelekezo kutoka kwa Mungu. Alikuwa na imani ya kwamba ahadi zake Bwana zingetimizwa. Bwana hakumwambia Nefi kwamba tufani hazingetokea au kwamba mawimbi hayangeipiga meli. Lakini

Yeye alimwambia Nefi ikiwa angefuata maelekezo Yake, angeweza kuiongoza familia yake kwa usalama kuvuka bahari hadi katika nchi ya ahadi.

Niligundua ya kwamba mimi pia nilikuwa nimesafiri kupitia katika nyika kwa muda wa miaka mingi, lakini sasa nilikuwa mbele ya bahari, nikijitayari-sha kwa safari mpya: ndoa. Nimepewa wito—na nafikiri hiyo ndiyo hali ilivyo kwa familia zote za Watakatifu wa Siku za Mwisho—kujenga meli kwa kufuata maelekezo ya Mungu.

Mara tu mume wangu na mimi tulipooana, matatizo yalijitokeza. Niliugua, na tulihangaika kuweka hali yetu ya kifedha katika uwiano na kufanya yale mazoea mazuri yote tuliyokuwa tumeamua kuyafuata.

Lakini ushauri ambao nilikuwa nimeupokea usiku ule ulisalia moyoni mwangu. Tulijaribu kila siku kujifunza na kulihifadhi neno la Mungu moyoni mwetu, kufuata mifano mizuri ya viongozi wetu wapendwa—ikiwa ni pamoja na Kristo—na kuboresha tabia yetu. Nilipata ushuhuda imara kuhusu maombi na kwa kweli nikaonja upendo wa Baba kwetu sisi. Nilianza kuamini zaidi na kupunguza hofu. Tuligundua kwamba shida ambazo tulikabiliana nazo zilikuja kuwa ngazi za

kujiboresha. Leo nyumba yetu huonekana kama mbingu ndogo.

Bado tupo mwanzoni mwa safari yetu, lakini kufunga ndoa na kuanzisha familia ulikuwa uchaguzi bora zaidi ambao niliwahi kufanya. Moyo wangu unajawa na furaha wakati ninapofikiria kuhusu ibada ya hekaluni tuliyopokea na kujua ya kwamba iliunganishwa kwa Mamlaka ya Mungu. Kadiri ninavyozidi kuelewa kuhusu umuhimu wa familia katika mpango wa Baba wa Mbinguni na utukufu wa agano tuli- lofanya, ndivyo ninavyotaka kusaidia familia zingine kupokea ibada hiyo.

Nilijifunza ya kwamba hatuhitaji kuwa na wasi wasi juu ya kile kita-kacho tendeka, kwa sababu “Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo, na ya moyo wa kiasi” (2 Timotheo 1:7). Tunahitaji tu kuwa watiifu, kufuata maelekezo yaliyotolewa katika maandiko na maneno ya manabii wa siku zetu, na kuomba katika maombi maelekezo zaidi ya kibinafsi.

Ikiwa tutafanya vitu hivi, tunaweza kuvuka bahari ya hizi siku za mwisho na tukijiamini kwamba bila kujali ni aina gani ya matatizo yatatupiga, wapendwa wetu watakuwa salama. ■

Mwandishi anaishi Paraná, Brazil.



Je, Ni Jinsi Gani Naweza Kujifunza **AKILINI MWANGU** na **MOYONI MWANGU**?

Ni nini unapaswa kufanya wakati unapokuwa na swali kuhusu kitu fulani cha kima-fundisho, kihistoria, au cha kibinafsi? Ni jinsi gani utapata jibu? Bwana anaahidi, “Mimi nitakujulisha wewe akilini mwako na katika moyo wako, kwa njia ya Roho Mtakatifu” (M&M 8:2). Ni kwa namna ganii waweza kutumia akili *na* moyo wako kutambua maongozi? Hapa kuna mawazo machache.

AKILI

Jifunze, Omba, Sikiliza

Mzee Robert D. Hales wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alisema kwamba wakati tunapofanya uamuzi muhimu wa maisha Baba wa Mbinguni anatutegemea sisi kutumia haki yetu ya kujiamulia, tuichunguze hali ilivyo katika akili zetu kulingana na kanuni za injili, na kuleta uamuzi wetu Kwake katika maombi. (The Holy Ghost, *Liahona*, Mei 2016, 105).

Njia ni hyo hiyo kwa swali lo lote lile. Unaposoma, omba kwa moyo wa kweli kuhusu majibu utakayopata njiani. Roho Mtakatifu atakupa misukumo—ikiwa ni kwa fikra, au maneno akilini mwako au kumbusho nyingine za kibinafsi—ili kukuongoza hadi kwenye majibu zaidi unayohitaji.

Tumia Nyenzo

Chunguza maandiko, pamoja na Mwongozo wa Maandiko na misaada mingine ya kujifunza. Unaweza pia kuchunguza katika nyenzo nyingine za WSM kama vile hotuba za mkutano mkuu, Mada za Injili kwenye LDS.org, majarida ya Kanisa, Mradi wa Magazeti ya Joseph Smith, na zaidi. (Ona ukurasa 54 kwa orodha kutoka nyenzo za Kanisa.)

Zungumza

Usiwe na hofu katika kuomba msaada Mzee Ronald A. Rasband wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alihamasisha, Mimi ninaenda kuwapeni changamoto. Unahitaji kufikiria juu ya mtu [ambaye anaweza kukusaidia kupata majibu]—rafiki unaye mwamini, mzazi au wazazi, babu na bibi, mwalimu, uaskofu, [au] mshauri . . . —na unahitaji maswali haya yajibiwe” (Face to Face broadcast, Jan. 20, 2016). Jaribu! Zungumza na mtu unaye mwamini kuhusu maswali yako na mtafute majibu kwa pamoja.

Omba

Sikiliza

Hotuba

KIELEZO NA JOSH TALBOT

Tafuta kujua ni nini unaweza kufanya wakati ukiwa na maswali.

Jifunze

Jifunze

Omba

Sikiliza

Subira



MAJIBU KUTOKA KWA MUNGU

“Kuzungumzia maswali ya ukweli ni sehemu muhimu ya kujenga imani, na tunatumia vyote akili na hisia zetu. Bwana alisema, ‘Mimi nitakujulisha wewe akilini mwako na katika moyo wako’ [M&M 8:2]. Siyo majibu yote yatakuja mara moja, lakini maswali mengi yanaweza kuji-biwa kwa kujifunza kwa nia halisi na kutafuta majibu kutoka kwa Mungu.

Mzee Neil L. Andersen wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, “Faith Is Not by Chance, but by Choice,” *Liahona*, Nov. 2015, 66.

MOYO

Jifunze, Omba, Sikiliza

Hizi ndizo hatua muhimu za kutafakari akilini na moyoni mwako. Rais Dieter F. Uchtdorf, Mshauri wa Pili Katika Urais wa Kwanza, alisema, “Kama unataka kutambua ukweli wa kiroho, unatakiwa kutumia vifaa sahihi. Huwezi kupata uelewa wa ukweli wa kiroho na vifaa ambavyo havina uwezo wa kuugundua” (“Receiving a Testimony of Light and Truth,” *Liahona*, Nov. 2014, 22). Roho Mtakatifu ni kifaa ambacho kupitia kwacho tunajifunza mambo ya kiroho. Kwa hivyo unapo omba na kumsikiliza Roho, kwa wakati wake utaweza kupata majibu.

Kuwa Mvumilivu

Rais Uchtdorf pia alieleza, Kadiri tunavyozidi kuelekea moyo na mawazo yetu kuelekea kwa Mungu, ndivyo tunavyozidi kupewa mwanga mwingi wa mbinguni juu ya nafsi zetu. Pole pole kile mwanzo kilichoonekana kuwa na ukungu, giza, na kiko mbali kinakuwa wazi, chenye kung’aa na kilichozeleka kwetu (Receiving a Testimony of Light and Truth, 22). Kutafuta majibu inaweza kuwa mchakato mrefu. Lakini ikiwa uko radhi kusikiliza ili kupata majibu, hata ikiwa itachukua muda, utapata.

Fanya Mazoezi ya Kutambua Misukumo

Unapozidi kutambua misukumo na kuwa tayari kuchukua hatua wakati Roho anapo kunong’oneza moyoni mwako, ndivyo inavyozidi kuwa rahisi kwako kutambua misukumo zaidi katika siku zijazo. Waweza “ukahisi kuwa hiyo ni sahihi” au ukahisi “mzubao wa mawazo” ikiwa siyo sahihi (ona M&M 9:8-9). Unaweza pia kuhisi kumbusho jepesi, hisia ya amani, au hisia nyingine ambayo ni maalum kwako. Bwana anakujua, na anajua jinsi utakavyo mwelewa Roho. Atakupata mwongozo wa kiupendo ambao ni wa kipekee kwako. Kwa hivyo endelea kusikiliza na kufanya mazoezi. ■


UFANYE UJUMBE KUWA WAKO KATIKA KUJIJIFUNZA KWAKO INJILI

*Angalia dokezo hizi za
kujifunza injili na kutafuta
majibu kwa maswali
ya kiroho.*

Na Bethany Bartholomew

Majarida ya Kanisa

Ni jinsi gani unasoma wakati unapotafuta majibu ya swali la kiroho au hata unapojaribu tu kuelewa maandiko vizuri zaidi? Ninamaanisha wewe—binafsi. Kila mtu ana tabia tofauti za kujifunza kwa ajili ya shule, lakini mara nyingine sisi husahau ya kwamba tunaweza kuufanya ujumbe kuwa wetu binafsi katika kusoma kwetu injili pia. Wakati utakapokuwa na swali la kiroho au la kimafundisho, jaribu baadhi ya vidokezi hivi ili kugundua ni kipi kitakuwa bora zaidi kwako.



1. TENGENEZA

Tengeneza orodha, chati, au ramani. (Tazama mfano hapa chini.)

Tengeneza mtandao wa kusoma. Andika maneno na mawazo na kisha uyaunganishe na laini na viputo kuonyesha jinsi yanavyohusiana.



TENGENEZA ORODHA, CHATI, AU RAMANI

Mara nyingine inasaidia kupanga mawazo yako kitaswira wakati wa kusoma injili kwa kuyaweka katika orodha, chati, au ramani ya aina fulani. Huu ni mfano wa aina ya chati mtu anayoweza kutengeneza wakati anaposoma nyaraka za Paulo katika Agano Jipya. Unaweza kutengeneza orodha, chati, au ramani yako mwenyewe ukitumia muundo unaoku-faa zaidi. Kuwa Mbunifu! Tafuta njia zenye kufurahisha ili kupanga usomaji wako wa injili.

NYARAKA ZA PAULO

WARAKA	PAMOJA NA MWENZA?	ANAANDIKA KUTOKA ... ?	MADA KUU ZA WARAKA
Mfano: 1 Timotheo	Haukutajwa	Laodikia (ona dokezo mwisho wa 1 Timotheo 6)	Mafundisho ya kweli, Mwokozi, maombi, imani na hisani, sifa za uongozi, ukengeufu, kuwahudumia maskini, kubaki mwaminifu, kuepuka utajiri wa kiulimwengu

2. ANDIKA

Andika mawazo na hisia unazopata wakati unaposoma maandiko katika shajara ya kujifunzia kusoma na ufanye mapitio ya mawazo hayo mara kwa mara.

Andika chini mawazo na hisia zako baada ya maombi yako, hata kama hisia hizo hazihusiani moja kwa moja na mada unayosoma. Ona kile ambacho Roho anakufundisha baada ya muda.

Andika maswali yako katika daf-tari, kwenye simu yako, au kijitabu kilicho kando ya kitanda chako kukukumbusha na kukusaidia kuendelea kufikiria kuhusu yale unayojifunza kila siku.



3. SIKILIZA NA UJADILI

Zungumza na mzazi au kiongozi anayeaminika. Ifanyieni kazi kwa pamoja. Yaweza chukua muda mrefu, lakini nyote wawili mtakua katika mchakato huo.

Mfundishe Mtu Mwingine. Chukueni zamu kushirikiana kile mnacho fahamu. Jadilianeni kile mlichoijifunza kutoka kwa kila mmoja.

Sikilizeni maandiko au simulizi zingine na vyanzo vingine vya WSM kwa sauti.

4. UCHUNGUZI

Chunguza misaada mingine ya kujifunza iliyoko katika maandiko na kwenye mtandao (tazama hapa chini ili kupata orodha ya nyenzo za usaidizi za WSM).

Chunguza kwenye LDS.org upate video na nyimbo kuhusu unacho jifunza.

Soma muktadha. Chunguza historia au sura zinazozingira mada au maandiko unayosoma.

RUHUSU MISAADA YA KUSAIDIA KUSOMA IKUSAIDIE

Kuna vyanzo vingi vya thamani vinavyo patikana katika maandiko na mtandao ili kukusaidia wewe wakati unaposoma mada muhimu. Hii ni orodha ya baadhi ya rasilimali zinazopatikana na mahali unapo-weza kuzipata:



KATIKA MAANDIKO

- Mwongozo wa Maandiko
- Wendo katika Biblia (matukio kutoka Agano la Kale na Jipya yakiwa katika mpangilio wa wendo na tarehe ya karibu)
- Ulinganifu wa Injili (Simulizi juu ya Mwokozi kutoka katika Injili za Mathayo, Marko, Luka, na Yohana ikiwa imeandaliwa kulingana na matukio, mahali, na tarehe)
- Tafsiri ya Joseph Smith ya Biblia
- Ramani na picha
- Mwongozo wa Vifupisho



KATIKA LDS.ORG

- Maandiko (scriptures.lds.org)
- Mkutano mkuu (conference.lds.org)
- Mada za Injili (topics.lds.org)
- Majarida (liahona.lds.org)
- Historia ya Kanisa (history.lds.org)
- Misaada ya kusoma (scriptures.lds.org)
- Masomo na nyenzo za kufundishia (lds.org/go/41754a)
- Maktaba ya Habari WSM (lds.org/media-library)
- Usaidizi kwa changamoto (lds.org/go/41754b)



NYENZO NYINGINE MTANDAONI

- Historia ya Familia (familysearch.org)
- Mormon Channel (mormonchannel.org)
- Maandiko yaliyonukuliwa katika mkutano mkuu (scriptures.byu.edu)
- Mormon Newsroom (mormonnewsroom.org)
- Kazi ya umisionari na ufundishaji injili (mormon.org)
- Mradi wa Magazeti ya Joseph Smith (josephsmithpapers.org)

5. FANYA

Igizeni simulizi kutoka kwenye maandiko au nyenzo zingine. Ni jinsi gani kuvaa viatu vya mtu yule yaweza kukusaidia kuelewa vyema kile unachosoma? Ni jinsi gani hali kama hizo zingekonekana katika maisha yako?

Tengeneza mtiririko wa maandiko ambao unaunganisha majibu unayopata katika maandiko yako. (Tazama mfano hapa chini.)

TENGENEZA MTIRIRIKO WA KUSOMA MAANDIKO

Mara nyingine inasaidia kuandika maandiko kadhaa yanayo zungumzia mada zilizo sawa. Angalia katika Mwongozo wa Maandiko, maandiko yanayohusiana na mada unayo soma. Kisha tumia marejeo na muktadha ili kuunganisha na maandiko na maelezo zaidi kuhusu mada hiyo. Andika maandiko yanayofuata katika mtiririko pembeni mwa maandiko ya awali na kadhalika. Unaweza pia kutafuta hotuba za mkutano kuhusu mada maalum ikusaidie katika uchunguzi wako (ona orodha ya mada kwenye conference.lds.org). Mtiririko wa kusoma maandiko kuhusu matumaini ni mfano.

MTIRIRIKO WA KUSOMA MAANDIKO

Maandiko kuhusu matumaini:

Anza: Moroni 7:40



(Etheri 12:4).



Moroni 7:3



Mafundisho na Maagano 138:14



Moroni 7:41



Maliza: Alma 46:39 (Andika Moroni 7:40 pembeni karibu na maandiko haya.)

Hotuba kuhusu matumaini:

- Askofu Dean M. Davies, "The Blessings of Worship," Okt. 2016 mkutano mkuu.
- Mzee Paul V. Johnson, "And There Shall Be No More Death," Apr. 2016 mkutano mkuu.
- Rais Dieter F. Uchtdorf, "He Will Place You on His Shoulders and Carry You Home," Apr. 2016 mkutano mkuu.
- Mzee L. Whitney Clayton, "Choose to Believe," Apr. 2015 mkutano mkuu.
- President Boyd K. Packer (1924–2015), "The Reason for Our Hope," Okt. 2014 mkutano mkuu.
- Rais Henry B. Eyring, "A Priceless Heritage of Hope," Apr. 2014 mkutano mkuu. ■





**Na Mzee
Quentin L. Cook**
Wa Akidi ya Mitume
Kumi na Wawili

JINSI YA KUPATA AMANI YA KWELI

Matamano ya kimbingu kwa watu wema kila mahali yamekuwa na siku zote yatazidi kuwa ni uwepo wa amani duniani. Kamwe tusikate tamaa katika kutimiza lengo hili. Lakini, Rais Joseph F. Smith (1838–1918) alifundisha, Kamwe haiwezekani kuwepo duniani Roho yule wa amani na upendo hadi wanadamu watakapo pokea ukweli wa Mungu na ujumbe wa Mungu, na kuutambua uwezo na mamlaka yake ambayo ni ya kimungu.

Kwa dhati tunatumaini na kuomba kwa ajili ya amani kote duniani, lakini ni kwa watu binafsi na familia ndiko tunakoweza kupata aina hii ya amani ambayo imeahidiwa kama **zawadi ya haki**. Amani hii ni zawadi iliyo ahidiwa kutokana na huduma na dhabihu ya Mwokozi ya kulipia dhambi.

Amani sio tu usalama au kukosekana kwa vita, ukatili, migogoro, na mabishano. Amani huja kutokana na **kujua ya kwamba Mwokozi anajua sisi ni akina nani** na anajua ya kwamba sisi **tuna imani katika Yeye, tunampenda Yeye, na tunashika amri Zake**, hata na

hususani katikati ya majaribu na maafa makubwa (ona M&M 121:7–8).

Ninaweza kugeukia wapi ili nipate amani? Wapi kimbilio langu wakati vile vyanzo vingine vinakoma kunitibu? (“Where Can I Turn for Peace?” *Wimbo*, no. 129). **Jibu ni Mwokozi**, ambaye ni kiini na mwasisi wa amani. Yeye ni “Mfalme wa Amani” (Isaya 9:6).

Tukijinyenyekeza mbele ya Mungu, **tukiomba** daima, **tukitubu** dhambi zetu, tukiingia katika maji ya **ubatizo na moyo uliopondoka na roho iliyovunjika, na kuwa wafuasi wa kweli** wa Yesu Kristo ni mifano yenye maana sana ya haki ambayo huzawadiwa kwa amani ya kudumu.

Kanisa ni Mahali pa kukimbilia ambapo wafuasi wa Kristo hupata amani. Baadhi ya vijana duniani husema wao ni wa kiroho lakini sio wa kidini. Kujihisi kiroho ni hatua nzuri ya kwanza. Hata hivyo, ni Kanisani ambapo **tunashirikishwa, tunafundishwa na kulishwa neno jema** la Mungu. La muhimu zaidi, ni mamlaka ya ukuhani Kanisani ambayo inawezesha **ibada na maagano matakatifu** ambayo huunganisha familia pamoja na kufanya kila mmoja



wetu afuzu kurudi kwake Mungu Baba na Yesu Kristo katika ufalme wa selestia. Ibada hizi huleta amani kwa sababu ni maagano na Bwana.

Mahekalu ni mahali ambapo nyingi kati ya ibada hizi hufanyika na pia ni kiini cha kimbilio la amani kutoka ulimwenguni. Wale ambao **hute-mbelea viwanja vya hekalu** au wanaoshiriki katika maonyesho ya nyumba za mahekalu pia huhisi amani hii.

Yesu Kristo ndiye kiini cha amani ya kweli. “Hata pamoja na majaribu ya maisha, kwa sababu ya Upatanisho wa Mwokozi na neema Yake, maisha ya haki yatazawadiwa kwa kuwa na amani binafsi (ona Yohana 14:26–27; 16:33). ■

Kutoka katika hotuba ya mkutano mkuu wa Aprili 2013.

Vitabu Vilivyo sahaulika, Ushuhuda Unao kumbukwa

Macho yote yalinitizama. Je, ninaweza kulitetea Kanisa kwa ushuhuda wangu rahisi?

Na Abegail D. Ferrer

Mwaka mmoja, nilikuwa na lengo la kuboresha kujifunza kwangu kiroho. Ningebeba vitabu vyangu vya Kanisa, makabrasha, vitabu vya kiada, na maandiko kila mahali, ikiwa ni pamoja na shuleni, kwa maana nilipata njaa ya neno la Mungu. Lakini juhudi zangu zilipunguka wakati nilipokuwa na kazi nyingi nikijisomea kwa ajili ya mtihani uliokuwa unakaribia.

Siku moja mwalimu wetu aliongoza majadiliano ambapo aliwauliza wanafunzi wote wasio Wakatoliki chumbani mle wasimame. Nilikuwa Mtakatifu wa Siku za Mwisho pekee yangu mle darasani. Wanafunzi wengine sita walisimama.

Kisha tukaulizwa: Nyinyi ni waumini wa kanisa gani? Ni nani alikuwa mwanzilishi wake? Kanisa lenu lilianzishwaje?

Nilikuwa wa mwisho kujibu. Nilikuwa na wasiwasi nilipogundua sikuwa nimebeba vitabu vyangu vya Kanisa, lakini nilijaribu kukumbuka yale niliyokuwa nimejifunza. Kifungu cha maandiko kilinjia akilini:

Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe.

“Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako” (Mithali 3:5–6).

Nilisimama darasani kwa ujasiri na kusahau hofu yangu. Nilisema kwamba mimi nilikuwa muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Nilisimulia simulizi ya mvulana mdogo, Joseph Smith, ambaye alimwona Mungu. Nilihisi moyo wangu ukiwaka, machozi yalinitoka machoni. Nieleza ya kwamba Kanisa lilianzishwa mnamo Aprili 6, 1830, na nilishuhudia ya kwamba nabii wa Mungu alikuwa ameitwa na ukuhani kurejeshwa. Nilishuhudia ya kwamba nilijua kwamba yote haya yalikuwa ya kweli.

Muda huu mrefu wa kusoma injili ulikuwa na thamani yake. Ulikuwa umeniwezesha kutetea imani yangu na kushirikiana na wengine injili. Nili-ona fahari wakati, wiki kadhaa baadaye, wanne kati ya marafiki zangu walijiunga nami kanisani.

Tukio hilo lilinifundisha umuhimu wa ushuhuda. Mara ya kwanza niliwa-za kwa nini Bwana hakuwa amenitia msukumo nibebe vitabu vyangu siku hiyo. Vingenisaidia kikamilifu kujibu maswali yaliyokuwa yakiulizwa. Lakini niligundua kwamba hatuhitaji kukariri kila kitu kuhusu Kanisa au kutegemea dondoo—tunapaswa kusoma, kuishi, na kushirikiana na wengine injili, tukimtegemea Roho Mtakatifu. Sikuwa na vitabu vyangu, lakini nilikuwa na ushuhuda wangu. ■

Mwandishi anaishi Cagayan, Ufilipino.



W A O WALIMWONA

Watu hawa kwa kweli walimwona Mwokozi mfufuka, lakini hata wewe pia unaweza kuwa shahidi wa Kristo kwa njia yako mwenyewe.

U nafikiria ingekuwaje kumshuhudia Mwokozi mfufuka? Kwani mamia ya watu katika wakati wa Yesu, hawakuhitaji kufikiria—waliuishi. Maandiko yanasimulia kwa kiasi kidogo mifano ipatayo dazani moja iliyoandikwa katika Agano Jipya na mara kadhaa katika Kitabu cha Mormoni wakati Bwana mfufuka alipowatokea watu. Watu hawa binafsi walishuhudia moja ya miujiza mikubwa zaidi katika historia: Yesu Kristo akishinda mauti na kumwezesha kila mmoja wetu kuishi tena. Makubwa yasiosadikika, sawa?

Basi inamaanisha nini haswa kuwa shahidi wa Kristo? Wacha tupeleleze chache ya nyakati hizi katika maandiko na kufikiri jinsi sisi, hata bila ya kumwona kimwili, tunavyoweza pia kuwa mashahidi wa Kristo.

Mariamumagdalena

Mariamumagdalena alikuwa shahidi wa kwanza. Asubuhi ya Jumapili baada ya Kusulibiwa Kwake, yeye alikuja kwenye kaburi la mawe na wanawake wachache wengine ili kuupaka mafuta mwili wa Bwana. Wakati Maria alipogundua kaburi liko tupu, alilia. Mtu mmoja alimwendea kutoka nyuma na kumwuliza, “Mama, unalilia nini?” Fikiria mshangao wake wakati alipogundua kwamba alikuwa Yesu, aliyefufuka kutoka kwa wafu. (ona Yohana 20:1–18.)



PENNANT © ISTOCK/GETTY IMAGES

Wanafunzi wawili wakiwa njiani kwenda Emau

Cleopa na mwanafunzi mwingine walikuwa wanate-mbea barabarani kwenda Emau wakati mgeni alipojiunga nao. Wao hawakumtambua mwenza wao mpya, lakini wakati wa mlo wa jioni pamoja, mgeni yule aliumega mkate. Mara macho yao yakafumbuliwa, na wakamta-mbua kwamba wamekuwa wanasafiri na Mwokozi wakati wote. “Je mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?” waliulizana wao kwa wao, wakitafakari uthibitisho ule kwamba walihisi kana kwamba kweli Yeye alikuwa pamoja nao. (Ona Luka 24:13-34.)



Wale Mitume Kumi


Wanafunzi wawili waliosafiri kwenda Emau na Kristo walirudi Yeruslemu na kuwaambia Mitume kumi kati yao kuhusu tukio lao. Wakati walipokuwa wanazungumza, Mwokozi Mwenyewe aliwatokea, akisema, “Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo.” (Ona Luka 24:36-41, 44-49.)

Mtume Tomaso

Mtume Tomaso hakuwepo wakati Mwokozi alipowatokea mara ya kwanza Mitume, kwa hiyo hakuamini kwamba Kristo amefufuka. Wiki moja baadaye, Kristo tena aliwatokea Mitume. Wakati huu Tomaso *alikuwa* pale, na kwa sababu alimwona Kristo, aliamini kwamba amefufuka. Mwokozi alimwonya Tomaso dhidi ya kuamini baada ya kuona tu: “Kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki” (Ona Yohana 20:24-29.)



MCHORO WA THOMAS NA BRIAN CALL



Mitume Kumi na Mmoja Kwenye Bahari ya Tiberia

Siku moja sio muda mrefu baada ya kufufuka, Mitume kadhaa walikwenda kuvua samaki katika bahari ya Tiberia lakini hawakuwa na bahati nzuri. Asubuhi iliyofuata, Bwana aliwatokea na kuwashauri kutupa nyavu upande wa kulia wa boti. Walipofanya hivyo, wavu ulinasa samaki wengi sana kiasi kwamba walishindwa kuvuta! Baada ya kufurahia pamoja, Mwokozi aliwafundisha kuhusu umuhimu wa kuwahudumia wengine, akisema, “Lisha Kondoo Wangu.” Mitume walitumia muda uliosalia wa maisha yao yote wakifanya hayo tu—kuwafundisha watu kuhusu Kristo—na katika baadhi ya kadhia, walitoa hata uhai wao kwa ajili hii. (Ona Yohana 21:1-22.)

KRISTO MFIJUKA KWENYE BAHARI YA TIBERIA NA DAVID LINDSLEY





MCHUNGUJI MMOJA, NA HOWARD LYON


Wanefi katika Amerika

Wakati wa kusulubiwa, ardhi katika mabara ya Amerika iliharibiwa kwa tetemeko la nchi, moto, maafa mengine ya asili, na siku tatu za giza ili kuashiria kifo cha Mwokozi. Baadaye, Kristo aliteremka kutoka mbinguni na kuutembelea umati wa watu 2,600 uliokusanyika karibu na hekalu huko Bountiful. Aliwaalika watu kugusa makovu katika mikono Yake na miguuni na ubavuni, alitoa mahubiri, na kuwabariki watoto wa Wanefi mmoja mmoja. Hata watu zaidi walikusanyika siku iliyofuata, na Mwokozi aliwatembelea na aliwafundisha. Wanafunzi hatimaye walianzisha Kanisa la Kristo, na Wanefi walipokea ushuhuda wenye nguvu kama huu kwamba wao na Walamani pia waliongolewa kwa Bwana. (Ona 3 Nefi 11-18; ona pia 3 Nefi 8-10; 4 Nefi 1.)

Mashahidi Wakati ule na Sasa

Kristo pia aliwatokea wengine wengi, pamoja na wanawake kadhaa waliokuja kwenye kaburi la mawe ili kumsaidia Mariamu Magdalena kuupaka mafuta mwili wa Kristo, kundi la zaidi ya wanaume 500, Yakobo na Paulo. (Ona Mathayo 28:9; Matendo ya Mitume 9:4-19; 1 Wakorintho 15:6-7; ona pia 3 Nefi 19; 26:13.)

Yawezekana tusiwe na nafasi ya kumwona Mwokozi kama mashahidi hawa walivyoweza, lakini wewe bado unaweza kuwa shahidi wa Kristo. Unaweza wewe binafsi kumtafuta Kristo, kama Mariamu alivyofanya alipokwenda kaburini, kwa kujifunza zaidi kuhusu Yeye. Au unaweza kutumia imani yako kwake Yeye kwa kutii amri na kufuata ushauri wa manabii. Au ungeweza kutambua baraka za Mwokozi katika maisha yako, kama wanafunzi wale wawili wakitembea kwenda Emau wali-vyofanya. Majira haya ya Pasaka, fikiria kuhusu nini inamaanisha kuwa shahidi wa Kristo. Watu hawa walikuwa mashahidi halisi ambao kwa kweli walimwona Kristo mfufuka—lakini hiyo sio njia pekee unayoweza kumshuhudia Yeye katika maisha yako. ■



JIFUNZE KUTOKA KWAKE

“Unaposikia ushuhuda wa Roho Mtakatifu juu ya [Kristo], ukithibitishwa na kurudiwa rohoni mwako katika matukio mengi tofauti na hali tofauti tofauti, kadiri unavyojitahidi kushikilia nuru ya mfano Wake katika maisha yako siku hadi siku, na kadiri unavyotoa ushuhuda wako kwa wengine na kuwasaidia kujifunza juu Yake na kumfuata Yeye, wewe ni shahidi wa Yesu Kristo,”

Mzee D. Todd Christofferson wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, “Kuwa shahidi wa Kristo,” *Liahona*, Mar. 2008, 63.

NAFASI YETU

MUNGU HUTUPA SISI ZANA

Mjomba wangu ni msanii na anatengeneza meli ndogo ndogo za mbao katika chupa za kioo. “Inachukua muda mrefu, umakini, na juhudi kuzitengeneza.

Siku moja niliona zana zake zote na kuona jinsi kila zana inavyotumika kwa kazi maalumu au kunakshi juu ya meli. Nilipo mwangalia akifanya kazi, nilishangazwa kwa jinsi alivyotumia zana hizo ili kutengeneza meli hizi. Nilikumbushwa hadithi ya Nefi akijenga meli (ona 1 Nefi 17–18). Alijenga kulingana na njia ya Bwana, sio njia ya binadamu. Mungu hutupa zana ili kujenga meli zetu wenyewe kwa njia Yake. Maandiko, imani, na upendo wa Mungu ni zana ambazo lazima nizitumie katika maisha yangu mwenyewe ili kwa uangalifu nijenge meli yangu mwenyewe pasipo kuweka nyufa. Najifunza kila siku kuwa mwanafunzi wa Bwana. ■

Maria Mercedes G. Monagas, Venezuela



KUJISIKIA MPWEKE

Ilikuwa majira ya a kuchipua ya baridi nchini Denmark. Ndio kwanza nimeanza umisionari, na ushuhuda wangu ulikuwa wa kuhangaika sana. Nilikuwa mwongofu wa miezi 19 tu na mwenye mashaka kuhusu kukabiliana na nchi ngeni, lugha nisyoweza kuisema, na mzingile wa mitaa nisyoweza kuelewa jinsi ya kujiongoza. Maombi yangu ya mwanzo yaliyojaa shukrani mara yakawa mashitaka makali: “Mungu, kwa nini umeniacha mpweke?”

Asubuhi moja nilimsihii Yeye katika maombi. Lakini badala ya kumuuliza “kwa nini” huku nikiwa na hasira

katika moyo wangu, niliomba ushahidi wa ukweli wa injili na ukomeshaji wa mashaka yangu.

Baada ya kuomba, nilifunua maandiko yangu. Nilitua kwenye Kumbu kumbu la Torati 31:6: “Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana Bwana, Mungu wako, yeye ndie anayekwenda pamoja nawe hatakupungukia wala kukuacha.”

Roho yangu ilijaa furaha nilipotambua jibu kwa maombi yangu: Mungu amekuwa pale wakati wote. Alikuwa tu anangojea maombi yangu ya dhati kuliko mashitaka ya kuachwa.

Mungu kamwe hataniacha, hata wakati mambo yote yanaonekana hayafai. Na tunaweza kuhisi mwanga Wake wa jua kwa njia ya maombi na maandiko Yake. ■

Clayton E. Texas, Merokani

NI ZAMU YAKO

Liahona Linakaribisha uzoefu wako na maoni yako katika kuishi injili. Peleka hadithi yako kwa liahona@ldschurch.org au barua pepe kwenda liahona@ldschurch.org. Tafadhali weka jina lako kamili, kata, na kigingi, na ruhusa ya wazazi.

SONGA MBELE

ASKARI WA KIKRISTO

“Waume na wake wanaotamani kupata makao katika ufalme wa Selestia, watagundua kwamba ni lazima wapambane kila siku.”

(Teachings of Presidents of the Church: Brigham Young [1997], 294).



“Ninawezaje kujua kama Mungu anasikiliza maombi yangu?”

Maombi ni baraka kubwa, na tumeahidiwa kwa mba Baba wa Mbinguni kila mara anasikiliza, lakini mara nyingi inakuwa kazi kutambua majibu Yake.¹

Fikiria juu ya hili: ama Mungu anakusikiliza wewe au Hakusikilizi. Kama hakusikilizi, hivyo basi hakuna sababu ya kuomba. Lakini kama ndiyo (na Anafanya!), inabidi tuelewe ni jinsi gani *hakika* tunawasiliana Naye kwa maombi, tambua majibu, na kwa uaminifu songa mbele.

Tunapohisi Yeye hasikilizi, huenda sisi tunahitaji uzoefu wa kukua binafsi. Unaweza kujiuliza wewe mwenyewe maswali machache: Je, mimi ni msafi? Je, malengo yangu ni yenye kustahili? Je, niko tayari kutenda yale anayoniambia?² Kama jibu kwa kila swali ni ndio, unaweza kuamini kwamba “Bwana Mungu wako . . . atakupaja majibu ya maombi yako” (M&M 112:10). Kumbuka, wakati mwingine majibu huja katika njia ya kutatiza au isiyo tarajiwa.

Kama ulijibiwa hapana kwa baadhi ya yale maswali, bado hujachelewa! Fanya masahihisho ya lazima katika maisha yako ili uweze kuwa na Roho. Kubali kufuata miongozo unayopokea.

Na usisahau kwamba kila mtu anapokea majibu kwa njia tofauti. Omba kwamba Roho Mtakatifu akufundishe wewe jinsi *wewe* unavyoweza kutambua majibu. Huenda isiwe rahisi kuyatambua kwa mara ya kwanza, lakini ni sawa na ujuzi mwingine: mazoezi hufanya mazoea. Kuwa na imani na amini kwamba Baba wa Mbinguni ana *sikiliza* wakati wote.

MUHTASARI

1. Ona Mathayo 7:7; Yakobo 1:5–6; Alma 33:4–11; Mafundisho na Maagano 8:1–2.
2. Tazama Richard G. Scott, “Learning to Recognize Answers to Prayer,” *Ensign*, Nov. 1989, 32.



Msikilize Roho

Jaribu kumsikiliza Roho Mtakatifu. Watu humsikiliza Roho Mtakatifu kwa njia

tofauti, hivyo huenda unasikiliza sauti, ndogo tulivu wakati yawezekana mwongozo unakuja kama hisia. Ninajua kwamba Roho Mtakatifu atakuambia wewe yale yote unayohitaji kujua—unatakiwa kusikiliza tu.

Elise G., umri miaka 13, Alberta, Canada

Majibu katika Kanisa

Mara moja nilipata kuwa na wasiwasiki mkubwa kuhusu kwenda miadi pamoja na mtu asiye muumini. Jumapili moja katika kipindi cha sakramenti, dada mmoja alitoa hotuba ambayo ilionekana kunilenga mimi moja kwa moja. Kwa wakati huo, nilipokea uhakikisho kwamba Bwana amejibu maombi yangu. Kabla, nilikuwa nimechanganyikiwa kuhusu nini nifanye, lakini wakati huo nikafarijiwa na Roho Mtakatifu, ambaye aliujaza moyo wangu kwa furaha na ujasiri. Mungu anatumia sisi kupitia hisia, mawazo, maandiko, na hata wazungumzaji kanisani!

Karen V., umri miaka 19, Minas Gerais, Brazil

Tafuta

Wakati fulani nilijiuliza kama Mungu angeweza kusikia maombi yangu, na kisha nikahisi jibu katika moyo wangu. Nilimsikia mtu akitoa ushuhuda kuhusu maombi, nami nilihisi Roho Mtakatifu. Ushauri wangu mwingine utakuwa ni kuwauliza wazazi wako, askofu, au waumini wengine wa kata yako. Unaweza hata kuomba kwa ajili ya msaada kwenye mada hii!

Joshua S., miaka 13, Oregon, USA



Kumbuka Wewe Ni Nani

Ninajua Mungu anatusikiliza sisi kwa sababu maombi hutoa hisia za

amani, faraja, na upendo katika moyo wangu. Ninaona kwamba Yeye ameniepusha na hatari nyingi siku hadi siku kwamba anailinda familia yangu, na nahisi kupendwa na Yeye. Kabla sijaenda shuleni, mara nyingi ninasema kauli mbiu ya Wasichana; inanisa- idia mimi kukumbuka kwamba mimi ni binti wa Baba wa Mbinguni, ambaye ananipenda.

Nicol M., umri miaka 19, Lima, Peru

Mwamini Yeye

Baba wa Mbinguni mara zote anayasikiliza maombi yetu, lakini wakati mwingine inaonekana kama hajibu maombi yetu kwa sababu huenda asijibu jinsi au wakati tunamtaka Yeye ajibu. Tunahitaji kuwa tayari kuyaweka mapenzi yetu Kwake na kuwa na imani kwamba Yeye anajua kilnacho- tufaa sisi. Baba wa Mbinguni anatupe- nda na mara zote anajaribu kutusaidia kujifunza na kukua akiwa anajibu maombi yetu.

Mosia M., miaka 17, Utah, Marekani

Ombeni Nanyi Mtapewa

Kupitia maandiko, tunafundishwa kwamba Mungu wakati wote atayasikia maombi yetu na atayajibu kama tunawasiliana Naye kwa imani na kwa nia ya dhati. Katika mioyo yetu tutahisi uthibitisho kwamba Yeye anatusikia, hisia za amani na tulivu. Pia tunaweza kuhisi kwamba kila kitu kitakuwa sawa kama tunafuata mapenzi ya Baba. Kama tunatia shaka kwamba Yeye anatusikia sisi, tunahitaji kutafuta

mwongozo katika maandiko na kisha tunaomba kujua kama mambo yale tunayosoma ni ya kweli.

Constanza L., umri miaka 20, Bío Bío, Chile



Maombi ya Mtoto

Ninajua Baba wa Mbinguni anayasikia maombi yangu kwa sababu ya maneno haya

katika wimbo wa Watoto "A Child's Prayer" (*katika Kitabu cha Nyimbo za Watoto*, 12): "Heavenly Father, are you really there? Na je unasikia na kujibu kila ombi la mtoto? Baadhi wanasema kwamba mbingu ipo mbali, lakini nahisi iko karibu nami wakati ninapoomba." Wakati ninapoukumbuka wimbo huo, ninajua Yeye anasikiliza kwa sababu ninamhisi Roho Mtakatifu na upendo Wake usio na mwisho kwangu. Ninapokumbuka kwamba Yeye ananipenda, ninaona faraja na kujua kwamba anayasikia maombi yangu.

Elaine B., umri miaka 16, Carolina Kaskazini, Marekani

Omba kwa Uaminifu

Baada ya maombi yako, unaweza kusikiliza hisia na dhamira ambayo inakuja kwenye moyo wako. Moja



USIKATE TAMAA

Kuwa mtiifu, kumbuka nyakati ambazo ume- msikiai Roho

Mtakatifu wakati uliopita, na omba kwa imani. Jibu lako litakuja, na utauona upendo na amani ya Mwokozi. Huenda lisije haraka au jinsi unavyotaka, lakini jibu litakuja. Usikate tamaa!

Mzee James B. Martino wa Sabini, "Turn to Him and Answers Will Come," Liahona, Nov. 2015, 59.

wapo linaweza kuwa jibu la maombi yako. Wakati tunapomba kwa dhati na moyo wa uaminifu, Baba yetu wa Mbinguni anajibu kulingana na imani tuliyo nayo Kwake. Hajibu tu kwa ajili ya kuridhisha udadisi wetu.

Jean-Claude N., miaka 16, Kasai-Kati, Jamhuri ya Kidemocrasia ya Kongo

SWALI LINALOKUJA

"Ni jinsi gani naweza kuwaambia rafiki zangu tusiongee bila heshima au yasiyofaa kuhusu watu wengine?"

Wasilisha majibu yako, na ukipenda, picha ya ubora wa hali ya juu kabla ya Mei 15, 2017, katika lahona.lds.org (bofya "Submit an Article") au kwa barua pepe kwenda lahona@ldschurch.org.

Tafadhali jumuisha taarifa ifuatayo: (1) jina kamili, (2) tarehe ya kuzaliwa, (3) kata au tawi, (4) kigingi au wilaya, (5) ruhusa yako iliyoandikwa, na kama u chini ya miaka 18, ruhusa iliyoandikwa na mzazi wako (barua pepe inakubalika) ili kuchapisha majibu yako na picha.

Majibu yanaweza kuhaririwa kwa ajili ya urefu au ufafanuzi.

Na Julie C. Donaldson

Inatokana na hadithi ya kweli

“I’ll try to repent, to do better, to pray”

(Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 98).

Uanafikiri wewe ni bora zaidi kuliko mtu mwingine ye yote kwa sababu wewe huapi, Nikolai alisema wakati wa mapumziko.

“Hiyo siyo kweli,” alisema Andrea.

“Kwa hiyo kwa nini husemi neno moja la kupa? Moja tuu? Halitakuua. Kila mtu anaapa.”

Andrea alipandisha mabega. “Sitaki tuu kufanya hivyo.”

Andrea alijua kuapa kulikuwa ni makosa na kunamfanya Roho Mtakatifu aondoke. Andrea alimtaka Roho Mtakatifu awe pamoja naye. Kwa hiyo hakuapa.

Andrea alikuwa mgeni shuleni, na kwa kadri ilivyokuwa, Nikolai alikuwa mtu pekee katika darasa lake la sita aliyetaka kuwa rafiki yake. Lakini Nikolai alimsumbua kuhusu kuapa kila siku ipitayo. Na kila siku Andrea alikuwa anachoka zaidi kusema hapana. Aidha, Andrea aliogopa kwamba Nikolai angeacha kuwa rafiki yake, na kisha kwa kweli atakuwa mpweke.

“Sema tuu neno moja la kupa,” Nikolai alisema

Andrea na Neno Baya

baada ya shule. “Kisha nitakuacha sitakusumbua tena.”

Mwishowe Andrea alichoka sana kusumbuliwa kwamba aseme neno moja la kipa—moja ambalo halikuwa *baya* sana.

Nikolai alikubali kwa kichwa. “Vizuri, sasa wewe ni mmoja wetu.”

Baada ya hapo, marafiki wengine wa Nikolai walizungumza na Andrea pia. Wali-kula chakula cha mchana pamoja naye na walicheza mpira wa miguu pamoja naye wakati wa mapumziko. Lakini kuwa



katika kundi la marafiki wa Nikolai ilikuwa kama kute-mbea kwenye tetemeko la ardhi. Kadiri Andrea alivyozidi kuishi pamoja nao, ndivyo alivyozungumza zaidi na kufanya kama wao. Na wote waliapa. Sana. Walichekana na kutukanana. Walisema mambo yasiyo na adabu kuhusu walimu wao. Walishikwa na wazimu na kufanya mambo mengi ya aibu. Pole pole Andrea alianza kusikia hasira mara kwa mara na kupata zaidi na zaidi sababu za kuapa.

Siku moja usiku wakati mama na baba wametoka, Andrea na dada yake mkubwa Katya walianza kubishana kuhusu maonesho gani ya kuangalia. Kabla Andrei bado hajafikiria kuhusu hilo, neno la kiapo liliruka mdomoni mwake.

Katya aliangalia kwa mshangao. “Ninamwambia Mama.”

Andrea alikimbilia kwenye chumba chake cha kulala na kufunga mlango kwa nguvu. Kosa lilikuwa nini kwa kila mmoja? Kwa nini wao walikuwa wanamfaya yeye kuwa mwenda wazimu wakati wote? Wazazi wake waliporudi nyumbani, Andrea alifungua mlango wake kidogo na kumsikia Katya akisema, “Mama, Andrea aliniapia.”

“Nini?” Mama alisikika kuwa ameshangazwa. “Andrea kamwe hawezi kuapa.”

Andrea alifunga mlango na kujibwaga kwenye kitanda chake. Alijifikiria jinsi alivyokuwa tofauti tangu alipoanza kuapa. Imekuwa ni muda mrefu tangu alipojisikia kuwa alikuwa na Roho Mtakatifu.

Andrea alipiga magoti pembeni mwa kitanda chake na kuomba. “Mpendwa Baba wa Mbinguni, nasikitika nimekuwa ovyo na mwenye hasira. Ninasikitika nilianza kuapa. Ninakwenda kufanya vizuri zaidi.”

Wakati Andrea alipokuwa anaomba, hisia nzuri zilijaza moyo wake. Kwa mara ya kwanza tangu alipoanza kuapa, alisika furaha ya kweli. Alijua Mungu alimpenda, na aliweza kumhisi Roho Mtakatifu. Alijisikia kusamehewa na alijua angeweza kubadilika na kuwa mwema zaidi.

Baada ya maombi yake, alimwambia Mama ukweli na alimwomba radhi Katya. Andrei alijisikia vizuri zaidi baada ya hapo. Nilijisikia vizuri kutubu.



Siku ya pili shuleni, Andrea hakula chakula cha mchana pamoja na kundi la Nikolai. Badala yake alikaa karibu na baadhi ya watoto asiowajua. Itachukua muda, lakini Andrea alijua atawapata marafiki waliokuwa wazuri na wenye furaha na wasioapa. Kama vile yeye. ■

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.



CHANGAMOTO YA CTR

“Nitatumia majina ya Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo kwa heshima. Sitaapa au kutumia maneno machafu” (My Gospel Standards).

Upande mmoja wa karatasi, andika au chora jinsi maneno mazuri yanavyo kufanya ujisikie. Upande mwingine, andika au chora jinsi maneno machafu yanavyo kufanya ujisikie.

Soma Walawi 19:12. Kwa nini ni muhihi kutumia majina ya Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo kwa heshima?

Muulize mzazi au kiongozi kwa nini tunapaswa kutumia lugha nzuri na jinsi jambo hilo lilivyo wabariki wao.

Ninajipa changamoto ya. . .





Na Mzee
David A. Bednar

Wa Akidi ya
Mitume Kumi
na Wawili

Ninawezaje kuisaidia familia yangu kuwa imara?



Waambie familia yako kuwa unawapenda na onyesha kwa vitendo.



Toa ushuhuda wako juu ya mambo unayojua kuwa ni ya kweli kwa njia ya Roho Mtakatifu. Shirikiana ushuhuda wako na wale unao wapenda zaidi.



Kwa hiari yako ungana na wana familia yako katika maombi ya familia na katika kujifunza maandiko. Jishughulishe katika jioni ya familia nyumbani na ifanye kuwa ya kupendeza.



Kuwa mwaminifu katika kujifunza, kuishi, na kuipenda injili ya urejesho ya Yesu Kristo.



Na Joy D. Jones

Rais Mkuu wa
Watoto

Jiandae kwa ajili ya HEKALU Kila Siku

Nilipokuwa na umri wa miaka tisa, nilikuwa na mwalimu mzuri sana wa Watoto aitwaye Dada Kohler. Nilikuwa na aibu sana, na alikuwa mpole sana kiasi kwamba nilipenda kuwa pamoja naye. Siku moja alimpa kila mmoja wetu kipande cha karatasi. Sisi wote tuliandika kile tulichotaka kufanya tutakapokuwa wakubwa. Niliandika: “Kwenda chuoni na kufunga ndoa hekaluni.” Nilibandika karatasi yangu juu ya mlango wa kabati. Nyakati za usiku, mwanga kutoka taa za mtaani ulimulika kupitia dirisha langu. Niliangalia juu kwenye kipande changu cha karatasi. Kilinikumbusha mimi kwamba nilitaka kwenda hekaluni.

Wakati huo, palikuwa na mahekalu 12 tu ulimwengu-ni. Nilitaka kwenda kwenye kila moja ya hayo.

Wakati wo wote mama na baba yangu walipopanga mapumziko, kila mara waliichukua familia yetu hekaluni. Tuliishi Oregon, Marekani. Hekalu la kari-bu lilikuwa maili 600 (965 km) mbali huko Cardston, Alberta, Canada. Gari letu halikuwa na kiyoyoyi. Kaka, dada yangu na mimi tulikaa katika kiti cha nyuma. Tulining'iniza kitambaa nje ya mlango wa gari. Kisha tunakiweka katika shingo zetu ili kujipoza.

Ulikuwa ni msisimko wakati tulipoliona hekalu. Sikujua sana kuhusu nini kilifanyika humo, lakini wazazi wangu kila mara walikuwa na furaha walipotoka nje. Nilijua hekalu lilikuwa muhimu sana. Nilijua ilikuwa ni nyumba ya Bwana. (Katika picha, mimi ni huyo niliyevaa shati jeupe.)



Baada ya kufikisha miaka 12, niliweza kufanya ubatizo hekaluni katika mahekalu kadha wa kadha. Kisha nilipokutana na mume wangu mtarajiwa, niligundua kwamba alilipenda hekalu pia! Tulioana katika Hekalu la Manti Utah.

Unaweza kujianda kwa ajili ya hekalu kila siku. Nenda hekaluni wakati uwezapo. Gusa kuta zake. Wakati mjukuu wangu Jarret alipokuwa na umri wa miaka 11, alifanya kazi ya historia ya familia kila Jumapili pamoja na baba yake. Alipata majina mengi ya mababu. Sasa kwamba ana umri wa miaka 12, anafanya ubatizo humo hekaluni kwa ajili ya mababu hao!

Wakati ukiwa hekaluni, unaweza kutembea mahali Yesu anapotembea. Ni nyumba Yake. Nina tumaini utaomba kila siku kwa Baba wa Mbinguni ili akusaidie kujiandaa kuingia hekaluni na kuhisi upendo Wake. ■

Star Anang'ara

Na Jane McBride

Imetokana na tukio halisi

"It's nice to be here with you in Primary"

(Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 254).

Star alivuta nguo zake. Bado Salijisikia vibaya kuvaa gauni kwenda kanisani. Katika kanisa lake la zamani, wasichana walivaa suruali au kaptula siku ya Jumapili. Lakini sio katika kanisa lake jipya. Yeye na mama yake walikuwa wamebatizwa tu katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Star alivuta pumzi alipojitazama katika kioo. Alikuwa na msisimko wa kwenda kanisani mara ya kwanza kama muumini rasmi, lakini pia alikuwa na wasi wasi. Mwanzoni, alishinda na mamake muda wote kanisani. Lakini wakati huu alikuwa anaenda kwenye darasa la Watoto wa Msingi.

Star alipepesa macho kwa kivuli chake kwenye kioo. Itakuwaje kama hatapatana na wengine? Vipi kama



watoto wengine hawangempenda?

"Star? Je uko tayari?" Mama alimwita.

Star alishuka ngazi "Je, naonekana vizuri?" aliuliza.

Mama alitabasamu. "Unaonekana mrembo."

Star alifanya uso. "Unapaswa kusema hivyo. Wewe ni mama yangu."

"Unasema kweli.

Ninastahili kusema hivyo. Kwa sababu ni ukweli."

Star alionyesha tabasamu dogo. Mama daima alikuwa na njia ya kumfanya ajihisi vyema. Lakini bado alikuwa anaogopa sana. Vipi kama hakukuwa na mtoto kati ya hao wengine aliyetaka kuzungumza naye? Alikuwa na marafiki shuleni lakini hawakuwa waumini wa kanisa lake jipya. Alitamani hata angalau angekuwa na rafiki hata mmoja wa kwenda pamoja naye kanisani.

"Nimekumbuka tu sasa hivi kitu fulani ninastahili kufanya," alimweleza mama yake.

Alikimbia juu akipanda ngazi na kupiga magoti kando ya kitanda chake. "Baba wa Mbinguni mpendwa,

tafadhali nisaidie nipate marafiki. Ninaamini yale wamisionari waliyonifundisha ni ya kweli, lakini mimi naogopa.”

Star alibaki amepiga magoti na kusikiliza. Baada ya muda alipata hisia tamu, yenye amani, na hakuwa na wasiwasi sana tena.

Kanisani Star na mama yake waliketi pamoja na familia iliyokuwa na wasichana watatu wadogo. Wazazi walijitambulisha na wakaanza kuzungumza na mama kabla ya mkutano kuanza. Star aliwasaidia wasichana wale kupaka rangi picha ya Yesu.

Askofu Andrews alielekea mahali walikokuwa. “Dada Cunningham! Star! Ni vyema kuwaona leo.” Aliwapa kila mmoja wao tabasamu zuri na kuwasalimia kwa mkono. Star alikuwa amesahau jinsi kila mtu kanisani alivyokuwa mzuri. Pengine atapata rafiki.

Baada ya mkutano wa sakramenti Star alienda kwenye darasa la Watoto wa Msingi. Aliwatazama wale watoto wengine akiwa na wasiwasi alipokuwa akiketi chini. Walikuwa wakizungumza wao kwa wao na walionekana kana kwamba hakuna aliyeonekana kumtambua. Moyo wa Star uliinama. Hata hivyo yeye atakuwa peke yake.

Mara msichana wa rika yake Star aliingia katika chumba hicho. “Anaonekana mwenye wasi wasi pia,” Star aliwaza. “Ninaweza kwenda kuzungumza naye.”

Star alivuta pumzi nzito, kisha akamkaribia yule msichana mgeni. “Mambo, jina langu ni Star. Mimi ni mgeni. Je ungependa kuketi na mimi?” Star aliishika pumzi yake. Je, msichana huyo angetaka kuwa rafiki yake?



Mdomo wa msichana huyo uliinuka kwa nusu tabasamu.

“Mimi ni Sara. Mimi ni mgeni pia. Familia yangu imehamia tu hapa kutoka Ontario.”

“Mama yangu na mimi tulibatizwa wiki mbili zilizopita,” Star alisema. “Sina uhakika na ninacho hitajika kufanya.”

Tabasamu la Sara lilizidi kuwa kubwa. “Tutajua la kufanya pamoja.”

Star na Sara waliketi na wenzao darasani. Mara nyingine Star alimtazama machoni Sara na kutabasamu. Sara alitabasamu pia. Star alijisikia mtulivu na mwenye furaha. Alijua kwamba Baba wa Mbinguni alikuwa amejibu ombi lake na kumsaidia kupata rafiki.

Darasani mwalimu

aliwataka Star na Sara wajitambulisha.

Star alisimama. “Jina langu ni Star Cunningham. Mama yangu nami tulibatizwa wiki mbili zilizopita.” Alipozi kidogo, na tabasamu likakua usoni mwake akimtazama rafiki yake mgeni. “Na huyu ni rafiki yangu Sara.” ■

Mwandishi anaishi huko Colorado, Marekani.

FIKIRIA KUHUSU HILO

Je, unawezaje kumkaribisha mtu mgeni Kanisani?

Kuwa Nuru

Na Elizabeth Pinborough

Upendo

Usisengenyeye

Samehe

Usaidizi

Kuhamasisha

Alika

Sikiliza

Kuweni Marafiki


“Inueni juu nuru yenu ili ing’are ulimwenguni. Tazama Mimi ni mwangaza ambao mtainua” (3 Nefi 18:24).

Tunaweza kuwa nuru kwa wengine kwa kuwa rafiki wa kweli. Soma mawazo yaliyoko hapo chini na ongeza baadhi ya kwako mwenyewe. Kila wakati unapoandika jina la mtu fulani unaetaka kumwonyesha upendo, weka rangi zaidi kama ya jua.

- Wapende wengine:** Unaweza kufanya mabadiliko makubwa katika maisha yao! Kristo ana wapenda wao, kwa hiyo jaribu kuwaonesha upendo huo.
Nani: _____
- Samehe:** Kama mtu fulani anakuumiza, jaribu kuona mambo kutoka kwenye mtazamo wao. Unaweza kuwasaidia wengine mioyo yao kulainika kama utasamehe.
Nani: _____
- Watie moyo:** Wasifie marafiki zako juu ya nguvu zao. Ona mazuri ndani yao hata kama wanahitaji kujiboresha. Kuwa kwako katika hali mzuri kunawasaidia pia!
Nani: _____
- Msikilize Roho Mtakatifu:** Maneno yako yanaweza kubadili hali mbaya kuwa mzuri. Roho Mtakatifu anaweza kukusaidia kujua nini cha kusema na jinsi ya kuonesha ukarimu.
Nani: _____
- Kamwe usisengenyeye:** Maneno mabaya yanaweza kuumiza. Wape wengine haki ya kutowatia hatiani kwa makosa, na puuza mawazo hasi.
Nani: _____
- Wasaidie marafiki zako:** Kuhudhuria tuu kwenye tukio la michezo ya rafiki zako au mchezo wa shule unaweza kuwasaidia kuhisi upendo wako.
Nani: _____
- Waalike wengine kujifunza kuhusu injili:** Hata kama hawakubali kile unachosema, wewe umeonesha kwamba unajali vya kutosha kushirikiana nao.
Nani: _____
- Fanya urafiki na watu wa aina mbali mbali:** Wengine wana mema mengi mno ya kushirikiana. Kristo alisaidia na kuwapenda watu wote bila kujali cho chote.
Nani: _____

Kueneza Injili

Tumia hizi kuelezea historia ya Kanisa!



Samuel Smith



Hyrum Smith



Parley P. Pratt

Baada ya Kanisa kuanzishwa, Baba wa Mbinguni alitaka kila mtu apate kujua kuhusu injili. Mmisionari wa kwanza alikuwa kaka yake Joseph Smith, Samuel, Hyrum, kaka mkubwa wa Joseph Smith, pia aliwafundisha wengine kuhusu injili. Siku moja mtu mmoja aliyeitwa Parley P. Pratt alimwambia Hyrum kuwa alikuwa ameshinda siku nzima akisoma Kitabu cha Mormoni. Hyrum alimfundisha zaidi kuhusu Kanisa, na kisha akabatizwa. Kisha Parley akahudumu misheni! Alikuwa kuwa kiongozi katika Kanisa.

Pata kujua zaidi kuhusu vigogo wa historia ya Kanisa hapa liahona.lds.org.



Kumfikiria Yesu

Na Lindsay Tanner

Imetokana na hadithi ya kweli

Mia alisisimka. Ilikuwa mara yake
ya kwanza kanisani! Wamisionari
waliieleza familia yake kuhusu Kanisa
hili. Wao waliamua kuja.

Mia aliangalia huku na huko. Aliona
nguo nyeupe juu ya meza. Kitu fulani
kilikuwa chini yake.

“Nini kipo chini ya nguo ile?” Mia
alimuuliza mmoja wa wamisionari.

Dada Hanson alitabasamu. “Ni
sakramenti.”

Sakramenti. Hilo lilikuwa neno
kubwa. Mia alikuwa amewasikia
wamisionari wakiwaambia Mama na

Baba yake kuhusu jambo hilo. Lakini
hakuwa na uhakika ilikuwa na nini.

Kila mtu aliimba wimbo. Watu
wawili waliifunua ile nguo nyeupe.
Sinia la mkate lililikuwa chini yake!
Mia aliwaona wakimega mkate
vipande vipande.

Baada ya wimbo mtu mmoja
mwanaume alisema maombi.
Wanaume wengine walipitisha
mkate kwa kila mtu.

“Mkate unatusaidia kukumbuka
mwili wa Yesu,” Dada Garcia
alinong’ona.



Mia alichukua kipande cha mkate. Alipiga picha akilini kuwa Yesu amesimama mbele yake.

Kisha kulikuwa na maombi mengine. Wanaume walipitisha sinia na vikombe vidogo vidogo vya maji.

“Maji yanatusaidia kukumbuka damu ya Yesu,” Dada Garcia alinong’ona. “Alikufa kwa ajili yetu kwa sababu Yeye anatupenda.”

Mia alichukua kikombe cha maji. Alifikiria ni kiasi gani Yesu alimpenda.

Alihisi kama alikuwa anamkumbatia kwa nguvu.


Baadaye Dada Hanson alimpa Mia picha ndogo ya Yesu. “Tunakula mkate na kunywa maji kumkumbuka Yesu na kuahidi kumfuata. Alitabasamu. “Ulifikiria nini kuhusu Sakramenti?”

Mia aliitazama picha ya Yesu. Alikumbuka hisia nzuri alizozipata. Alitabasamu. “Zilikuwa nzuri! Ninampenda Yesu.” ■

Mwandishi anaishi California, Marekani.

Yesu Alitupatia Sakramenti

Na Kim Webb Reid



Yesu alijua muda Wake duniani ulikuwa karibu umekwisha. Aliwakusanya Mitume Wake pamoja kwa ajili ya Karamu ya Mwisho. Aliwapatia sakramenti na kuwaambia daima wamkumbuke Yeye.



Yesu alikwenda kwenye bustani kuomba. Aliumia kwa dhambi zote na mambo ya kuhuzunisha katika maisha ya kila mtu. Kisha alikufa msalabani na alizikwa katika kaburi la kuchongwa.

Asubuhi ya Jumapili baada ya Yesu kufa, baadhi ya wanawake walikuja kaburini. Jiwe mlangoni lilikuwa limebingirishwa mbali, na kaburi lilikuwa tupu! Yesu alikuwa wapi?



Alikuwa hai tena! Mariamu Magdalena alimwona Yesu. Aliwatembelea Mitume wake ili wawe tayari kufundisha injili baada ya Yeye kurudi mbinguni.



Ninapochukuwa sakramenti, mimi humkumbuka Yesu.
Ninakumbuka kwamba Yeye aliishi na alikufa na akafufuka
kwa ajili yangu ili niweze kuishi tena! ■



Maua Meupe ya Pasaka



Maua meupe mazuri ya Pasaka yaweza kutukumbusha kuhusu ile siku ya ajabu wakati Yesu alipofufuka. Maua meupe matano yamefichika katika picha hii. Kila wakati utakapopata moja, sema kitu kimoja ambacho umejifunza juu ya Yesu.





Na Mzee Bruce R. McConkie (1915-1985)
 Wa Akidi ya Mitume
 Kumi na Wawili

NGUVU ZA MUNGU

Imani ni nguvu na nguvu ni ukuhani.

Mungu ni Mungu kwa sababu Yeye ni mfano wa imani yote na nguvu zote na ukuhani wote. Maisha aishiyo Yeye yanaitwa uzima wa milele.

Na kwa kiasi ambacho sisi tunakuwa kama Yeye ndiyo kiasi ambacho tunapata imani yake, tunapata nguvu Zake, na kuufanyia kazi ukuhani Wake. Na wakati inapokuwa tumekuwa kama Yeye katika ukamilifu na maana ya kweli, hapo nasi pia tutapata uzima wa milele.

Imani na ukuhani vinakwenda pamoja. Imani ni nguvu na nguvu ni ukuhani. Baada ya kuwa na imani, tunapokea ukuhani. Kisha, kupitia ukuhani, tunakua katika imani hadi, kupata nguvu zote, nasi tunakuwa kama Bwana wetu.

Muda wetu hapa katika mwili wenye kufa umetengwa rasmi kama muda wa maandalizi na kujaribiwa. Ni nafasi yetu tukiwa hapa kuikamilisha imani yetu na kukua katika nguvu za ukuhani. . . .

Ukuhani mtakatifu ulifanya zaidi katika kuwakamilisha wanadamu katika siku za Henoko kuliko wakati mwingine wo wote. Uljulikana kwa

wakati huo kama mfano wa Henoko (ona M&M 76:57), ilikuwa ni nguvu ambayo kwayo yeye na watu wake walihamishwa. Na walichukuliwa hai



kwa sababu walikuwa na imani na walitumia nguvu za ukuhani.

Alikuwa Henoko ambaye Bwana aliweka naye agano la milele kwa mba wale wote waliopokea ukuhani watakuwa na nguvu, kupitia imani, kuongoza na kusimamia vitu vyote duniani, kuweka ujasili kwa majeshi ya mataifa, na kusimama katika utukufu na kuinuliwa mbele za Bwana.

Melkizedeki alikuwa mtu wa imani ya jinsi hiyo, “na watu wake walitenda haki, na waliipata mbingu, na waliutafuta mji wa Henokoi” (Joseph Smith Tafsiri ya, Mwanzo 14:34). . . .

Ni nini, basi, mafundisho ya ukuhani? Na jinsi gani tunaweza kuishi kama watumishi wa Bwana?

Mafundisho haya ni kwamba Mungu Baba yetu ametukuka, mkamilifu, na

kiombe aliye inuliwa ambaye ana ukuu wote, nguvu zote, na mamlaka yote, ambaye anajua mambo yote na sifa zake zote hazina mwisho, na ambaye anaishi katika muundo wa familia.

Ni kwamba Baba yetu wa Milele anafurahia hali hii ya juu ya utukufu na ukamilifu na nguvu kwa sababu imani Yake ni kamilifu na ukuhani Wake hauna ukomo.

Ni kwamba ukuhani ni jina halisi la nguvu ya Mungu, na kwamba kama tunahitaji kuwa kama Yeye, lazima tupokee na kuutendea kazi ukuhani Wake au nguvu kama Yeye Anavyozitumia. . . .

Ni kwamba tuna nguvu, kwa imani, kutawala na kudhibiti mambo yote, vyote kimwili na kiroho; kutenda miujiza na kukamilisha maisha; kusimama mbele ya Mungu na kuwa kama Yeye kwa sababu sisi tumepata imani Yake, ukamilifu Wake, na nguvu Zake, au kwa maneno mengine ukamilifu wa ukuhani Wake.

Haya, basi, ndiyo mafundisho ya ukuhani, kuliko basi hakuna kitu wala hapawezi kuwa na kitu cho chote kilicho zaidi ya huu. Hii ndio nguvu tunayoweza kuipata kupitia imani na haki. . . .

Hakika kuna nguvu katika ukuhani—nguvu ambayo tunaitafuta kuipata ili kuitumia, nguvu ambayo tunaomba kwa bidii juu yetu na juu ya vizazi vyetu milele. ■

Kutoka katika hotuba ya kikao kikuu cha ukuhani yenye kichwa cha habari “Mafundisho ya Ukuhani,” Ensign, Mei 1982, 32-34; capitalization standardized.



**KONDOO WENGINE NINAO,
NA ELSPETH YOUNG**

Bwana mfukuka aliwatembelea “kondoo Wake wengine” (3 Nefi 15:21) katika mabara ya Amerika na sehemu nyingine. Wanefi “wakaona alama za misumari katika mikono yake na katika miguu yake; na hivi walifanya wakienda mbele mmoja mmoja, mpaka walipoenda wote, na waliona kwa macho yao na kupapasa kwa mikono yao, na walijua ukweli na walishuhudia wenyewe kwamba ni yeye, ambaye manabii waliandika kwamba anapaswa kuja” (3 Nefi 11:15).

Pia Katika Toleo Hili

KWA VIJANA WAKUBWA

Kuzielewa **Baraka Zako za Kipatriaki**

Baraka za Kipatriaki hazitumbii sisi kila kitu kitakacho tokea katika maisha yetu, bali zinatoa mwongozo ambao unaweza kusaidia kutuongoza sisi katika furaha kubwa ambayo Baba wa Mbinguni ameiweka kwa kila mmoja wetu.



uk.
44

KWA VIJANA



uk.
58

WALIMWONA **YEYE**

Walikuwa mashahidi wa Kristo mfufuka. Jinsi tunavyoweza kusimama kama mashahidi leo.

KWA WATOTO

Yesu Alitupatia Sakramenti

Tunachukua sakramenti kila wiki. Lakini watoto wako wanajua ni kwa nini?



uk.
76



SWAHILI

KANISA LA
YESU KRISTO
LA WATAKATIFU
WA SIKU ZA MWISHO